sahani Sahani zote ni safi sasa.

All the plates are clean now.

vikombe Vikombe vyote ni safi sasa.

All the cups are clean now.

visahani Visahani vyote ni safi sasa.

All the saucers are clean now.

bilauri Bilauri zote ni safi sasa.

All the glasses are clean now.

nguo Nguo zote ni safi sasa.

All the clothes are clean now.

C. Concord with pi.

vikombe Vikombe vipi si safi?

Which cups are not clean?

kikombe Kikombe kipi si safi?

Which cup is not clean?

sahani (pl.)	Sahani zipi si safi?	Which plates are not clean?
sahani	Sahani ipi si safi?	Which plate is not clean?
nguo	Nguo ipi si safi?	Which cloth is not clean?

D. Concord with ote.

bilauri	Mariamamu amevunja bilauri zote.	Mariamamu has broken all the glasses.
vyombo	Mariamamu amevunja vyombo vyote.	Mariamamu has broken all the dishes.
visahani	Mariamamu amevunja visahani vyote.	Mariamamu has broken all the saucers.
vikombe	Mariamamu amevunja vikombe vyote.	Mariamamu has broken all the cups.
sahani	Mariamamu amevunja sahani zote.	Mariamamu has broken all the plates.

3.

A. Concords in successive short sentences.

sahani moja	Sahani moja imeanguka. Ipi? Yako. Nani ameziangusha?	One plate has fallen. Which one? Yours. Who made it fall?
sahani mbili	Sahani mbili zimeanguka. Zipi? Zako. Nani ameziangusha?	Two plates have fallen. Which ones? Yours. Who made them fall?
kikombe kimoja	Kikombe kimoja kimeanguka. Kipi? Chako. Nani amekiangusha?	One cup has fallen. Which one? Yours. Who made it fall?
vikombe viwili	Vikombe viwili vimeanguka. Vipi?	Two cups have fallen. Which ones?

Vyako.

Yours.

Nani ameviangusha?

Who made them fall?

B. Neuter vs. simple stems; concord including object prefix.

kalamu Kalamu yangu imevunjika.

My pen is broken.

Nani ameivunja? or:

Who broke it?

Nani aliyeivunja?

bilauri Bilauri yangu imevunjika.

My glass is broken.

Nani ameivunja?

Who broke it?

kisahani Kisahani changu kimevunjika.

My saucer is broken.

Nani amekivunja?

Who broke it?

kikombe Kikombe changu kimevunjika.

My cup is broken.

Nani amekivunja?

Who broke it?

C. -kuwa ngapi?; concord with ngapi.

vikombe Vikombe safi vilikuwa vingapi?

How many clean cups were there?

Vilikuwa vîne.

There were four.

visahani Visahani safi vilikuwa vingapi?

How many clean saucers were

there?

Vilikuwa vîne.

There were four.

sahani Sahani safi zilikuwa ngapi?

How many clean plates were

there?

Zilikuwa ñne.

There were four.

bilauri Bilauri safi zilikuwa ngapi?

How many clean glasses were

there?

Zilikuwa ñne.

There were four.

D. Concord: Noun and two adjectives.

vikombe Kuna vikombe vipya vingapi?

How many new cups are there?

Kuna vitano.

There are five.

visahani Kuna visahani vipya vingapi?

How many new saucers are there?

Kuna vitano.

There are five.

kalamu	Kuna kalamu mpya ngapi? Kuna tano.	How many new pens are there? There are five.
nguo	Kuna nguo mpya ngapi? Kuna tano.	How many new cloths are there? There are five.
nyumba	Kuna nyumba mpya ngapi? Kuna tano.	How many new houses are there? There are five.

Unit 48

1. Basic Dialogue. Lighting the lamp.

Hamisi

giza (MA)

darkness

-ingia

to enter

Giza laingia.

It's getting dark.

taa (N)

a lighting device

(lamp, light bulb, etc.)

mafuta (pl. MA)

oil, grease

-washa

to cause to light up

Tafadhali, nipatie taa ya mafuta,

Please get me the lamp so I [can]

niwashe.

light [it].

Hadija

-chukua

to take, carry

Chukua taa. Nimeileta.

Here it is.

('Take it. I've brought it.')

Hamisi

Inayo mafuta ya kutosha?

Does it have enough oil?

Hadija

-tia

put, pour

chupa (N)

bottle

jioni

evening

Ndiyo, tulitia chupa mbili jana

Yes, we put in two bottles yesterday

jioni.

evening.

chakula	Wachukuzi wanacho chakula cha kutosha usiku huu?	Do the porters have enough food for tonight?
ninyi	Ninyi mnacho chakula cha kutosha usiku huu?	Do you have enough food for tonight?
watoto	Watoto wanacho chakula cha kutosha usiku huu?	Do the children have enough food for tonight?

D. -tia.

↓	Tutatia mafuta katika taa.	We will put oil into the lamp.
chupa	Tutatia mafuta katika chupa.	We will put oil into the bottle.
maji	Tutatia maji katika chupa.	We will put water into the bottle.
kikombe	Tutatia maji katika kikombe.	We will put water into the cup.
bilauri	Tutatia maji katika bilauri.	We will put water into the glass.
maziwa	Tutatia maziwa katika bilauri.	We will put milk into the glass.
chupa	Tutatia maziwa katika chupa.	We will put milk into the bottle.

E. Imperative plus subjunctive.

mafuta	Lete mafuta nitie katika chupa hii.	Bring oil for me to put into this bottle.
maziwa	Lete maziwa nitie katika chupa hii.	Bring milk for me to put into this bottle.
maji	Lete maji nitie katika chupa hii.	Bring water for me to put into this bottle.
wino	Lete wino nitie katika chupa hii.	Bring ink for me to put into this bottle.

3.

A. Imperative plus subjunctive.

kalamu	Mletee kalamu aitengeneze.	Bring him the pen so that he can fix it.
--------	----------------------------	---

kalamu (pl.)	Mletee kalamu azitengeneze.	Bring him the pens so that he can fix them.
baiskeli	Mletee baiskeli aitengeneze.	Bring him the bicycle so that he can fix it.
viti	Mletee viti avitengeneze.	Bring him the chairs so that he can fix them.
motokaa	Mletee motokaa aitengeneze.	Bring him the car so that he can fix it.
taa	Mletee taa aitengeneze.	Bring him the lamp so that he can fix it.

B. Second person plural object prefix.

vikombe	Juma aliwapatieni vikombe vingapi jana jioni? Hakutupatia vikombe vyo vyote!	How many cups did Juma get you yesterday evening? He didn't bring us any cup at all!
viazi	Juma aliwapatieni viazi vingapi jana jioni? Hakutupatia viazi vyo vyote!	How many potatoes did Juma get you yesterday evening? He didn't bring us any at all!
mayai	Juma aliwapatieni mayai mangapi jana jioni? Hakutupatia mayai yo yote!	How many eggs did Juma get you yesterday evening? He didn't bring us any egg at all!
maembe	Juma aliwapatieni maembe mangapi jana jioni? Hakutupatia maembe yo yote!	How many mangoes did Juma get you yesterday evening? He didn't bring us any mango at all!
mikate	Juma aliwapatieni mikate mingapi jana jioni?	How many loaves of bread did Juma bring you yesterday evening?

	Hakutupatia mikate yo yote!	He didn't bring us any loaf of bread at all!
taa	Juma aliwapatieni taa ngapi jana jioni? Hakutupatia taa zo zote!	How many lamps did Juma bring you yesterday evening? He didn't bring us any lamp at all!
chupa	Juma aliwapatieni chupa ngapi jana jioni? Hakutupatia chupa zo zote!	How many bottles did Juma bring you yesterday evening? He didn't bring us any bottle at all!
ng'ombe	Juma aliwapatieni ng'ombe wangapi jana jioni? Hakutupatia ng'ombe wo wote!	How many cattle did Juma bring you yesterday evening? He didn't bring us any cattle at all!

Conversation Starters

1. A (an employer) returns from a trip, and discusses the trip with B (a domestic servant).
2. A then questions B about the state of the house, the dishes, etc. in his absence, and about the adequacy of supplies for the immediate future.

Unit 49

1. Basic Dialogue. Lighting the lamp.

Son

kiberiti (VI)
(or: kibiriti)

box or book of matches

kijiti cha kiberiti (VI)

a single match

Tafadhali, nipatie kiberiti.

Please get me a match.

Mother

Viberiti vyote vimekwisha.

They're all gone.

Son

pesa (N)

coins

Unazo pesa za kumumua vingine?

Do you have money to buy some more?

Mother

senti (N) (or: pesa (N))

small change

sanduku (N)

box

Ndiyo. Chukua senti kutoka

Yes, take some change out of the

sandukuni.

box.

haraka (N)

haste

Na ufanye haraka. Giza laingia.

And hurry, it's getting dark.

('Darkness enters.')

Son

Ndiyo, mama.

Yes, Mother.

2.

A. Concords with ~pya.

kiberiti Tafadhali, nipatie kiberiti
kipya.

Please get me a new match.

viberiti	Tafadhali, nipatie viberiti vipya.	Please get me some new matches.
sanduku	Tafadhali, nipatie sanduku jipya.	Please get me a new box.
nguo	Tafadhali, nipatie nguo mpya.	Please get me some new clothes.
chupa	Tafadhali, nipatie chupa mpya.	Please get me a new bottle.
taa	Tafadhali, nipatie taa mpya.	Please get me a new lamp.

B. Meaning of me-tense of -(kw)isha.

viberiti	Viberiti vimekwisha, mama.	The matches are all used up, mother.
vikombe	Vikombe vimekwisha, mama.	The cups are all gone, mother.
siagi	Siagi imekwisha, mama.	The butter is all gone, mother.
sahani	Sahani zimekwisha, mama.	The plates are all gone, mother.
pesa	Pesa zimekwisha, mama.	The money is all gone, mother.
mafuta	Mafuta yamekwisha, mama.	The oil is all gone, mother.
maji	Maji yamekwisha, mama.	The water is all gone, mother.
njugu	Njugu zimekwisha, mama.	The ground nuts are all gone, mother.

C. ~a plus infinitive.

-nunua	Mnazo pesa za kununua mafuta?	Do you have money to buy oil?
-lipa	Mnazo pesa za kulipa kodi?	Do you have money to pay taxes?
-tosha	Mnazo pesa za kutosha?	Do you have money enough?

D. -chukua.

↓	Nani alichukua senti kutoka sandukuni?	Who took the change from the box?
---	--	-----------------------------------

kalamu	Nani alichukua kalamu kutoka sandukuni?	Who took the pen from the box?
meza	Nani alichukua kalamu kutoka mezani?	Who took the pen from the table (drawer)?
viberiti	Nani alichukua viberiti kutoka mezani?	Who took the matches from the table (drawer)?
nyumba	Nani alichukua viberiti kutoka nyumbani?	Who took the matches from the house?
motakaa	Nani alichukua viberiti kutoka motokaani?	Who took the matches from the car?
bilauri	Nani alichukua viberiti kutoka bilaurini?	Who took the matches from the glass?
mafuta	Nani alichukua mafuta kutoka bilaurini?	Who took the oil from the glass?
taa	Nani alichukua mafuta kutoka taani?	Who took the oil from the lamp?

3.

A. Multiple concords.

pesa	Unazo pesa za kutosha? Sina pesa zo zote.	Do you have enough money? I don't have any money at all.
senti	Unazo senti za kutosha? Sina senti zo zote.	Do you have enough change? I don't have any change at all.
mafuta	Unayo mafuta ya kutosha? Sina mafuta yo yote.	Do you have enough oil? I don't have any oil at all.
maji	Unayo maji ya kutosha? Sina maji yo yote.	Do you have enough water? I don't have any water at all.
mikate	Unayo mikate ya kutosha? Sina mikate yo yote.	Do you have enough bread? I don't have any bread at all.

uji	Unao uji wa kutosha? Sina uji wo wote.	Do you have enough gruel? I don't have any gruel at all.
nyama	Unayo nyama ya kutosha? Sina nyama yo yote.	Do you have enough meat? I don't have any meat at all.

B. Li-tense vs. past negative with -ku-.

kuchukua	Ulichukua senti ngapi kutoka sandukuni? Sikuchukua nyingi.	How many cents did you take out of the box? I didn't take many.
kuweka	Uliweka senti ngapi sandukuni? Sikuweka nyingi.	How many cents did you put into the box? I didn't put many.
kuona	Uliona senti ngapi sandukuni? Sikuona nyingi.	How many cents did you see in the box? I didn't see many.

C.

kuchukua	Mlichukua viberiti vingapi nyumbani? Hatukuchukua vingi.	How many matches did you (pl.) take out of the house? We didn't take many.
kuweka	Mliweka viberiti vingapi nyumbani? Hatukuweka vingi.	How many matches did you (pl.) put in the house? We didn't put many.
kuona	Mliona viberiti vingapi nyumbani? Hatukuona vingi.	How many matches did you (pl.) see in the house? We didn't see many.

Unit 50

1. Basic Dialogue. I'm not hungry.

Mother

Unakitaka chakula hiki?

Do you want this food?

Son

Hapana, sikitaki asante.

No, thank you.

Mother

wa nini?

Why [not]?

Son

-maliza

to finish

Kwa sababu sina njaa.

Because I'm not hungry. I've just

Nimemaliza kula sasa hivi.

now finished eating.

Mother

kinywaji (VI)

a drink

Pengine wataka kinywaji.

Maybe you'd like a drink.

Son

Ndiyo. Tafadhali nipatie bilauri

Yes, a glass of orange juice would

moja ya maji ya machungwa.

be fine.

Mother

-nywa

to drink

Basi chukua. Mimi nitakunywa soda.

Here you are. ('Then, take') I'll

have some soda.

Notes

A. The phrase sasa hivi.

Note the use of hivi, which has the form of the proximal demonstrative,

plural VI class, as modifier of sasa 'now' to produce sasa hivi 'just now.' The phrase hivi sasa is also used in this sense.

2.

A. Concord: Noun and demonstrative.

chakula	Unataka chakula hicho?	Do you want that food?
karanga	Unataka karanga hizo?	Do you want those ground nuts?
mkate	Unataka mkate huo?	Do you want that bread?
kinywaji	Unataka kinywaji hicho?	Do you want that drink?
siagi	Unataka siagi hiyo?	Do you want that butter?
nyama	Unataka nyama hiyo?	Do you want that meat?

B. -me-maliza plus infinitive.

-la	Juma amemaliza kula sasa hivi.	Juma has just now finished eating.
-leta	Juma amemaliza kuleta kinywaji sasa hivi.	Juma has just now finished bringing a drink.
-tuletea	Juma amemaliza kutuletea vinywaji sasa hivi.	Juma has just now finished bringing us drinks.
-fanya	Juma amemaliza kufanya kazi sasa hivi.	Juma has just now finished working.

C. hu-tense; concord with ~ingi.

chai	Watu wote wa nchi hii hunywa chai nyingi.	Everyone in this country drinks a lot of tea.
kahawa	Watu wote wa nchi hii hunywa kahawa nyingi.	Everyone in this country drinks a lot of coffee.
maziwa	Watu wote wa nchi hii hunywa maziwa mengi.	Everyone in this country drinks a lot of milk.
soda	Watu wote wa nchi hii hunywa soda nyingi.	Everyone in this country drinks a lot of soda.

maji ya machungwa	Watu wote wa nchi hii hunywa maji ya machungwa mengi.	Everyone in this country drinks a lot of orange juice.
----------------------	--	---

D.

nyama	Watu wengi wa nchi hii hula nyama nyingi.	Many people in this country eat a lot of meat.
karanga	Watu wengi wa nchi hii hula karanga nyingi.	Many people in this country eat a lot of ground nuts.
muhogo	Watu wengi wa nchi hii hula muhogo mwingi.	Many people in this country eat a lot of cassava.
mahindi	Watu wengi wa nchi hii hula mahindi mengi.	Many people in this country eat a lot of maize.

3.

A. Me-tense vs. negative with -ja-.

wewe	Umamaliza kula sasa? Hapana, sijamaliza bado.	Have you finished eating now? No, I haven't finished yet.
ninyi	Mmemaliza kula sasa? Hapana, hatujamaliza bado.	Have you all finished eating now? No, we haven't finished yet.
watu wote	Watu wote wamamaliza kula sasa? Hapana, hawajamaliza bado.	Has everyone finished eating now? No, they haven't finished yet.

B. Present affirmative vs. negative, with object prefix.

chakula	Unakitaka chakula hiki? Hapana, sikitaki, asante.	Do you want this food? No, I don't want it, thank you.
mkate	Unautaka mkate huu? Hapana, siutaki, asante.	Do you want this bread? No, I don't want it, thank you.
mikate	Unaitaka mikate hii? Hapana, siitaki, asante.	Do you want these loaves? No, I don't want them, thank you.

embe	Unalitaka embe hili? Hapana, silitaki, asante.	Do you want this mango? No, I don't want it, thank you.
maembe	Unayataka maembe haya? Hapana, siyataki, asante.	Do you want these mangoes? No, I don't want them, thank you.
ndizi	Unaitaka ndizi hii? Hapana, siitaki, asante.	Do you want this banana? No, I don't want it, thank you.
ndizi (pl.)	Unazitaka ndizi hizi? Hapana, sizitaki, asante.	Do you want these bananas? No, I don't want them, thank you.
kiazi	Unakitaka kiazi hiki? Hapana, sikitaki, asante.	Do you want this potato? No, I don't want it, thank you.
viazi	Unavitaka viazi hivi? Hapana, sivitaki, asante.	Do you want these potatoes? No, I don't want them, thank you.

C. Negative present of monosyllabic verb stem, with loss of ku-.

Mariamamu	Mariamamu anakula viazi? La, hali viazi, anakula mkate.	Is Mariamamu eating potatoes? No, she isn't eating potatoes. She's eating bread.
watoto	Watoto wanakula viazi? La, hawali viazi, wanakula mkate.	Are the children eating potatoes? No, they aren't eating potatoes. They are eating bread.
wewe	Unakula viazi? La, sili viazi, ninakula mkate.	Are you eating potatoes? No, I'm not eating potatoes. I'm eating bread.
ninyi	Mnakula viazi? La, hatuli viazi, tunakula mkate.	Are you all eating potatoes? No, we aren't eating potatoes. We're eating bread.

D.

Daudi	Daudi anakunywa kahawa? La, hanywi kahawa, anakunywa chai.	Is Daudi drinking coffee? No, he isn't drinking coffee. He's drinking tea.
-------	--	--

wote	Wote wanakunywa kahawa? La, hawanywi kahawa, wanakunywa chai.	Are they all drinking coffee? No, they aren't drinking coffee. They're drinking tea.
wewe	Unakunywa kahawa? La, sinywi kahawa, ninakunywa chai.	Are you drinking coffee? No, I'm not drinking coffee. I'm drinking tea.
ninyi	Mnakunywa kahawa? La, hatunywi kahawa, tunakunywa chai.	Are you (pl.) drinking coffee? No, we aren't drinking coffee. We're drinking tea.

Conversation Starters

1. A inquires of B about what the people of his country customarily eat and how they spend their leisure time. B replies, and asks similar questions about the people of A's country.

2. Within the limits of the vocabulary that has been met up to this point, give an account of a typical day in your own life. Do the same for a day in the life of a domestic servant.

Unit 51

1. Basic Dialogue. What grade are you in?

Magese

-soma

to read, study

darasa (MA)

class

Unasoma darasa gani mtoto?

What class are you in, [child]?

Juma

Niko katika darasa la tano.

I'm in Standard 5.

Magese

somo (MA)

an academic subject, a lesson

Wapenda masomo gani shuleni?

What subjects do you like in school?

Juma

hesabu (N)

arithmetic

dini (N)

religion

Napenda hesabu, Kiingereza, dini
na historia.

I like arithmetic, English, religion
and history.

Magese

-endelea

to continue

-tumaini

to hope

Watumaini kuendelea katika masomo?

Do you hope to continue in your
studies?

Juma

Mungu (MI)	God
-jalia	to assist (ordinarily in the sense of God's help)
mpaka	to, until
chuo (VI)	school, college
Mungu akinijalia nitaendelea katika masomo mpaka chuo cha juu.	If God helps me, I will go on in my studies to college.

Magese

mwishowe	finally
Mwishowe utafanya kazi gani?	What kind of work will you do after that?

Juma

siasa (N) (or: utetezi (U))	politics
Nitafanya kazi ya siasa.	I'm going into politics.

Notes

A. Juu with no possessive following it.

chuo cha juu higher school

Here, juu is used without a possessive or a linking -a following it.

cf. Note 35.C.

B. First and second person subject prefixes used with locative stems.

niko katika darasa la tano I'm in Standard 5.

The first-person and second-person subject pronouns as well as the third-person pronouns may be used before the stem -ko, and before -po and -mo:

yuko nyumbani	he's at home
yupo nyumbani	he's at the house
yumo nyumbani	he's in the house

The difference in meaning between -po and -ko is not sharply defined. Generally speaking, -po implies a more definite idea of the location, while -ko has to do more with the mere existence of something regardless of place. -mo implies location of something within something else.

2.

A. -endelea plus infinitive; mpaka.

-soma Utaendelea kusoma mpaka How late are you going to read?
saa ngapi?

-fanya Utaendelea kufanya kazi How late are you going to work?
mpaka saa ngapi?

-tembea -ogelea

B. -jua plus infinitive.

-ogelea Watoto wote wanajua Do all the children know how to
kuogelea? swim?

-soma -andika -sema

3.

A. Nouns with the same stem but different prefixes.

mpishi	Baba yake ni mpishi.	His father is a cook.
	Yeye afanya kazi ya upishi.	He does cooking.
mkulima	Baba yake ni mkulima.	His father is a farmer.
	Yeye afanya kazi ya ukulima.	He does farming.
mtetezi	Baba yake ni mtetezi.	His father is a politician.
	Yeye afanya kazi ya utetezi.	He does political work.

mpagazi	Baba yake ni mchukuzi Yeye afanya kazi ya kibarua.	His father is a porter. He does casual labor.
mwandishi	Baba yake ni mwandishi. Yeye afanya kazi ya uandishi.	His father is a secretary. He does secretarial work.

B. Personal subject prefixes with locative stems.

wewe	Uko wapi? Nimo nyumbani.	Where are you? I am in the house.
ninyi	Mko wapi? Tumo nyumbani.	Where are you (pl.)? We are in the house.
yeye	Yuko wapi? Yumo nyumbani.	Where is he? He is in the house.
wao	Wako wapi? Wamo nyumbani.	Where are they? They are in the house.

4. A asks B, a child, about his school work and about his chores at home.

Unit 52

1. Basic Dialogue. If you drink too much. . .

Mirambo

Mwone, yule mtu hawezi kutembea
vyema.

Look at him! That man can't walk
properly.

Sangai

pombe (N)

beer

Yeye anakwisha kunywa pombe.

He's been drinking beer.

('he has finished drinking beer')

Mirambo

Mwe unapenda kunywa pombe?

Do you like to drink it?

Sangai

wakati (U) (pl. nyakati)

time

Nyakati nyingine mimi hunywa kidogo
tu.

Sometimes I drink just a little.

Mirambo

-lewa

to become drunk

Pombe ni mbaya kwa sababu inamfanya
mtu alewe.

Beer is bad because it makes a person
(that he should become) drunk.

Sangai

Ndiyo. Mtu akinywa nyingi atalewa.

Yes, anyone who drinks much will get
drunk.

NotesA. The distal demonstratives (-le).

yule mtu that man over there

A third series of demonstratives are formed on the stem -le. The general meaning is 'that/those over there'. These may be called 'distal' demonstratives. The three series of demonstratives may be compared in the following table.

	'neutral'	'proximal'	'distal'
	<u>h</u> u y o	<u>h</u> u y u	y u <u>l</u> <u>l</u> <u>e</u>
WA	sg. <u>h</u> y <u>o</u>	<u>h</u> yu	y <u>u</u> <u>l</u> e
	pl. <u>h</u> a <u>o</u>	<u>h</u> awa	w <u>a</u> <u>l</u> e
MI	sg. <u>h</u> u <u>o</u>	<u>h</u> uu	<u>u</u> <u>l</u> e
	pl. <u>h</u> i <u>y</u> <u>o</u>	<u>h</u> ii	<u>i</u> <u>l</u> e
MA	sg. <u>h</u> i <u>l</u> <u>o</u>	<u>h</u> ili	<u>l</u> i <u>l</u> e
	pl. <u>h</u> a <u>y</u> <u>o</u>	<u>h</u> aya	y <u>a</u> <u>l</u> e
VI	sg. <u>h</u> i <u>ch</u> <u>o</u>	<u>h</u> iki	<u>k</u> i <u>l</u> e
	pl. <u>h</u> i <u>v</u> <u>y</u> <u>o</u>	<u>h</u> ivi	<u>v</u> i <u>l</u> e
N	sg. <u>h</u> i <u>y</u> <u>o</u>	<u>h</u> ii	<u>i</u> <u>l</u> e
	pl. <u>h</u> i <u>z</u> <u>o</u>	<u>h</u> izi	<u>z</u> i <u>l</u> e
U	<u>h</u> uo	<u>h</u> uu	<u>u</u> <u>l</u> e
PA ('mahali')	hapo	hapa	<u>p</u> a <u>l</u> e
KU	huko	huku	<u>k</u> u <u>l</u> e
MU	humu	humu	<u>m</u> u <u>l</u> e

B. The ki-tense.

mtu akinywa nyingi atalewa	if a person drinks much he will get drunk
Mungu akinijalia . . .	if God helps me . . .

These sentences contain verb forms with the prefix ki-. This prefix stands between the subject and object prefixes, and in this respect resembles the tense prefixes na-, li-, etc. A crude but serviceable kind of translation equivalent for the ki- form is 'he drinking', 'he helping', 'I being', etc. Forms with ki- in this slot do not ordinarily serve as the main verb in a complete sentence.

2.

A. weza plus infinitive; le.

-tembea	Wale watu hawawezi kutembea vyema.	Those people cannot walk well.
-soma	Wale watu hawawezi kusoma vyema.	Those people cannot read well.
-sema	-andika	

B. Kidogo after mass nouns.

pombe	Nyakati nyingine mimi hunywa pombe kidogo.	Sometimes I drink a little beer.
kahawa	Nyakati nyingine mimi hunywa kahawa kidogo.	Sometimes I drink a little coffee.
chai	Nyakati nyingine mimi hunywa chai kidogo.	Sometimes I drink a little tea.
maji	Nyakati nyingine mimi hunywa maji kidogo.	Sometimes I drink a little water.

C. Two examples of the ki-tense.

akienda	Mtoto akienda shuleni hujifunza kusoma.	If a child goes to school, he learns how to read.
---------	---	---

ukifanya Ukifanya kazi vizuri sana
utapata mshahara wa kutosha.

If you work very well you will
get enough pay.

D. Mara.

kuona Ulimwona mara ngapi? Mara
mbili.

How many times did you see him?
Twice.

kusaidia Ulimsaidia mara ngapi? Mara
mbili.

How many times did you help him?
Twice.

kusikia Ulimsikia mara ngapi? Mara
mbili.

How many times did you hear him?
Twice.

kutazama Ulimtazama mara ngapi?
Mara mbili.

How many times did you look at
him? Twice.

E. -fanya plus subjunctive.

chai Chai hai mfanyi mtu alewe.

Tea does not make one drunk.

kahawa Kahawa hai mfanyi mtu alewe.

Coffee does not make one drunk.

maji Maji hai mfanyi mtu alewe.

Water does not make one drunk.

maji ya Machungwa hai mfanyi
mtu alewe.

Orange juice does not make one
drunk.

3.

A. Concords: Noun and adjectives.

pombe Pombe ni nzuri? Hapana, ni
mbaya.

Is the beer good? No, it is bad.

vyakula Vyakula ni vizuri? Hapana,
ni vibaya.

Are the foods good? No, they are
bad.

nyama Nyama ni nzuri? Hapana, ni
mbaya.

Is the meat good? No, it is bad.

maembe Maembe ni mazuri? Hapana,
ni mabaya.

Are the mangoes good? No, they
are bad.

machungwa Machungwa ni mazuri? Hapana,
ni mbaya.

Are the oranges good? No,
they are bad.

ndizi Ndizi ni nzuri? Hapana, ni
mbaya.

Are the bananas good? No,
they are bad.

Unit 53

1. Basic Dialogue. Juma hurt his leg.

Asha

ndugu (N-pers.)

kinsman of same generation

Baba, ndugu yangu Juma yuko wapi?

Father, where is my ndugu Juma?

Hamisi

Alipelekwa hospitalini na mama.
(or:...hospitali...)

He was taken to the hospital by [his]
mother.

Asha

Kwa nini?

Why?

Hamisi

-umia

be hurt

mkono (MI)

arm, hand

mguu (MI)

leg, foot

Kwa sababu aliumia mkono na mguu.

Because he hurt [his] arm and [his]
foot.

Asha

Aliumiaje?

How did he get hurt?

Hamisi

kisu (VI)

knife

Alijiuniza mwenyewe kwa kisu.

He hurt himself with a knife.

Asha

mgonjwa (WA)

a sick person

Yeye mgonjwa sana?

Is he very ill?

Hamisi

Hapana, lakini alikuwa akiumwa.

No, but he was in pain.

Notes

A. Passive stems.

Ndugu yangu aliniuma.	My brother bit me.
Niliumwa na ndugu yangu.	I was bitten by my brother.
Ndugu yangu aliniumiza.	My brother hurt me.
Niliumizwa na ndugu yangu.	I was hurt by my brother.

Passive stems may be derived from simple stems, or from other derived stems, by use of a suffix whose most common form is -w-. When the passive suffix is used in the same word with another derivational suffix, it follows that suffix.

In sentences containing passive verbs, the word for the agent or means by which the action is performed follows the word na.

B. Passive stems formed on roots which contain vowels.

Wachukuzi walikula nyama.	The porters ate the meat.
Nyama ililiwa na wapagazi.	The meat was eaten by the porters.
Maziwa yamenywewa na watoto.	The milk has been drunk by the children.

Passive stems derived from monosyllabic verbs do not have ku-, and the passive suffix itself is -iw- or -ew-. For details see the exercises.

C. Difference in meaning between -umwa and -umia.

Nilium <u>wa</u> (na) kichwa.	I had a headache.
Nilium <u>ia</u> kichwa.	I hurt my head.

Note the difference in meaning between the derived verb stems in the above examples. The underlying simple stem -uma means 'to cause pain, injure, bite'.

The word na is used by some speakers after -umwa, but is omitted by others.

D. The reflexive prefix -ji-.

Ninajifunza Kiswahili.	I'm studying Swahili.
Nilimwumiza Daudi.	I hurt Daudi.
Nilijiumiza.	I hurt myself.
Walijiumiza.	They hurt themselves.

The prefix -ji- occupies the same slot as the other object prefixes. It is a 'reflexive' prefix, which indicates that the object of the verb is the same as its subject. It has the invariable shape -ji- regardless of the person, class or number of the subject.

The stem -funza means 'to teach'. -jifunza 'to study, learn' is literally 'to teach oneself'.

2.

A. -umia.

m̄guu	Juma aliumia m̄guu.	Juma hurt his leg.
miguu	Juma aliumia miguu.	Juma hurt his legs.
m̄kono	Juma aliumia m̄kono.	Juma hurt his hand.
mikono	Juma aliumia mikono.	Juma hurt his hands.
kichwa	Juma aliumia kichwa.	Juma hurt his head.

B. -aumwa.

kichwa	Juma anaumwa kichwa.	Juma has a headache.
m̄guu	Juma anaumwa m̄guu.	Juma has a sore foot.
miguu	Juma anaumwa miguu.	Juma's feet hurt.
m̄kono	Juma anaumwa m̄kono.	Juma has a sore arm.

C. -jiumiza.

kisu	Nilijiumiza kwa kisu.	I hurt myself with a knife.
kiti	Nilijiumiza kwa kiti.	I hurt myself with a chair.

bilauri baiskeli kalamu

D. Kuna plus locative.

↓	Kuna wagonjwa wengi hospitalini?	Are there many patients in the hospital?
mtu	Kuna watu wengi hospitalini?	Are there many people in the hospital?
mji	Kuna watu wengi mjini?	Are there many people in town?
mgonjwa	Kuna wagonjwa wengi mjini?	Are there many sick people in town?
mtoto	Kuna watoto wengi mjini?	Are there many children in town?
shule	Kuna watoto wengi shuleni?	Are there many children in the school?

E. -wa plus ki-tense.

kufanya	Ulikuwa ukifanya nini saa sita mchana?	What were you doing at twelve noon?
kula	Ulikuwa ukila chakula saa sita mchana?	Were you eating at twelve noon?
kusoma	Ulikuwa ukisoma saa sita mchana?	Were you reading at twelve noon?
kutembea	Ulikuwa ukitembea saa sita mchana?	Were you walking at twelve noon?
kuandika	Ulikuwa ukiandika barua saa sita mchana?	Were you writing a letter at twelve noon?

F. Concord: Noun, adjective, subject prefix.

nguo mpya	Nguo mpya zilipelekwa hospitali.	New clothes were ^{taken} _{sent} to the hospital.
mayai	Mayai yalipelekwa hospitali.	Eggs were taken to the hospital.
maziwa	ndizi vyakula vyote	

mahindi	Mahindi yote yalipelekwa sokoni.	All the maize was taken to the market.
muhogo	Muhogo wote ulipelekwa sokoni.	All the cassava was taken to the market.

mayai njugu nguruwe maembe mazima

H. Passive plus na.

baba	Kodi ililipwa jana na baba yangu.	The tax was paid yesterday by my father.
------	-----------------------------------	--

mama ndugu

I. -wa plus na-tense.

kichwa	Jana nilikuwa ninaumwa kichwa.	Yesterday, I had a headache.
ngu	Jana nilikuwa ninaumwa ngu.	Yesterday, I had a sore foot.
mkono	Jana nilikuwa ninaumwa mkono.	Yesterday, I had a sore arm.
vitu	Vitu hivi vyote vimeletwa na ndugu yangu.	All these things have been brought by my brother.
visu	Visu hivi vyote vimeletwa na ndugu yangu.	All these knives have been brought by my brother.
viti	machungwa mayai njugu ndizi nyama siagi	
mikate		

3.

A. Passive of verbs whose roots contain no vowel.

pombe	Pombe yote imenywewa. Nani ameinywa?	All the beer has been drunk. Who has drunk it?
chai	Chai yote imenywewa. Nani ameinywa?	All the tea has been drunk. Who has drunk it?
kahawa	Kahawa yote imenywewa. Nani ameinywa?	All the coffee has been drunk. Who has drunk it?

soda	Soda yote imenywewa. Nani ameyinywa?	All the soda has been drunk. Who has drunk it?
maji	Maji yote yamenywewa. Nani ameyanywa?	All the water has been drunk. Who has drunk it?
B.		
viazi	Viazi vyote vimeliwa. Nani amevila?	All the potatoes have been eaten. Who has eaten them?
maembe	Maembe yote yameliwa. Nani ameyala?	All the mangoes have been eaten. Who has eaten them?
mkate	Mkate wote umeliwa. Nani ameula?	All the bread has been eaten. Who has eaten it?
mikate	Mikate yote imeliwa. Nani ameila?	All the loaves of bread have been eaten. Who has eaten them?
nyama	Nyama yote imeliwa. Nani ameila?	All the meat has been eaten. Who has eaten it?
samaki	Samaki yote imeliwa. Nani ameila?	All the fish has been eaten. Who has eaten it?

Conversation Starters

1. A and his friend B, who are parents, discuss the things that they do for their children, related to their needs for food, clothing, education.

Unit 54

1. Basic Dialogue. Where have you been recently?

Sangai

Habari za siku nyingi?

How have you been all this time?

('News of many days?')

Mirambo

Njema.

Fine!

Sangai

Ulikuwa wapi siku hizi zote?

Where have you been all these days?

Mirambo

Nilikuwa huko Mbeya.

I was at Mbeya.

Sangai

Ulikuwa ukifanya nini?

What were you doing?

Mirambo

Nilikuwa nikifanya kazi ya ukarani.

I was doing clerical work.

Notes

A. Huko with names of places.

Tulikuwa nyumbani.

We were at home.

Tulikuwa huko Mbeya.

We were at Mbeya.

The locative suffix -ni is used with such words as nyumba 'house' and soko 'market'. With names of cities the word huko 'there' or hapa 'here' may be used. The literal translation of the second sentence is thus 'we were there [at] Mbeya'.

B. Verb phrases in which the first verb is -wa.

Nilikuwa nikifanya kazi.	I was working.
Atakuwa akifanya kazi.	He will be working.
Alilewa.	He got drunk.
Alikuwa amelewa.	He was drunk.
Amelewa.	He is drunk.
Ilikuwa imevunjika.	It was broken [when I saw it].

Verb phrases of this kind lend great flexibility to the expression of time and aspect with Swahili verbs. Basically, the action as a whole is located in past or future time by the use of -li- or -ta- as prefix with -wa. The shape of the action, whether continuing or completed at that time, is indicated by the use of -na-, -ki-, or of -me- as prefix for the second verb.

2.

A. Huko with names of cities.

Mbeya	Tulikuwa huko Mbeya.	We were at Mbeya.
Utete	Tulikuwa huko Utete.	We were at Utete.
soko	Tulikuwa sokoni.	We were at the market.
kanisa	Tulikuwa kanisani.	We were at the church.
Nairobi	Tulikuwa huko Nairobi.	We were in Nairobi.

B. -wa plus ki-tense.

kwenda	Nilikuwa nikienda nyumbani.	I was going home.
kula	Nilikuwa nikila chungwa.	I was eating an orange.
kujifunza	Nilikuwa nikijifunza Kiswahili.	I was learning Swahili.
kuondoka	Nilikuwa nikiondoka shuleni.	I was leaving school.
kuogelea	Nilikuwa nikiogelea.	I was swimming.

kusaidia Nilikuwa nikiwasaidia I was helping my parents.
wazazi wangu.

3.

A. Lini?

wao	Waendeleo kusoma mpaka saa saba. Walianza lini kusoma?	Let them go on reading till one o'clock. When did they begin reading?
yeye	Aendeleo kusoma mpaka saa saba. Alianza lini kusoma?	Let him/her go on reading till one o'clock. When did he/she begin reading?
wao	Waendeleo kuogelea mpaka saa saba. Walianza lini kuogelea?	Let them go on swimming till one o'clock. When did they begin swimming?
yeye	Aendeleo kuogelea mpaka saa saba. Alianza lini kuogelea?	Let him/her go on swimming till one o'clock. When did he/she begin swimming?
wao	Waendeleo kutusaidia mpaka saa saba. Walianza lini kutusaidia?	Let them go on helping us till one o'clock. When did they begin helping us?
yeye	Aendeleo kutusaidia mpaka saa saba. Alianza lini kutusaidia?	Let him/her go on helping us till one o'clock. When did he/she begin helping us?

B. -wa plus ki-tense: negative vs. affirmative.

wewe	Ulikuwa ukisoma? Hapana. Sikuwa nikisoma, nilikuwa nikiandika.	Were you (sg.) reading? No, I was not reading, I was writing.
ninyi	Mlikuwa mkisoma? Hapana. Hatukuwa tukisoma, tulikuwa tukiandika.	Were you (pl.) reading? No, we were not reading, we were writing.

karani	Karani alikuwa akisoma? Hapana. Hakuwa akisoma, alikuwa akiandika.	Was the clerk reading? No, he was not reading, he was writing.
C.		
wazungu	Wazungu hao walikuwa wakinywa chai? Hawakuwa wakinywa chai. Walikuwa wakinywa pombe.	Were those Europeans drinking tea? They were not drinking tea, they were drinking beer.
mzungu	Mzungu huyo alikuwa akinywa chai? Hakuwa akinywa chai. Alikuwa akinywa pombe.	Was that European drinking tea? He was not drinking tea, he was drinking beer.
wakulima	Wakulima hao walikuwa wakinywa chai? Hawakuwa wakinywa chai. Walikuwa wakinywa pombe.	Were those farmers drinking tea? They were not drinking tea, they were drinking beer.
ninyi	Mlikuwa mkinywa chai? Hatukuwa tukinywa chai. Tulikuwa tukinywa pombe.	Were you drinking tea? We were not drinking tea, we were drinking beer.

Unit 55

1. Basic Dialogue. How's the family?

Hasani

Habari gani za watoto wako?

How are your children?

Hadija

Hawajambo.

They're all right.

Hasani

kweli

true

Kweli, una watoto wangapi sasa?

Really, how many children do you
have now?Hadija

Nina watoto watatu.

I have three.

Hasani

kiume (VI)

the male sort

kike (VI)

the female sort

Watoto hao ni wa kiume au wa kike?

Are they boys or girls?

Hadija

mwanamke (pl. wanawake)

woman

mwanamume (pl. wanaume)

man

Mmoja ni mwanamke na wawili ni
wanaume.

One is a girl and two are boys.

Hasani

umri (U)

age

Mtoto wako mkubwa ana umri gani?

What is the age of your eldest?
('...your big [one]')

Hadija

Ana miaka kumi na mitatu sasa. Thirteen.

Notes

A. Numerals which take concordial prefixes.

Ana miaka mitano. He is five years old.

Ana miaka sita. He is six years old.

The numerals from 1 - 5, and also 8, take concordial prefixes. None of the other numerals do so.

B. Stating the ages of persons.

Note that the way of stating ages, as in the above examples, is literally 'he has (five) years'.

2.

A. Numbers and ages.

5	Mtoto wangu mkubwa ana miaka mitano sasa.	My eldest child is five years old now.
6	Mtoto wangu mkubwa ana miaka sita sasa.	My eldest child is six years old now.
7	Mtoto wangu mkubwa ana miaka saba sasa.	My eldest child is seven years old now.
8	Mtoto wangu mkubwa ana miaka minane sasa.	My eldest child is eight years old now.
9	Mtoto wangu mkubwa ana miaka tisa sasa.	My eldest child is nine years old now.
10	Mtoto wangu mkubwa ana miaka kumi sasa.	My eldest child is ten years old now.
11	Mtoto wangu mkubwa ana miaka kumi na mmoja sasa.	My eldest child is eleven years old now.

12 Mtoto wangu mkubwa ana miaka My eldest child is twelve years
kumi na miwili sasa. old now.

13 14 15 16 17 18 19

3.

A. The double plurals; subjunctive.

↓	Wanaume waende shuleni; wanawake wakae nyumbani.	The men are to go to school, the women are to stay home.
soko	Wanaume wakae nyumbani; wanawake waende sokoni.	The men are to stay home, the women are to go to the market.
kanisa	Wanaume wakae sokoni; wanawake waende kanisani.	The men are to stay at the market, the women are to go to church.
boma	Wanaume wakae kanisani; wanawake waende bomani.	The men are to stay at church, the women are to go to the District Office.
shule	Wanaume wakae bomani; wanawake waende shuleni.	The men are to stay at the District Office, the women are to go to school.

B. Double singular vs. double plural.

mwanamke	Kuna mwanamke mmoja nyumbani. Kuna wanawake wengi shuleni.	There is one woman at home. There are many women at school.
mwanamume	Kuna mwanamume mmoja nyumbani. Kuna wanaume wengi shuleni.	There is one man at home. There are many men at school.
mkulima	Kuna mkulima mmoja nyumbani. Kuna wakulima wengi shuleni.	There is one farmer at home. There are many farmers at school.
mtoto	Kuna mtoto mmoja nyumbani. Kuna watoto wengi shuleni.	There is one child at home. There are many children at school.
karani	Kuna karani mmoja nyumbani. Kuna makarani wengi shuleni.	There is one clerk at home. There are many clerks at school.

Conversation Starters

1. A and his friend B, who are parents, exchange information about the ages of their respective children, the grades that the children are in at school, and their favorite subjects.

Unit 56

1. Basic Dialogue. When are you coming to see us?

Mirambo

-amkia

to greet, visit

Utakuja lini kutuamkia?

When are you coming to visit us?

Magese

nafasi (N)

opportunity

Jumatano

Wednesday

pamoja na

together with

mke (WA)

wife

Nikipata nafasi, nitakuja siku ya

If I get a chance, I'll come on

Jumatano pamoja na mke wangu na

Wednesday along with my wife

watoto.

and children.

Mirambo

baada (N)

after

livu (N)

leave time

Baada ya livu yako, utakwenda wapi?

Where are you going when your

leave is over?

Magese

labda

perhaps

-rudi

to return

hakika (N)

certainty

Labda nitarudi tena Mbeya, lakini

I may go back to Mbeya again, but

sina hakika.

I'm not sure.

Notes

A. The days of the week.

Jumamosi	Saturday
Jumapili	Sunday
Jumatatu	Monday
Jumaane	Tuesday
Jumatano	Wednesday
Alhamisi	Thursday
Ijumaa	Friday

Given above are the days of the week in Swahili. When naming them in series it is customary to begin with Jumamosi. The terminations -mosi, -pili, etc. are related to forms meaning respectively 'one' and 'two'. Saturday is thus 'day-one', and Tuesday is 'day-four'.

B. The noun baada.

The noun baada, like juu, does not serve as subject or object of a verb, nor occur in the plural.

2.

A. -amkia.

wazazi	Umekuja hapa kuwaamkia wazazi wako?	Have you come here to visit your parents?
rafiki	Umekuja hapa kumwaamkia rafiki yako?	Have you come here to visit your friend?
jamaa	Umekuja hapa kumwaamkia jamaa yako?	Have you come here to visit your companion?
baba	Umekuja hapa kumwaamkia baba yako?	Have you come here to visit your father?
ndugu	Umekuja hapa kumwaamkia ndugu yako?	Have you come here to visit your brother?

B. -pata nafasi.

kusoma	Sikupata nafasi ya kusoma darasa la saba.	I did not have the opportunity of studying the seventh grade.
kusema	Sikupata nafasi ya kusema na Mwandishi Mkuu.	I did not have the opportunity of speaking to the General Secretary.
kuendelea	Sikupata nafasi ya kuendelea na masomo.	I did not have the opportunity of continuing with [my] studies.
kujifunza	Sikupata nafasi ya kujifunza hesabu.	I did not have the opportunity of learning arithmetic.
kuona	Sikupata nafasi ya kuona mashindano ya farasi.	I did not have the opportunity of watching the horse races.

C. pamoja na

mke	Nilikwenda Mbeya pamoja na mke wangu.	I went to Mbeya together with my wife.
mtoto	Nilikwenda Mbeya pamoja na mtoto wangu mkubwa.	I went to Mbeya together with my eldest child.
Mwandishi Mkuu	Nilikwenda Mbeya pamoja na Mwandishi Mkuu.	I went to Mbeya together with the General Secretary.
rafiki	Nilikwenda Mbeya pamoja na rafiki yangu.	I went to Mbeya together with my friend.
wachukuzi	Nilikwenda Mbeya pamoja na wachukuzi wengine.	I went to Mbeya together with some porters.

D. 'Future progressive.' -ta- plus -ki-.

mimi	Baada ya mwaka huu, nitakuwa nikiishi Kenya.	After this year I shall be living in Kenya.
sisi	Baada ya mwaka huu, tutakuwa tukiishi Kenya.	After this year we will be living in Kenya.
yeye	Baada ya mwaka huu, atakuwa akiishi Kenya.	After this year he will be living in Kenya.

wao	Baada ya mwaka huu, watakuwa wakiishi Kenya.	After this year they will be living in Kenya.
wewe?	Baada ya mwaka huu, utakuwa ukiishi Kenya?	After this year will you (sg.) be living in Kenya?
niryi?	Baada ya mwaka huu, mtakuwa mkiishi Kenya?	After this year will you (pl.) be living in Kenya?

3.

A. Me-tense, affirmative vs. negative.

kurudi	Daudi amerudi nyumbani? Hapana, hajarudi bado.	Has Daudi gone back home? No, he hasn't gone back yet.
kwanza	Daudi ameanza kusoma? Hapana, hajaanza bado.	Has Daudi begun reading? No, he hasn't begun yet.
kumaliza	Daudi amemaliza kusoma? Hapana, hajamaliza bado.	Has Daudi finished reading? No, he hasn't finished yet.
kula	Daudi amekula maharagwe? Hapana, hajala bado.	Has Daudi eaten beans? No, he hasn't eaten yet.
kwisha	Churvi imekwisha? Hapana, haijaisha bado.	Is the salt all gone? No, it isn't all gone yet.

B. Ta-tense, affirmative vs. negative.

wewe	Utapata nafasi ya kutuamkia? Hapana. Sitapata nafasi.	Will you have a chance to come to see us? No, I will not have a chance.
ninyi	Mtapata nafasi ya kutuamkia? Hapana. Hatutapata nafasi.	Will you (pl.) have a chance to come to see us? No, we will not have a chance.
wewe	Utaendelea katika masomo? Hapana. Sitaendelea.	Will you continue with your studies? No, I will not continue.

ninyi Mtaendelea katika masomo?

Hapana, hatutaendelea.

Will you (pl.) continue with your studies?

No, we will not continue.

wewe Utalipa vitu hivyo?

Hapana, sitalipa.
(or: Sitavilipa)

Will you pay for those things?

No, I will not pay for them.

ninyi Mtalipa vitu hivyo?

Hapana, hatutalipa.

Will you (pl.) pay for those things?

No, we will not pay for them.

Unit 57

1. Basic Dialogue. Where will you go after your leave?

Mirambo

-rudishwa

to be caused to return

Unadhani utarudishwa tena hapa?

Do you think you will be sent back
here?

Magese

maana

meaning, significance; because

-ahidi

to promise

kwamba

that ('saying')

-hama

to move from one place to
another

Sichani, maana nimekwisha ahidiwa
kwamba nitahamishwa.

I don't think so, because I've already
been promised that I'll be moved.

Mirambo

ungependa

you would like

Unadhani ungependa kurudi hapa?

Do you think you would like to return
here?

Magese

Ndiyo. Ningefurahi sana.

Yes, I would be very happy.

Mirambo

-kosa

to lack, err

Asante sana. Na tafadhali usikose
kuja siku hiyo ya Jumatano!

Thanks very much. And please don't
fail to come on [that] Wednesday
[that we talked about].

Notes

A. Statements in indirect discourse.

Unadhani kwamba utarudishwa?	} Do you think you will be returned?
Unadhani kuwa utarudishwa?	
Unadhani utarudishwa?	

These three sentences are freely interchangeable with one another. That is, a statement in indirect discourse may follow the preceding verb directly, or it may be introduced by kuwa or kwamba.

2.

A. -hama.

Mbeya	Mwaka jana tulihama (kutoka) Mbeya.	We moved from Mbeya last year.
kaskazini	Mwaka jana tulihama (kutoka) kaskazini.	We moved from the north last year.
kusini	Mwaka jana tulihama (kutoka) kusini.	We moved from the south last year.
mashariki	Mwaka jana tulihama (kutoka) mashariki.	We moved from the east last year.
magharibi	Mwaka jana tulihama (kutoka) magharibi.	We moved from the west last year.

B. -hamisha.

Tanga	Serikali ilituhamisha mpaka Tanga.	The government moved us to Tanga.
mji mpya	Serikali ilituhamisha mpaka mji mpya.	The government moved us to a new town.
kijiji kidogo	Serikali ilituhamisha mpaka kijiji kidogo.	The government moved us to a small village.

jimbo jingine	Serikali ilituhamisha mpaka jimbo jingine.	The government moved us to a different district.
C. <u>-kosa</u> plus infinitive.		
kuja	Msikose kuja siku ya Jamatano.	Don't fail to come on Wednesday.
kuamkia	Msikose kuwaamkia wazazi wenu.	Don't fail to welcome your parents.
kusoma	Msikose kusoma barua hii.	Don't fail to read this letter.
kurudisha	Msikose kurudisha visahani vyote.	Don't fail to return all the saucers.
kuendelea	Msikose kuendelea katika kazi yenu.	Don't fail to continue with your work.

D. -kosa plus noun.

mvua	Mwaka huu tumekosa mvua.	We have been short of rain this year.
matunda	Mwaka huu tumekosa matunda.	We have been short of fruit this year.
nazi	Mwaka huu tumekosa nazi.	We have been short of coconuts this year.
mboga	Mwaka huu tumekosa mboga.	We have been short of vegetables this year.

3.

A. Adjective vs. related causative stem.

chakula	Chakula tayari? Hapana. Nitakitayarisha sasa hivi.	Is the food ready? No, I will prepare it right away.
nguo	Nguo tayari? Hapana. Nitaitayarisha sasa hivi.	Is the dress ready? No, I will get it ready right away.

kahawa	Kahawa tayari? Hapana. Nitaitayarisha sasa hivi.	Is the coffee ready? No, I will get it ready right away.
uji	Uji tayari? Hapana. Nitautayarisha sasa hivi.	Is the gruel ready? No, I will get it ready right away.
ng'ombe	Ng'ombe tayari? Hapana. Nitamtayarisha sasa hivi.	Is the cow ready? No, I will get it ready right away.

B.

vyombo	Vyombo vyote ni safi? Hapana. Nitavisafisha sasa.	Are all the dishes clean? No, I will clean them now.
vikombe	Vikombe vyote ni safi? Hapana. Nitavisafisha sasa.	Are all the cups clean? No, I will clean them now.

sahani bilauri taa

C. Causative vs. causative plus passive.

vyombo	Rudisha vyombo nyumbani sasa. Vimekwisha rudishwa tayari. Nani amevirudisha?	Return the utensils to the house now. They have been returned already. Who returned them?
vitunguu	Rudisha vitunguu nyumbani sasa. Vimekwisha rudishwa tayari. Nani amevirudisha?	Return the onions to the house now. They have been returned already. Who has returned them?
njugu	maharagwe muhogo	

Unit 58

1. Basic Dialogue. Why didn't you come to see us?

Mirambo

mbona?

why?

Mbona hukuja siku ile ya Jumatano?

Why didn't you come that Wednesday?

Magese

-sikitika

to be sorry

homa (N)

fever

Ah! Nasikitika sana. Mke wangu
alipata homa.

Oh, I'm very sorry. My wife got a
fever.

Mirambo

Homa gani?

What kind of fever?

Magese

Sijui kwa hakika, lakini nadhani ni
malaria.

I'm not sure, but I think it is
malaria.

Mirambo

Ulimpeleka hospitali?

Did you take her to the hospital?

Magese

kidonge (VI)

tablet, pills

-piga

to hit

sindano (N)

needle

-pigwa sindano

to get an injection

Ndiyo. Alipata dawa ya vidonge,
na pia alipigwa sindano.

Yes, she got some pills and also was
given a shot.

Notes

A. Concordial agreement involving numeral phrases.

mananasi kumi na mawili	twelve pineapples
watoto kumi na wawili	twelve children

In numeral phrases which end with the numbers 1 - 5, or 8, the word for 1 - 5 or 8 must agree concordially with the noun to which the whole phrase refers. The first numeral in the phrase (kumi 'ten' in these examples) takes no concordial prefixes.

2.

A. Concord: Nouns with number over ten.

ng'ombe	Bwana Sangai ana ng'ombe kumi na wawili.	Mr. Sangai has twelve cows.
watoto	Bwana Sangai ana watoto kumi na wawili.	Mr. Sangai has twelve children.
mikate	Bwana Sangai ana mikate kumi na miwili.	Mr. Sangai has twelve loaves.
nazi	Bwana Sangai ana nazi kumi na mbili.	Mr. Sangai has twelve coconuts.
mananasi	Bwana Sangai ana mananasi kumi na mawili.	Mr. Sangai has twelve pineapples.

B.

vikombe	Mkewe ana vikombe kumi na vinne.	His wife has fourteen cups.
sahani	Mkewe ana sahani kumi na ñne.	His wife has fourteen plates.
nguo	Mkewe ana nguo kumi na ñne.	His wife has fourteen dresses.
samaki	Mkewe ana samaki kumi na ñne. (or: ...wanne.)	His wife has fourteen fish.

sindano	Mkewe ana sindano kumi na nine.	His wife has fourteen needles.
rafiki	Mkewe ana rafiki kumi na wane.	His wife has fourteen friends.
vidonge	Mkewe ana vidonge kumi na vinne.	His wife has fourteen pills.

3. Devise short conversations giving ten different reasons why Mirambo didn't go to see Sangai on Wednesday.

Unit 59

1. Basic Dialogue. Is your wife feeling better?

Mirambo

ulipoondoka

when you left

hali (N)

condition

namna, namna (N)

kind, sort

Ulipoondoka leo, hali yake ilikuwa
namna gani?

When you left today, what was her
condition like?

Magese

-onekana

to seem, appear, become visible

Leo anaonekana hajambo kidogo.

Today she seems to be a little better.

('Today she seems she has no trouble
a little.')

Mirambo

-ambukiza

to infect

ugonjwa (U)

illness

Unadhani ameambukizwa ugonjwa
huo huko Mbeya au hapa?

Do you think that she caught the disease
there in Mbeya, or here?

Magese

mbu (N-anim.)

mosquitoes

Nadhani ni hapa, kwa sababu hakuna
mbu wengi huko Mbeya.

I think it was here, because there
aren't many mosquitoes there in
Mbeya.

NotesA. -po- as an equivalent for 'when.'

uliondoka	you left
ulipoondoka	when you left
utamwona	you will see him
utapomwona	} when you see him
utakapomwona	

The relative prefix -po- is commonly used as an equivalent for the 'when' of an English adverbial clause. It stands between the tense prefix and the object prefix. The form with -takapo- is considered more standard than the form with -tapo-, but both are widely used.

2.

A. Huko with locative.

vitunguu	Hakuna vitunguu huko sokoni.	There are no onions in the market.
maharagwe	Hakuna maharagwe huko sokoni.	There are no beans in the market.
pilipili	samaki	nazi

B. One use of namna.

ugonjwa	Hali ya ugonjwa wake ilikuwa namna gani?	What was the condition of his sickness?
homa	Hali ya homa yake ilikuwa namna gani?	What was the condition of his fever?
miguu	watoto	motokaa kazi jamaa

3.

A. Concord; -onekana.

machungwa	Hali ya machungwa haya ni namna gani?	What is the condition of these oranges?
~bichi	Yanaonekana mabichi sana.	They look very unripe.

ng'ombe	Hali ya ng'ombe hawa ni namna gani?	What is the condition of these cows?
zuri	Wanaonekana wazuri sana.	They look very good.
nguruwe	Hali ya nguruwe hawa ni namna gani?	What is the condition of these pigs?
baya	Wanaonekana wabaya sana.	They look very bad.
njugu	Hali ya njugu hizi ni namna gani?	What is the condition of these nuts?
bovu	Zinaonekana mbovu sana.	They look very spoiled.
mahindi	Hali ya mahindi haya ni namna gani?	What is the condition of this maize.
bichi	Yanaonekana mabichi sana.	It looks very unripe.
chakula	Hali ya chakula hiki ni namna gani?	What is the condition of this food?
zuri	Kinaonekana kizuri sana.	It looks very delicious.
vitunguu	Hali ya vitunguu hivi ni namna gani?	What is the condition of these onions?
baya	Vinaonekana vibaya sana.	They look very spoiled.

B. Verb forms with -po-.

kumaliza	Nilimaliza kazi. Nilipomaliza kazi, niliondoka nyumbani.	I finished working. When I finished work, I left the house.
kuona	Niliona motakaa. Nilipoona motakaa, niliondoka nyumbani.	I saw a motor car. When I saw the motor car, I left the house.
kusikia	Nilisikia gari la moshi. Niliposikia gari la moshi, niliondoka nyumbani.	I heard a train. When I heard the train, I left the house.

kupata Nilipata taa na mafuta.
Nilipopata taa na mafuta,
niliondoka nyumbani.

I got a lamp and oil.
When I got the lamp and oil,
I left the house.

Unit 60

1. Basic Dialogue. The children have coughs.

Mutisya

Watoto wako hawajambo?

Are your children all right?

Hamisi

-koha

to cough

Hawajambo, lakini wanakohoakohoa.

They're all right, but they have
light coughs.

Mutisya

Umewapeleka hospitali?

Have you taken them to the hospital?

Hamisi

-shughulika

to be busy

Bado sijawapeleka, kwa sababu
ninashughulika na ugonjwa wa
mama yao.

I haven't taken them yet because
I'm kept busy ('I'm busied') with
the illness of their mother.

Mutisya

-faa

to be suitable

Je, huoni ingefaa kuwapeleka
hospitali pamoja na mama yao?

But don't you think it would be a
good idea to take them to the
hospital along with their mother?

Hamisi

Ndiyo, nadhani nitafanya hivyo.

Yes, I think I'll do so.

Mutisya

-salimia

to convey regards to

-pa	to give
wape	give to them
~pole	kind, gentle

Usikose kufanya hayo, na unisalimie Don't (fail) to do it, and convey my
na kuwapa (or:...,uwape) pole. regards, and my condolences.

Notes

A. -faa with 'impersonal prefix.'

Itafaa kuwasaidia. } Itafaa tuwasaidie. }	It will be a good idea to help them.
Ingefaa kuwapeleka nyumbani.	It would be a good idea to take them home.

The verb -faa with subject prefix i- is followed by an infinitive, or by the subjunctive. The translation is usually 'it is/will be/would be suitable to...' or 'it is a good idea to...'. There is no noun subject 'implied' for the verbs in these sentences; the N-class prefix with -faa is said to be used 'impersonally.'

B. The phrase -pa pole.

Wape pole.	Condole with them.
Wamekuja kutupa pole.	They have come to condole with us.

2.

A. -faa plus infinitive.

kueleza	Itafaa kueleza mambo haya yote.	It will be a good thing to explain about all these affairs.
kuelewa	Itafaa kuelewa mambo haya yote.	It will be a good thing to understand all these affairs.
kula	Itafaa kula dawa hii yote.	It will be a good thing to take all this medicine.

kusafisha	Itafaa kusafisha vyombo hivi vyote.	It will be a good thing to clean all these utensils.
kuuza	Itafaa kuuza mboga hizi zote.	It will be a good thing to sell all these vegetables.

B. Pamoja na.

baba	Tulikwenda pwani pamoja na baba yetu.	We went to the beach together with our father.
ndugu	Tulikwenda pwani pamoja na ndugu yetu.	We went to the beach together with our brother.
rafiki	Tulikwenda pwani pamoja na rafiki yetu.	We went to the beach together with our friend.
mpishi	Tulikwenda pwani pamoja na mpishi wetu.	We went to the beach together with our cook.
wazazi	Tulikwenda pwani pamoja na wazazi wetu.	We went to the beach together with our parents.

C. -salimia; WA nouns vs. N-personal nouns.

wazazi	Tusalimie wazazi wako.	Give our regards to your parents.
baba	Tusalimie baba yako.	Give our regards to your father.
ndugu	Tusalimie ndugu yako.	Give our regards to your brother.
watoto	Tusalimie watoto wako.	Give our regards to your children.
rafiki	Tusalimie rafiki yako.	Give our regards to your friend.

3.

A. Me-tense: affirmative vs. negative.

kupeleka	Umewapeleka watoto hospitalini? Bado sijawapeleka.	Have you taken the children to the hospital? I haven't taken them yet.
kufuta	Umepangusa maji? (or: Umefuta maji?)	Have you wiped up the water?

Bado sijapangusa.

I haven't wiped it yet.

or: Sijafuta.

kutia Umetia mafuta katika taa?

Have you put oil in the lamp?

Bado sijayatia.

I haven't put it in yet.

kupatia Umenipatia viberiti?

Have you gotten me some matches?

Bado sijakupatia.

I haven't gotten you any yet.

B.

kusafisha Mpishi amesafisha jiko?

Has the cook cleaned the kitchen?

Bado hajasafisha.

He hasn't cleaned it yet.

kuwasha Mpishi amewasha taa?

Has the cook lit the lamp?

Bado hajawasha.

He hasn't lit it yet.

kununua Mpishi amenunua mafuta

Has the cook bought any more oil?

mengine?

Bado hajanunua.

He hasn't bought any yet.

kupa Mpishi amewapa watoto

Has the cook given the children

mkate?

some bread?

Bado hajawapa.

He hasn't given them any yet.

kutayarisha

Mpishi ametayarisha chakula

Has the cook prepared food for

cha mchana?

the day? (or: the midday meal?).

Bado hajatayarisha.

He hasn't prepared any yet.

Conversation Starters

1. A went to see C on Thursday. He tells B what C and the various members of C's household were doing when he got there.

2. A is debating whether to take his child to the hospital. He seeks advice from B.

READING SELECTION I

Dar es Salaam

Dar es Salaam ni mji mkubwa kuliko yote nchini Tanganyika, pia ni mji mkuu wa serikali. Kuna watu wa makabila mbalimbali, lakini wote husema Kiswahili. Lugha ya Kiswahili inasemwa na kila mtu hata Wazungu, Wahindi na Waarabu.

Upande wa mashariki ya Dar, kuna bahari. Bahari hii huitwa Bahari ya Hindi. Katika sehemu ya magharibi ya mji kuna majumba maarufu ya shughuli mbalimbali, kama vile, shule, boma, hospitali, na mengineyo. Bwana Gavana ni mtu mkubwa na maarufu sana mjini. Jumba lake zuri liko karibu na pwani. Pia ofisi za idara za serikali ziko karibu na pwani.

Wakati wa mchana watu huwa wengi katika hoteli. Wengine huenda kula chakula, na wengine hupenda kunywa kinywaji tu kama soda au maji ya machungwa. Katika hoteli vyakula vingi huuzwa. Katikati ya mji kuna maduka makubwa na madogo. Maduka haya yanauza vyakula, nguo, vyombo vya nyumbani, na vingine vya aina mbali mbali. Vingine vinauzwa ghali kuliko vingine, pia vingine vinauzwa rahisi.

Soko liko katikati ya mji vile vile. Huko kunapatikana samaki wa baharini, machungwa ya Utete na Morogoro, vitunguu, pilipili na muhogo wa Bagamoyo. Unajua wakulima wa Bagamoyo hupanda sana muhogo, kwa hivyo hupenda kuusa mazao yao katika soko hili maarufu.

kuliko	'than'	kama vile	'for example'
mbalimbali	'various'	gavana (N-pers.)	'governor'
kila	'each'	kama	'as'
bahari (N)	'sea, ocean'	katikati (N)	'in the midst'
hata	'even'	duka (MA)	'shop'
jumba (MA)	'building'	aina (N)	'kind'
maarufu	'famous'	ghali	'expensive'
shughuli (N)	'business'	rahisi	'cheap, easy'
		vile vile	'also'

Questions and Answers over Reading Selection

QuestionsSample Answers

- | | |
|--|---|
| 1. Dar es Salaam ni mji mkubwa? | Ndiyo, ni mkubwa kuliko miji yote nchini. |
| 2. Mji mkuu wa serikali ya Tanganyika ni mji gani? | Ni Dar es Salaam. |
| 3. Katika mji wa Dar es Salaam, kuna kabila moja tu? | Hapana, kuna makabila mengi mbalimbali. |
| 4. Watu wote wa Dar es Salaam husema lugha gani? | Husema zaidi Kiswahili. |
| 5. Kiswahili kinasemwa na watu wengi wa Dar es Salaam? | Ndiyo. Lugha hii inasemwa na kila mtu. |
| 6. Kuna nini upande wa mashariki wa Dar? | Kuna bahari. |
| 7. Bahari hii huitwaje? | Bahari hii huitwa Bahari ya Hindi. |
| 8. Kuna nini katika sehemu ya magharibi ya mji? | Kuna majumba mbalimbali. |
| 9. Jumba la Bwana Gavana liko wapi? | Liko karibu ya pwani. |
| 10. Mtu gani ni mkubwa mjini? | Bwana Gavana. |
| 11. Kuna majumba gani mengine karibu ya pwani? | Kuna ofisi za idara za serikali. |
| 12. Watu huwa wachache katika hoteli? | Hapana, huwa wengi. |
| 13. Watu wote huenda hoteli kula chakula? | Hapana, wengine huenda kunywa kinywaji tu. |
| 14. Vyakula huuzwa katika hoteli? | Ndiyo, bwana. Vyakula vingi huuzwa katika hoteli. |

15. Kuna maduka makubwa katikati
ya mji?

Ndiyo. Kuna makubwa na madogo pia.

16. Maduka haya yanauza nini?

Mengine yanauza nguo na vyombo vya
nyumbani, na mengine yanauza vyakula.

17. Vingine vinauzwa ghali?

Ndiyo, lakini pia vingine ni rahisi.

18. Soko liko karibu na pwani?

La, liko katikati ya mji.

Review Sentences, Units 1 - 60.

- | | |
|--|--|
| 1. Afadhali uondoke sasa usilikose
gari la moshi. | You'd better leave now so as not to
miss the train. |
| 2. Ijapokuwa sikuja jana nilizipata
habari. | Although I didn't come yesterday, I
got the news. |
| 3. Unataka kupumzika sasa? | Do you want to rest now? |
| 4. Una nguo za aina ngapi? | How many kinds of clothes do you have? |
| 5. Ukija leo jioni tutakwenda
kuwatazama jamaa zetu. | If you come this evening, we will go
visit our relatives. |
| 6. Unaweza kusoma na kuandika? | Can you read and write? |
| 7. Nikipata pesa za kutosha
nitamtembelea ndugu yangu. | If I get enough money, I will visit
my brother. |
| 8. Watapewa chakula na mama yao. | They will be given food by their mother. |
| 9. Usijiumize kwa kisu hicho. | Don't hurt yourself with that knife. |
| 10. Juma, iwashe taa sasa. | Juma, light the lamp now. |
| 11. Nina tamaa ya kunywa pombe
kidogo. | I feel like drinking a little beer. |
| 12. Ndugu yangu, usikate tamaa,
Mungu atakusaidia. | Don't give up, brother, God will help
you. |
| 13. Sijui kwa hakika, lakini nadhani
atakuja leo jioni. | I don't know for sure, but I think he
will come this evening. |
| 14. Wakipata nafasi, watakuja kesho? | If they get a chance, will they come
tomorrow? |
| 15. Ningefurahi sana kama ungekuja
hapa. | I would be very glad if you would come
here. |
| 16. Itafaa sana umpe pesa zake. | It would be a very good idea for you
to give him his money. |

- | | |
|--|---|
| 17. Itanilazimu kwenda Dodoma
kumwona rafiki yangu. | I will have to go to Dodoma to see
my friend. |
| 18. Mji wa Nairobi uko kati ya
Moshi na Kisumu. | The city of Nairobi is between Moshi
and Kisumu. |
| 19. Vikombe vyote vinevunjika. | All the cups are broken. |
| 20. Vinevunjwa na mtoto. | They were broken by a child. |
| 21. Ameangusha vikombe chini. | He has dropped the cups. |
| 22. Je, sahani pia zimevunjika? | Were the plates broken too? |
| 23. Nipatie vyombo vya kupakulia. | Get me the dishes. |
| 24. Mtoto hataki maziwa hata kidogo. | The child doesn't want any milk at all. |
| 25. Baada ya kufika walisoma
vitabu. | After arriving, they read some books. |
| 26. Nguo zake zilikuwa chafu sana. | His clothes were very dirty. |
| 27. Tafadhali unisalimie Hasani
ukimwona. | Please give my regards to
Hasani if you see him. |
| 28. Nasikitika kwa sababu ya hayo
yaliyotokea. | I am sorry because of what has
happened. |
| 29. Akirudisha vitabu mpe barua hii. | When he returns the books, give him
this letter. |
| 30. Nisaidie kwa baiskeli yako,
tafadhali. | Please lend me your bicycle. |
| 31. Kwa heri, nitarudi baada ya siku
chache. | Good bye, I'll be back in a few days. |
| 32. Miguu yangu yauma sana. | My feet hurt very much. |
| 33. Nitakwenda kumwona bwana daktari. | I'll go see the doctor. |
| 34. Watoto wangu wawili wanakohoakohoa. | My two children have light coughs. |
| 35. Wapishi hao walikuwa wakila nyama. | Those cooks were eating meat. |

36. Pengine zitarudishwa nyumbani
kesho. Maybe they (N plu.) will be returned
to the house tomorrow.
37. Leo asubuhi nitatengeneza
motakaa yangu. This morning I will repair my car.
38. Habari za nyumbani, wote
hawajambo? How's everything at home? Is everyone
all right?
39. Hawajambo, asante. They're fine, thank you.
40. Mume wangu ameambukizwa ugonjwa
wa malaria. My husband has contracted malaria.

Unit 61

1. Basic Dialogue. I don't feel too well.

Ahamed

mwalimu (WA)

teacher

Tafadhali, mwalimu, naumwa.
(or:..., mimi ni mgonjwa.)

Please, teacher, I'm ill.

Magese

Wewe mgonjwa? Waumwa nini?

Are you ill? What are you suffering
from?

Ahamed

shingo (MA)

neck

jino (MA: plu. meno)

tooth

Kichwa, shingo na meno.

[My] head, neck and teeth.

Magese

mafua (or: kamasi)

cold in the head

Pengine una mafua?

Maybe you have a cold?

Ahamed

pua (N)

nose

sawa

like, equal, level

Hapana, kwa sababu ninapumua sawa
sawa.

No, because I'm breathing all right.

Magese

tabibu (MA-pers)

doctor

(or: daktari, mganga)

Jitayarishe, tutakwenda kwa tabibu.

Get yourself ready; we will go to the
doctor.

2.

A. WA nouns vs. N-personal nouns.

watoto	Watoto wetu wengi waumwa meno.	Many of our children have toothaches.
walimu	Walimu wetu wengi waumwa meno.	Many of our teachers have toothaches.
ndugu	Ndugu zetu wengi waumwa meno.	Many of our brothers have toothaches.
rafiki	Rafiki zetu wengi waumwa meno.	Many of our friends have toothaches.

3.

A. -a plus infinitive; personal object prefixes.

watoto	Hakuna mtu wa kuwafunza watoto hesabu. Wafunze hesabu.	There is no one to teach the children arithmetic. Teach them arithmetic.
mtoto	Hakuna mtu wa kufunza mtoto hesabu. Mfunze hesabu.	There is no one to teach the child arithmetic. Teach him arithmetic.
mimi	Hakuna mtu wa kufunza hesabu. Nifunze hesabu.	There is no one to teach me arithmetic. Teach me arithmetic.

B. Concord: Noun in first sentence, object prefix in second; adjective vs. related causative verb.

nguo	Nguo si tayari. Nitazitayarisha.	The dresses aren't ready. I will get them ready.
mimea	Mimea si tayari. Nitaitayarisha.	The plants aren't ready. I will get them ready.
mayai	Mayai si tayari. Nitayatayarisha.	The eggs aren't ready. I will get them ready.

uji	Uji si tayari. Nitautayarisha.	The porridge isn't ready. I will get it ready.
nimi	Mimi si tayari. Nitajitayarisha.	I am not ready. I will get ready.

C. Object prefixes, including the reflexive -ji-.

watoto	Watoto ni wagonjwa. Baba hawezi kuwasaidia.	The children are sick. Father can't help them.
Hamisi	Hamisi ni mgonjwa. Baba hawezi kumsaidia.	Hamisi is sick. Father can't help him.
ng'ombe	Ng'ombe ni mgonjwa. Baba hawezi kumsaidia.	The cow is sick. Father can't help it.
baba	Baba ni mgonjwa. Hawezi kujisaidia.	Father is sick. He can't help himself.

D. Verb phrases with -wa-.

ninyi	Mlikuwa mkiumwa shingo? Hapana, hatukuwa tukiumwa shingo. Tulikuwa tukiumwa kichwa.	Did you have stiff necks? No, we didn't have stiff necks. We had headaches.
wewe	Ulikuwa ukiumwa shingo? Hapana, sikuwa nikiumwa shingo. Nilikuwa nikiumwa kichwa.	Did you have a stiff neck? No, I didn't have a stiff neck. I had a headache.

rafiki yako rafiki zako

Unit 62

1. Basic Dialogue. You've hurt your finger!

Sangai

kidole (VI)

finger

damu (N)

blood

Kidole chako chatoka damu!

There is blood coming from your
finger! ('your finger is coming-
from blood')

Je uliumia?

Are you hurt?

Mutisya

-jeruhi

to bruise, wound

mlango (MI)

door

Ndiyo, bwana, nilijeruhiwa na mlango. Yes, I was bruised by a door.

Sangai

-vimba

swell

Hata kimevimba sana.

It is even swollen quite a bit.

Mutisya

usaha (U)

pus

Ndiyo, jana kilitoka usaha kidogo. Yes, yesterday a little pus came out
[of it] ('out of it a little').

Sangai

mshipa (MI)

vein, artery (or any thin,
elongated tissue, such as a
nerve or tendon)

Natumaini mshipa salama.

I hope the blood vessels are all right.

Mutisya

-pona

to recover from illness or injury

Kitapona tu, asante.

Oh, it will get better, thanks.

NotesA. Grammatical subject vs. logical subject.

Kidole chake kilitoka damu. }

Damu ilitoka kidoleni mwake. }

Some blood came out of his finger.

These two sentences are synonymous. Note that the verb stem remains the same. The subject prefix agrees with whichever noun precedes it.

2.

A. MI-class with numbers 2 - 12.

2	Jumba hilo lina milango miwili.	That large building has two doors.				
3	Jumba hilo lina milango mitatu.	That large building has three doors.				
4	5	6	7	8	9	10
11	Jumba hilo lina milango kumi na moja.	That large building has eleven doors.				
12	Jumba hilo lina milango kumi na miwili.	That large building has twelve doors.				

B. VI-class with numbers 1 - 10.

1	Nimejeruhiwa kidole kimoja.	I am hurt on one finger.
2	Nimejeruhiwa vidole viwili.	I am hurt on two fingers.
4	Nimejeruhiwa vidole vinnie.	I am hurt on four fingers.
5	Nimejeruhiwa vidole vitano.	I am hurt on five fingers.
7	Nimejeruhiwa vidole saba.	I am hurt on seven fingers.

- 9 Nimejeruhiwa vidole tisa. I am hurt on nine fingers.
 10 Nimejeruhiwa vidole kumi. I am hurt on ten fingers.

C. Grammatical subject which is different from logical subject.

↓	Kidole chake kinatoka usaha kidogo.	His finger is discharging a little pus.
damu	Kidole chake kinatoka damu kidogo.	His finger is bleeding a little.
mishipa	Mishipa yake inatoka damu kidogo.	His blood vessels are bleeding a little.
ḡguu	ḡguu wake unatoka damu kidogo.	His foot is bleeding a little.
pua	Pua yake inatoka damu kidogo.	His nose is bleeding a little.

3.

A. Interchange of grammatical and logical subjects with -toka.

kidole	Kidole chake kilitoka damu.	His finger bled.
	Damu ilitoka kidoleni mwake.	His finger bled.
ḡguu	ḡguu wake ulitoka damu.	His foot bled.
	Damu ilitoka ḡḡnuni mwake.	His foot bled.
pua	Pua yake ilitoka damu.	His nose bled.
	Damu ilitoka puani mwake.	His nose bled.
kichwa	Kichwa chake kilitoka damu.	His head bled.
	Damu ilitoka kichwani mwake.	His head bled.
shingo	Shingo lake lilitoka damu.	His neck bled.
	Damu ilitoka shingoni mwake.	His neck bled.

4. The members of A's family have been having all kinds of misfortunes recently. He tells B about them. B inquires about details and expresses sympathy.

Unit 63

1. Basic Dialogue. Late to class.

Ahamed

-chelewa

to be late, delay, be too long

Nasikitika, nimechelewa.

I'm sorry. I'm late.

Magese

neni

word

Si neni. Tumeanza sasa hivi.

No matter. We've just now begun.

-kaa kitako

to sit down

Tafadhali nenda ukakae kitako.

Please go sit down.

ukurasa (U) (plu. in N class)

page

Tazameni ukurasa wa kumi na mbili.

Look at page 12.

----- . -----

-ongea

to converse

-fungua

to close

kitabu (VI)

book

Sasa fungeni vitabu vyenu tuongee.

Now close your books, and we will

converse.

Notes

A. Plural imperative.

Zitayarishe sasa hivi!Get them ready right now.
(said to one person)**Zitayarisheni sasa hivi!**Get them ready right now.
(said to more than one person)**Njoo nyumbani!**

Come to the house. (one person)

Njoooni nyumbani!

Come to the house. (more than one)

The plural imperative in Swahili ends with -ni. The preceding vowel is -e for those verbs whose singular imperative ends in -a.

B. 'Sitting down.'

In preparing the original edition of this course, we found that Swahili speakers who worked on or criticized the manuscript displayed an unusual lack of unanimity with regard to 'sitting down'. In that edition, we said that '-kaa kitako is commonly used in Zanzibar and Tanganyika, but kitako is regarded as redundant and somewhat vulgar on the Kenya coast.' Later critics have suggested that 'sit (on a chair)' is -kaa kiti, and that 'sit (on the ground)' is either -kaa kitako or -kaa chini.

C. Other expressions for Si neno.

In place of Si neno, one more frequently hears Si kitu (lit. 'It is nothing.') or haidhuru, from the verb -dhuru 'to cause loss or damage'.

2.

A. -chelewa plus infinitive.

darasa	Kwa nini ulichelewa kuja darasani?	Why were you late to [come] to class?
kanisa	Kwa nini ulichelewa kuja kanisani?	Why were you late to come to church?
shule	chakula	

B. Negative imperative.

kurudi	Usichelewe kurudi nyumbani!	Don't delay in returning home.
kufanya	Usichelewe kufanya kazi yako.	Don't delay in doing your work.
kutayarisha	Usichelewe kutayarisha chakula.	Don't delay in preparing food.
kuwasha	Usichelewe kuwasha taa.	Don't delay in lighting the lamp.
kuletea	Usichelewe kutuletea kahawa.	Don't delay in bringing us coffee.
kuamkia	Usichelewe kuwaamkia wazee.	Don't delay in welcoming the elders.

C. N-class with numbers.

1	Kitabu hiki kina ukurasa mmoja tu.	This book has only one page.
2	Kitabu hiki kina kurasa mbili.	This book has two pages.
3	Kitabu hiki kina kurasa tatu.	This book has three pages.
11	Kitabu hiki kina kurasa kumi na moja.	This book has eleven pages.

12	Kitabu hiki kina kurasa kumi na mbili.	This book has twelve pages.
13	Kitabu hiki kina kurasa kumi na tatu.	This book has thirteen pages.
21	Kitabu hiki kina kurasa ishirini na moja.	This book has twenty-one pages.
22	Kitabu hiki kina kurasa ishirini na mbili.	This book has twenty-two pages.
23	Kitabu hiki kina kurasa ishirini na tatu.	This book has twenty-three pages.

2.

A. Negative -ja- tense vs. plural imperative.

kutayarisha	Bado hamjawatayarisha watoto? Watayarisheni sasa hivi!	Haven't you got the children ready yet? Get them ready right now.
kumaliza	Bado hamjamaliza kufanya kazi yenu? Malizeni sasa hivi!	Haven't you finished doing your work yet? Finish it right away.
kuenda	Bado hamjaenda ryumbani? Nendeni sasa hivi!	Haven't you gone home yet? Go right away.
kuja	Bado hamjaja hapa? Njooni sasa hivi!	Haven't you come here yet? Come right away.
kupa	Bado hamjawaqa watoto vitabu? Wapeni sasa hivi!	Haven't you given the children books yet? Give [them to] them right away.
kwanza	Bado hamjaanza kujifunza? Anzeni sasa hivi!	Haven't you started learning yet? Start right away.

kujifunza	Bado hamjajifunza kusoma?	Haven't you learned how to read yet?
	Jifunzeni sasa hivi!	Learn right away.

B. Imperatives: singular vs. plural.

kupata	Pata taa.	Get the lamp. (you sing.)
	Pateni taa.	Get the lamp. (you pl.)
kuleta	Lete maji.	Bring some water.
	Leteni maji.	Bring some water.
kutengeneza	Tengeneza kahawa.	Make some coffee.
	Tengenezeni kahawa.	Make some coffee.
kula	Kula ndizi hizi.	Eat these bananas.
	Kuleni ndizi hizi.	Eat these bananas.
kuenda	Nenda shuleni.	Go to school.
	Nendeni shuleni.	Go to school.
kunywa	Kunywa chai hii.	Drink this tea.
	Kunyweni chai hii.	Drink this tea.
kuona	Ora farasi.	Look at the horse.
	Oneni farasi.	Look at the horse.

C. Imperatives: affirmative vs. negative.

kuleta	Lete vitabu vingine; usivilete vyote.	Bring some of the books. Don't bring them all.
kuzuza	Uza vitabu vingine; usiviuze vyote.	Sell some books. Don't sell them all.
kununua	Nunua vitabu vingine; usivinunue vyote.	Buy some books. Don't buy them all.
kusafisha	Safisha vitabu vingine; usivisafishe vyote.	Clean some of the books. Don't clean them all.
kusoma	Soma vitabu vingine; usivisome vyote.	Read some of the books. Don't read them all.

Unit 64

1. Basic Dialogue. Classroom Routine.

Magese

ubao (U)	blackboard
Tafadhali, Bwana Aramian, nenda	Mr. Aramian, please go to the black-
ubaoni ukaandike maneno haya.	board and write these words.

Magese

Bwana Butler, tafadhali anza	Mr. Butler, please begin to read.
kusoma.	

Basil	That's enough.
-------	----------------

maana (MA)	meaning
Unajua maana ya neno 'alasiri'?	Do you know the meaning of the word
	'alasiri'?

Magese

-funua	to open
Sasa tufunue vitabu tusome Somo la	Now let's open [our] books and read
Tisa.	Lesson Nine.
kosa (MA)	a mistake
Msifanye makosa mkisoma.	Don't make mistakes as you read!
	('don't make mistakes you-reading')

Notes

A. The prefix -ka- with subjunctives.

Funua kitabu usome Somo la Nane. Open [your] book and read Lesson Eight.

Nenda ubaoni ukaandike maneno haya. Go to the board and write these words.

In a command or request involving two verbs, the second is in the subjunctive. If the first verb involves going somewhere, the prefix -ka- is used after the subject prefix of the second verb.

2.

A. Word order with lini; -anza plus infinitive.

kusoma	Juma alianza lini kusoma?	When did Juma begin reading?
kusema	Juma alianza lini kusema?	When did Juma begin speaking?
kula	Juma alianza lini kula?	When did Juma begin eating?
kufanya	Juma alianza lini kufanya kazi?	When did Juma begin working?
kupanda	Juma alianza lini kupanda mahindi?	When did Juma begin raising corn?

B. Ka-tense with the second of two verbs.

kuandika	Nenda ubaoni ukaandike maneno haya.	Go to the board and write these words.
kusoma	Nenda ubaoni ukasome maneno haya.	Go to the board and read these words.
kueleza	Nenda ubaoni ukaeleze maana ya maneno haya.	Go to the board and explain the meaning of these words.
kusema	Nenda ubaoni ukaseme maneno haya.	Go to the board and speak ('pronounce') these words.

C.

vitabu	Nenda nyumbani ukalete vitabu vyako vyote.	Go home and bring all your books.
vitu	Nenda nyumbani ukalete vitu vyako vyote.	Go home and bring all your things.

nguo	Nenda nyumbani ukalete nguo zako zote.	Go home and bring all your clothes.
senti	Nenda nyumbani ukalete senti zako zote.	Go home and bring all your small change.
machungwa	Nenda nyumbani ukalete machungwa yako yote.	Go home and bring all your oranges.
masomo	Nenda nyumbani ukalete masomo yako yote.	Go home and bring all your lessons.
watoto	Nenda nyumbani ukawaleta watoto wako wote.	Go home and bring all your children.
wagonjwa	Nenda nyumbani ukawaleta wagonjwa wako wote.	Go home and bring all your sick persons.

D.

kutazama	Nendeni sokoni <u>n</u> katazame nazi.	Go to the market and have a look at the coconuts.
kununua	Nendeni sokoni <u>n</u> kanunue nazi.	Go to the market and buy coconuts.
kuleta	Nendeni sokoni <u>n</u> kaleta nazi.	Go to the market and bring coconuts.
kutafuta	Nendeni sokoni <u>n</u> katafute nazi.	Go to the market and look for coconuts.

3.

A. Subjunctive without -ka- vs. subjunctive with -ka- after -enda.

kusaidia	Njoo <u>u</u> msaidie mwalimu. Nenda uk <u>a</u> msaidie mwalimu.	Come and help the teacher. Go and help the teacher.
kuandika	Njoo ubaoni uandike maneno haya. Nenda ubaoni ukaandike maneno haya.	Come to the board and write these words. Go to the board and write these words.

kahawa	Njoo jikoni utengeze kahawa.	Come into the kitchen and make coffee.
	Nenda jikoni ukatergeneze kahawa.	Go into the kitchen and make coffee.
kuogelea	Njoo pwani uogelea.	Come to the beach and swim.
	Nenda pwani ukaogelea.	Go to the beach and swim.

B. Negative ja-tense vs. subjunctive.

kuondoka	Hawajaondoka shuleni. Sasa wafunge vitabu, waondoke shuleni.	They haven't yet left the school. Now let them close the books, and leave the school.
kusaidia	Hawajatusaidia. Sasa wafunge vitabu, watusaidie.	They haven't yet helped us. Now let them close the books, and help us.
kula	Hawajala chakula. Sasa wafunge vitabu, wale.	They haven't eaten food yet. Now let them close the books, and eat.
kuenda	Hawajaenda nyumbani. Sasa wafunge vitabu, waende.	They haven't gone home yet. Now let them close the books, and go.

Conversation Starters

1. Describe a typical class hour.
2. From this point on, all class sessions should be conducted entirely in Swahili. Add to the content of Units 1 - 64 whatever words and phrases are necessary to make this possible.

Unit 65

1. Basic Dialogue. A letter from a student abroad.

Asha

dada (N-pers)

sister

Dada yako anafanya kazi gani?

What work is your sister doing?

Maina

-shinda

to be first, win

mtihani (MI)

a school examination

Ulaya

Europe

Mwaka jana alishinda mtihani wa

Last year she passed the Higher

juu akaenda Ulaya kusoma.

Examination and went to Europe to
study.Asha

-safiri

to travel

Alisafiriye?

How did she travel?

Maina

-ruka

to fly

ndege (N), ndege Ulaya

bird, airplane ('European bird')

Aliruka kwa ndege Ulaya.

She flew by plane.

juzi

day before yesterday

peleka

to send

ya kwamba

that ...

chuo (VI)

school

B. Indirect statements.

kuwa na Alituletea barua akasema
ya kwamba ana vitabu
vingi.

She sent us a letter saying that she
has many books.

kuhitaji Alituletea barua akasema
ya kwamba anakitaji
vitabu vingi.

She sent us a letter saying that she
needs many books.

kusoma kununua kupoteza

C. A-tense; -tumaini plus infinitive.

mimi Natumaini kushinda mtihani
wa juu na kwenda Ulaya.

I hope to pass the Higher Examination,
and go to Europe.

sisi Twatumaini kushinda
mtihani wa juu na kwenda
Ulaya.

We hope to pass the Higher Examination,
and go to Europe.

Mariamamu ndugu yangu ndugu zangu

D. halafu plus ka-tense.

kwenda Mwaka jana nilishinda
mtihani wa juu, halafu
nikaenda Ulaya.

Last year I passed the Higher
Examination, then I went to Europe.

kupata Mwaka jana nilishinda
mtihani wa juu, halafu
nikapata kazi.

Last year I passed the Higher
Examination, then I got a job.

kurudi Mwaka jana nilishinda
mtihani wa juu, halafu
nikerudi nyumbani.

Last year I passed the Higher
Examination, then I returned home.

kuendelea Mwaka jana nilishinda
mtihani wa juu, halafu
nikaendelea kusoma.

Last year I passed the Higher
Examination, then I continued
studying.

3.

A. Kuliko

ndege	Unapenda kusafiri kwa ndege au kwa gari la moshi? Ninapenda kusafiri kwa ndege kuliko kwa gari la moshi.	Do you like to travel by plane, or by train? I prefer traveling by plane to traveling by train.
michezo	Unapenda michezo au masomo? Ninapenda masomo kuliko michezo.	Do you like playing, or studying? I prefer studying to playing.
ndizi	Unapenda ndizi mbichi au mbivu? Ninapenda mbivu kuliko mbichi.	Do you like green bananas, or ripe ones? I prefer ripe to green ones.
nazi	Unapenda nazi, au mananasi? Ninapenda nazi kuliko mananasi.	Do you like coconuts, or pineapples? I prefer coconuts to pineapples.

B. A-tense: affirmative vs. negative.

kusafiri	Wasafiri mara nyingi? Hapana, sisafiri mara nyingi, nasafiri mara chache tu.	Do you travel often? No, I do not travel often, I travel only a little.
kuruka kwa ndege	Waruka kwa ndege mara nyingi? Hapana, siruki kwa ndege mara nyingi, naruka mara chache tu.	Do you fly often? No, I do not fly often, I fly only a little.

kusoma Wasoma mara nyingi?

Hapana, sisomi mara
nyingi, nasoma mara
chache tu.

Do you read often?

No, I do not read often, I read
only a little.

kunu- Wamung'unika mara nyingi?
ng'unika

Hapana, sinung'uniki
mara nyingi, nanung'unika
mara chache tu.

Do you grumble often?

No, I do not grumble often, I
grumble only a little.

Unit 66

1. Basic Dialogue. My parents are going to night school.

Maina

Wazazi wako wanajua kusoma na
kuandika?

Do your parents know how to read and
write?

Juma

Ndiyo, wanajua kusoma kidogo tu.

Yes, they know how to read just a
little.

Maina

Na kuandika je?

And what about writing?

Juma

-hudhuria

to attend

Wameanza kuhudhuria masomo ya jioni.

They've begun to attend night school.

Maina

Wanafunzwa masomo gani?

What subjects are they being taught?

Juma

-ambia

to tell

Waliniambia wanajifunza hesabu, na
kuandika Kiswahili na Kiingereza.

They told me they are learning
arithmetic, and to write Swahili
and English.

Maina

aina

kind, sort

Hesabu za aina gani?

What kind of arithmetic?

Juma

-jumlisha

to add

-toa

to take away

Za kujumlisha na kutoa.

Addition and subtraction.

2.

A. Aina.matunda Mmeleta matunda ya aina
gani?

What sort of fruit have you brought?

vitabu Mmeleta vitabu vya aina
gani?

What sort of books have you brought?

vyakula nguo nyama

B. -hudhuria.masomo Twapenda kuhudhuria masomo
ya jioni.We like to attend the evening
classes.

shule Twapenda kuhudhuria shuleni.

We like to attend the school.

kanisa Twapenda kuhudhuria kanisani.

We like to attend the church.

michezo Twapenda kuhudhuria mashindano
ya farasi.

We like to attend the horse races.

3.

A. -ambia plus indirect statement.kuanza Bwana Sangai alianza lini
masomo ya jioni?When did Mr. Sangai start the evening
classes?Aliniambia ya kwamba
alianza juzi.

He told me that he began recently.

kuhitimu Bwana Sangai alihitimu lini
masomo ya jioni?When did Mr. Sangai complete the
evening classes?Aliniambia ya kwamba
alihitimu juzi.He told me that he completed them
recently.

<p>kuchelewa Bwana Sangai alichelewa lini masomo ya jioni? Aliniambia ya kwamba alichelewa juzi.</p>	<p>When did Mr. Sangai come late for the evening classes? He told me that he came late recently.</p>
<p>4. Extra vocabulary.</p>	
<p>matunda Sokoni kuna matunda mbalimbali, kama vile machungwa, maembe, na kadhalika.</p>	<p>At the market there are various fruits such as oranges, mangoes and so forth.</p>
<p>nguo Madukani kuna nguo mbalimbali, kama vile mashati, kanzu, suruali, na kadhalika.</p>	<p>At the shops there are various kinds of clothing such as shirts, kanzus, trousers and so forth.</p>
<p>vinywaji Hotelini kunauzwa vinywaji mbalimbali, kama vile chai, kahawa, pombe, na kadhalika.</p>	<p>At the hotel there are sold various beverages such as tea, coffee, beer and so forth.</p>
<p>makabila Nchini Tanganyika kuna watu wa makabila mbalimbali, kama vile Wanyamwezi, Wabondei, Wazaramo, na kadhalika.</p>	<p>In Tanganyika there are people of different tribes such as the Nyamwezi, Bondei, Zaramo and so forth.</p>
<p>mboga Sokoni kuna mboga mbalimbali, kama vile mchicha, kábeji, na kadhalika.</p>	<p>At the market there are various vegetables such as mchicha, cabbages and so forth.</p>

Conversation Starters

1. Describe your own high school or college. Where was it located? How did you get to it? What did you study? Use the dictionary to add specialized vocabulary for the names of the various academic disciplines.

2. Tell about a letter which you have sent or received recently.

Unit 67

1. Basic Dialogue. What is it like at night school?

Maina

-endesha

to run, cause to go, drive [a car]

Nani anayeendesha shule hizi za
jioni?

Who [is it] that is running these
night schools?

Juma

msaada (MI)

assistance

-tolewa

to be put forward, be produced,
be taken away

Nafikiri sehemu ya msaada hutolewa
na Serikali.

I think a part of the support is
supplied by the government.

Maina

-kubali

to accept

Ni watu wa umri gani wanaokubaliwa?

What age people are accepted? ('It
is people of what age who are
accepted?')

Juma

hoja (N)

necessity; what is urgent

Sidhani umri ni hoja.

I don't think the age is important.

Maina

-julisha

to make known, inform, cause
to know

Basi, nitawajulisha wengi.

O.K., I'm going to tell a lot of
people.

('I'm going to cause many people to know.')

Juma

Hata ada yenyewe ni ndogo sana.

And besides, the fees themselves are very low.

Maina

Kweli? Asante! Kwa heri!

Really? Thanks! Good-bye!

Notes

A. Relative counterparts of the na- and li-tenses.

Anaendesha shule.

He runs the school.

...anayeendesha shule...

...who runs the school...

he who runs the school...

Wanakubaliwa.

They are accepted.

...wanaokubaliwa...

...who are accepted...

The verbs in the two complete sentences above are 'indicative' forms. An 'indicative' form is one that can serve as the only verb in a complete statement.

The verbs in the second and fourth examples are 'relative' counterparts of the indicative forms. In general, there is a relative counterpart for any indicative verb form in Swahili. These are generally translated into English by relative clauses beginning with who or which.

For the na and li tenses, the relative forms are like the indicative forms except for the presence of a relative affix, which occupies a slot between the tense prefix and the object prefix.

The relative affixes are identical in form with the set of suffixes found in Unit 18, Note C.

2.

A. Relatives, li-tense.

kukubaliwa	Mtu aliyekubaliwa jana ataanza kesho.	The person who was accepted yesterday will begin tomorrow.
kuja	Mtu aliyekuja jana ataanza kesho.	The person who came yesterday will begin tomorrow.
kulipa	Mtu aliyelipa ada jana ataanza kesho.	The person who paid fees yesterday will begin tomorrow.
kutumwa	Mtu aliyetumwa jana ataanza kesho.	The person who was sent yesterday will begin tomorrow.

B. Relatives, li-tense, monosyllabic stem.

kuja	Wapagazi waliokuja asubuhi wamekwenda nyumbani.	The porters who came in the morning have gone home.
kuanza	Wapagazi walioanza asubuhi wamekwenda nyumbani.	The porters who began in the morning have gone home.
kukubaliwa	Wapagazi waliokubaliwa asubuhi wamekwenda nyumbani.	The porters who were accepted in the morning have gone home.
kutumwa	Wapagazi waliotumwa asubuhi wamekwenda nyumbani.	The porters who were sent in the morning have gone home.

C. Relatives, li-tense, stative verb stem.

vikombe	Vikombe vilivyovunjika viko mezani.	The broken cups are on the table.
kikombe	Kikombe kilichovunjika kiko mezani.	The broken cup is on the table.

visahani	Visahani vilivyovunjika viko mezani.	The broken saucers are on the table.
kisahani	Kisahani kilichovunjika kiko mezani.	The broken saucer is on the table.
visu	Visu vilivyovunjika viko mezani.	The broken knives are on the table.
kisu	Kisu kilichovunjika kiko mezani.	The broken knife is on the table.
sahani (sg.)	Sahani iliyovunjika iko mezani.	The broken plate is on the table.
sahani zote	Sahani zote zilizovunjika ziko mezani.	All the broken plates are on the table.
kalamu (sg.)	Kalamu iliyovunjika iko mezani.	The broken pen is on the table.
kalamu zote	Kalamu zote zilizovunjika ziko mezani.	All the broken pens are on the table.

D. Relatives, na-tense.

upishi	Watu wanaofanya kazi ya upishi waitwa wapishi.	People who do cooking are called cooks.
ukulima	Watu wanaofanya kazi ya ukulima waitwa wakulima.	People who do farming are called farmers.
ukarani	Watu wanaofanya kazi ya ukarani waitwa makarani.	People who do clerical work are called clerks.
kufunza	Watu wanaofanya kazi ya kufunza waitwa waalimu.	People who do teaching are called teachers.

3.

A. Li-tense: indicative vs. relative.

vikombe	Vikombe vipi vilivunjika? Vilivyovunjika viko jikoni.	Which cups got broken? The broken ones are in the kitchen.
---------	--	---

kikombe	Kikombe kipi kilivunjika? Kilichovunjika kiko jikoni.	Which cup got broken? The broken one is in the kitchen.
visu	Visu vipi vilivunjika? Vilivyovunjika viko jikoni.	Which knives got broken? The broken ones are in the kitchen.
kisu	Kisu kipi kilivunjika? Kilichovunjika kiko jikoni.	Which knife got broken? The broken one is in the kitchen.
sahani (sg.)	Sahani ipi ilivunjika? Iliyovunjika iko jikoni.	Which plate got broken? The broken one is in the kitchen.
sahani (pl.)	Sahani zipi zilivunjika? Zilizovunjika ziko jikoni.	Which plates got broken? The broken ones are in the kitchen.

B. Relative, na-tense, in question and answer.

kuendesha	Nani anayeendesha shule hii? Mtu anayeendesha shule hii anaitwa Bw. Hasani.	Who runs this school? The person who runs this school is Mr. Hasani.
kufunza	Nani anayefunza hesabu shuleni humu? Mwalimu anayefunza hesabu shuleni humu anaitwa Bw. Abdallah.	Who teaches arithmetic in this school? The teacher who teaches arithmetic in this school is called Mr. Abdallah.
kutenge- neza	Nani anayeweza kutengeneza kalamu yangu? Fundu anayeweza kutengeneza kalamu yako anaitwa Bw. Juma.	Who can repair my pen? The repairman who can repair your pen is called Mr. Juma.

Unit 68

1. Basic Dialogue. What about the fees?

Maina

mwezi (MI)

month

Je, ni kiasi gani kwa mwezi?

How much is it a month, by the way?

Juma

shilingi (N)

shilling

Ni kama shilingi tano tu.

It's only about 5 shillings.

Maina

haki (N)

justice

Haki? (or: Kweli?)

Is that right?

Juma

Ndiyoi!

Yes!

Maina

Wanahitaji vitabu vipi?

Which books do they need?

Juma

bure

for nothing

Ukiisha lipa ada, vitabu utavipata
bure.

Once you have paid the fee, you get
the books free.

Maina

namu (N)

desire, longing

Jamaa. Walio na hamu ya elimu,
sasa wanayo nafasi.

Brother! Those who have a desire for
education, now [they] have the
opportunity.

Juma

Tena!

Right. ('[you can say that] again!')

NotesA. Relative counterparts of forms with the stem -na.

Wana vitabu.	They have books.
...walio na vitabu...	{ ...who have books...
	{ they who have books...
...aliye na njaa...	{ ...who is hungry...
	{ he who is hungry...

The present relative affirmative forms corresponding to past aliyekuwa, waliokuwa are formed on a special stem -li-, to which we may assign the English translation 'be'. The relative affix is placed after this stem, not before it. Note that this stem is identical in sound with the prefix for the li-tense, but for practical purposes the two elements should be regarded as distinct.

2.

A. Relative counterparts of forms with the stem -na.

vitabu	Watoto walio na vitabu waende nyumbani.	The children who have books should go home.
kalamu	Watoto walio na kalamu waende nyumbani.	The children who have pens should go home.
chakula	Watoto walio na chakula waende nyumbani.	The children who have food should go home.
njaa	Watoto walio na njaa waende nyumbani.	The children who are hungry should go home.

B. Relative counterparts of indicatives in -wa na -, (past tense).

vitabu	Watoto waliokuwa na vitabu walikwenda nyumbani.	The children who had books went home.
--------	--	---------------------------------------

kalamu	Watoto waliokuwa na kalamu walikwenda nyumbani.	The children who had pens went home.
chakula	Watoto waliokuwa na chakula walikwenda nyumbani.	The children who had food went home.
njaa	Watoto waliokuwa na njaa walikwenda nyumbani.	The children who were hungry went home.

C.

dawa	Mgonjwa aliye na dawa akae hospitali.	Have the patient who has medicine stay in the hospital.
homa	Mgonjwa aliye na homa akae hospitali.	Have the patient who has a fever stay in the hospital.
mafua	Mgonjwa aliye na mafua akae hospitali.	Have the patient who has a chest complaint stay in the hospital.
malaria	Mgonjwa aliye na malaria akae hospitali.	Have the patient who has malaria stay in the hospital.

D.

dawa	Mgonjwa aliyekuwa na dawa alikaa hospitali.	The patient who had medicine stayed in the hospital.
homa	Mgonjwa aliyekuwa na homa alikaa hospitali.	The patient who had a fever stayed in the hospital.
mafua	Mgonjwa aliyekuwa na mafua alikaa hospitali.	The patient who had a chest complaint stayed in the hospital.
malaria	Mgonjwa aliyekuwa na malaria alikaa hospitali.	The patient who had malaria stayed in the hospital.

3.

A. Na-tense, indicative vs. relative.

kichwa	Wagonjwa wengine wanaumwa kichwa.	Some patients have headaches.
	Wanaumwa kichwa waje humu.	Have those who have headaches come in.

Unit 69

1. Basic Dialogue. A shortage of professional people.

Magese

haba

few

Nchi yetu ina walimu haba sana.

Our country has very few teachers.

Hata matabibu wachache pia.

('Even doctors [are] few like-wise.')

tangu

since

-zidi

to increase

mwanafunzi (WA)

student

Lakini tangu juzi juzi

But (since) recently students have

wanafunzi wamezidi.

increased [in number].

Butler

mia

hundred

[Haikuwa] Si mwaka jana mia tatu
walipokwenda Amerika?Wasn't it last year that 300 went to
America?Sangai

zaidi (N)

more, excess

Natumaini mwaka ujao wataruka
zaidi ya hao.I hope next year ['the year which
comes'] more will fly than that.Sangai

~gumu

hard, difficult

gharama (N)

expense, outlay

Kumbuka ni vigumu sana kupata pesa
za kulipa gharama.Remember it is very hard to get the
money to pay the expenses.

NotesA. Relative counterparts of the a-tense.

mwaka ujao	the year which comes
miezi ijayo	months which come
mtu aliye na njaa	a person who is hungry

These relative forms (cf. Unit 68) are all formed with subject prefix, plus stem (-ja or -li), plus relative affix. The first two examples illustrate relative counterparts of the a-tense.

2.

A. Multiples of ten.

10	Wanafunzi kumi walikwenda Ulaya mwaka jana.	Ten students went to Europe last year.					
20	Wanafunzi ishirini walikwenda Ulaya mwaka jana.	Twenty students went to Europe last year.					
30	40	50	60	70	80	90	100

B.

19. Kitabu ndicho ninachotaka.
A book is what I want.
20. Mwambie kwamba matata
yamekwisha.
Tell him that the trouble is over.
21. Harusi yake itakuwa siku ya
Jumamosi.
His wedding will be on Saturday.
22. Nikipata pesa nitanunua
motakaa.
If I get the money, I'll buy a car.
23. Huo ulikuwa mwisho wa dansi.
That was the end of the dance.
24. Walimu walifika shuleni kitambo.
The teachers got to school early.
25. Usichanganye unga na maji.
Don't mix the meal with water.
26. Nataka msaada wa pesa.
I want financial assistance.
27. Watu wanaofanya kazi ya upishi
wanaitwa wapishi.
People who do culinary work are
called cooks.
28. Ye yote atakayeniuliza mwambie
aningoje.
Whoever asks for me, tell him to
wait for me.

29. Alikaa hapa kwa muda wa saa moja hivi. He stayed here for about an hour.
30. Kama akija, atatupigia simu. If he comes, he will call us up.
31. Kumbuka kumsalimia Bwana Hasani. Remember to say hello to Hasani.
32. Watakapofika tutasafiri mpaka Mbeya. When they get here, we will make a trip to Mbeya.
33. Pole, utapata nafuu. Take it easy, you'll get better.
34. Walimshangilia mkubwa wao alipofika. They greeted their leader noisily when he arrived.
35. Baba yake amepona, sasa hajambo. His father recovered; he's all right now.
36. Mtoto anapolia anataka kunyonya. When a child cries, it wants to nurse.
37. Ana wasiwasi juu ya mguu wake uliovimba. He's worried about his swollen foot.
38. Yafaa kuzuia magonjwa kwa kutumia dawa. It's a good idea to prevent diseases through the use of medicine.
39. Wapatieni vitu wanavyotaka ili waondoke. Get them the things they want, so that they may go.
40. Kile ndicho kitabu ninachokisoma. That one there is the book I am reading.

Unit 8:

1. Basic Dialogue. Getting into town from the airport.

Abasi

m̄zigo (MI)

load

Mizigo yangu iko tayari sasa.

My luggage ('loads') is ready now.

kwenye

which has/where there is

Tafadhali, ichukue mpaka kwenye
teksi.

Please take it to the taxi stand.

piga

to strike, hit

simu

telephone, telegraph

Kwanza, nataka kupiga simu.

First, I want to make a phone call
(or: to send a telegram)

Hamisi

Bwana, unataka teksi?

Do you want a taxi, sir?

Abasi

Ndiyo. Bei gani kutoka hapa mpaka
m̄jini?

Yes. How much from here to downtown?

Hamisi

Itaonyeshwa na mita. Una mizigo
mingapi?

It is shown by the meter. How many
bags have you?

Abasi

~eusi

black

~ekundu

red

Nina miwili mikubwa nyeusi, na mmoja mwekundu. ~zito	I have two big black ones, and one red one. heavy
Mwekundu ni mdogo, lakini ni mzito sana.	The red one is small, but it is very heavy.

NotesA. The stem ~enye.

mahali penye teksi	a place where there are taxis
kahawa yenye sukari	coffee with sugar in it
kijana mwenye mchumba	a young fellow who has a fiancée

The stem ~enye is used as in these examples. With the ku concord it is frequently used without an antecedent, as in the basic dialogue for this unit.

2.

A. ~enye; concords with ~wili 'two'.

nyumba	Tulifika kwenye nyumba mbili.	We arrived where there were two houses.
mti	Tulifika kwenye miti miwili.	We arrived where there were two trees.
shule	Tulifika kwenye shule mbili.	We arrived where there were two schools.

jumba shamba hoteli

B. Concords with ~ingine and ~eusi.

vitabu	Vitabu vingine ni vyeusi.	Some books are black.
kitu	Kitu kingine ni cheusi.	Some thing is black. (or: the other thing...)
meza	Meza nyingine ni nyeusi.	Some tables are black.
baiskeli	Baiskeli nyingine ni nyeusi.	Some bicycles are black.
nguo	Nguo nyingine ni nyeusi.	Some clothes are black.

wino Wino mwingine ni mweusi. Some ink is black.

C. Concorde with ingine and ekundu.

kitabu Vitabu vingine ni vyekundu. The other books are red.

tunda Tunda jingine ni jekundu. The other piece of fruit is red.

baiskeli nguo wino

D. Concorde with ingine and zito.

mzigo Mizigo mingine ni mizito. Some luggage is heavy.

barua Barua nyingine ni nzito. Some letters are heavy.

jembe Majembe mengine ni mazito. Some hoes are heavy.

meza jiko kiti kitabu

3.

A. -po- as an equivalent for 'when.'

kusema Alikuwa akisema. He was speaking.
 Nilifika alipokuwa I arrived while he was speaking.
 akisema.

kusoma Alikuwa akisoma. He was reading.
 Nilifika alipokuwa I arrived when he was reading.
 akisoma.

kufanya Alikuwa akifanya kazi. He was working.
 Nilifika alipokuwa I arrived when he was working.
 akifanya kazi.

kula Alikuwa akila. He was eating.
 Nilifika alipokuwa akila. I arrived when he was eating.

B.

kurudi Bado hajarudi. He hasn't returned yet.
 Atakaporudi, When he returns I'll go with him.
 nitakwenda naye.

kumaliza	Bado hajamaliza kazi yake. Atakapomaliza kazi yake nitakwenda naye.	He hasn't finished his work yet. When he finishes his work I'll go with him.
kuingia	Bado hajaingia nyumbani. Atakapoingia nyumbani nitakwenda naye.	He hasn't entered the house yet. When he enters the house, I'll go with him.
kuondoka	Bado hajaondoka. Atakapoondoka, nitakwenda naye.	He hasn't left yet. When he leaves I'll go with him.
giza	Giza halijaingia. Giza litakapoingia, tutawasha taa.	It is not dark yet. When it gets dark, we will light the lamps.
teksi	Teksi haijafika. Teksi itakapofika, tutakwenda.	The taxi hasn't arrived. When the taxi arrives, we will go.
mvua	Mvua haijanyesha. Mvua itakaponyesha tutapanda mbegu.	It hasn't rained yet. When the rain falls, we will plant seeds.

Unit 82

1. Basic Dialogue. A trip to Tanga.

Sangai

Ninakusudia kusafiri Tanga kesho. I'm planning to make a trip to Tanga tomorrow.

Magese

nauli (N) fare

kiasi (KI sg. only) amount

Nauli ya kutoka hapa mpaka Tanga How much is the fare from here to ni kiasi gani? Tanga?

Sangai

Ni shilingi thelathini na mbili. It's 32 shillings.

Magese

Utakapofika Korogwe utashuka? Are you going to get off (to disembark) when you get to Korogwe?

Sangai

La. Nitakwenda moja kwa moja. No, I'm going to go straight on.

abiria (N-an.) passenger

~refu long, tall

mwendo (MI) journey

Kwa gari ni mwendo wa siku moja tu. By bus it is a trip of only one day.

Si mrefu. It's not long.

Magese

Vema. Ujaliwapo kufika nisalimie Good! If you are helped (i.e. by jamaa. God) to arrive, give my regards

to (your) family.

- - - - -

2.

A. Some sentences containing nijaliwapo.

kufika	Nijaliwapo kufika Tanga nitakuwa na furaha.	If I am helped to arrive at Tanga, I will be happy.
kuhitimu	Nijaliwapo kuhitimu masomo nitakuwa na furaha.	If I am helped to finish my education, I will be happy.
kupata	Nijaliwapo kupata mavuno mazuri nitakuwa na furaha.	If I am helped to get a good harvest, I will be happy.

B. -shuka katika-.

gari	Shukeni katika gari!	Get off the train!
motakaa	Shukeni katika motakaa!	Get out of the car!
baiskeli	Shukeni katika baiskeli!	Get off the bicycle!
mti	Shukeni katika mti!	Get down from the tree!

C. Things that can be refu.

mwendo	Mwendo ule ni mrefu.	That is a long journey.
mkate	Mkate ule ni mrefu.	That loaf of bread is long.
mtoto	Mtoto yule ni mrefu.	That child is tall.
mwanamke	Mwanamke yule ni mrefu.	That lady is tall.
jembe	Jembe lile ni refu.	That hoe is long.
gari la moshi	Gari la moshi lile ni refu.	That train is long.
ndizi	Ndizi zile ni ndefu.	Those bananas are long.

D. Sentences containing another form of -jalia.

kufika	Ujaliwe kufika Tanga.	May you be helped to reach Tanga.
kupata	Ujaliwe kupata mimea mizuri.	May you be helped to get good crops.
kuhitimu	Ujaliwe kuhitimu mtihani wako.	May you be helped to pass your examination.
kupona	Ujaliwe kupona homa yako.	May you be helped to recover from your fever.

3. A and B discuss a trip that one of them has taken recently, to see a friend of his get married.

Unit 83

1. Basic Dialogue. How much is the basket?

Hadija

kikapu (VI)

basket

Kikapu hiki kidogo ni bei gani?

How much is this little basket?

Mr. Patel

Shilingi mbili na senti hamsini.

Two shillings and fifty cents.

Hadija

-punguza

to make less

Nakitaka, lakini nipunguzie kidogo.

I want it, but reduce it a little
for me.

Mr. Patel

Ah! Hiyo ndiyo bei yake.

Ah! That is its price.

Hadija

Ndiyo, lakini nitakupa shilingi
moja tu.

Yes, but I'll give you just one
shilling.

Mr. Patel

Shilingi moja ni kidogo sana!

One shilling is very low.

Hadija

-dhuru

to harm

Haidhuru. Nitakupa shilingi
moja na senti kumi.

No matter. I'll give you 1.10.

(to be continued)

2. This entire series of exercises, involving the comparison of numbers, should be done orally with books closed. The exercises are printed chiefly as a guide to the tutor.

A. Which of the prices is greater - the first or the second?

a.	1s - 3s	shilingi moja	-	shilingi tatu	tatu
	2s - 3s	shilingi mbili	-	shilingi tatu	tatu
	3s - 6s	shilingi tatu	-	shilingi sita	sita
	6s - 3s	shilingi sita	-	shilingi tatu	sita
	4s - 6s	shilingi nne	-	shilingi sita	sita

f.	4s - 5s	k.	8s - 10s	p.	8s - 7s
	7s - 4s		7s - 5s		7s - 9s
	7s - 6s		6s - 4s		3s - 5s
	8s - 9s		9s - 10s		5s - 9s
	9s - 6s		10s - 11s		8s - 4s

3.

A. Of each set of three numbers, which is greatest?

a.	3-5-7	tatu - tano - saba	saba
	4-2-3	nne - mbili - tatu	nne
	6-7-5	sita - saba - tano	saba
	1-3-2	moja - tatu - mbili	tatu
	8-4-5	nane - nne - tano	nane

f. 3-6-5

9-8-7

4-8-3

2-4-6

7-6-5

k. 9-10-11

7-6-8

5-3-4

2-6-9

6-4-7

p. 4-3-5

8-9-7

6-9-7

8-4-6

3-5-1

Unit 84

1. Basic Dialogue. Settling on a price. (continued)

Patel

Ah! Siuzi. Ukitaka toa shilingi moja na senti ishirini na tano... Ah, I won't sell, but if you want to pay 1.25...

Hadija

ghali expensive
Ndiyo lakini naona ni ghali, bado. Yes, but it seems to me it is still high.

Patel

mwisho (MI) end
Utatoa kiasi gani, mwisho wako? What amount will you give, your last price?

Hadija

Nitakupa shilingi moja na senti I'll give you \$1.15.
kumi na tano.

Patel

rahisi cheap
Vema. Kwako tu. Lakini ni rahisi All right. Only for you. But it's very cheap.
sana.

Hadija

-shika to grasp, hold fast
Vema. Shika shilingi mbili na Fine. Take these two shillings and
nirudishie =/85 cts. give me back 85 cts.

2.

A. Practice in imitation, reading, and dictation.

5 cts.	45 cts.	85 cts.
10 cts.	50 cts.	90 cts.
15 cts.	55 cts.	95 cts.
20 cts.	60 cts.	18
25 cts.	65 cts.	1.10
30 cts.	70 cts.	1.25
35 cts.	75 cts.	1.30
40 cts.	80 cts.	1.50

B.

shs. 1.25	shs. 2.80	shs. 4.00
shs. 1.50	shs. 3.00	shs. 4.20
shs. 1.75	shs. 3.15	shs. 5.40
shs. 2.00	shs. 3.35	shs. 6.60
shs. 2.20	shs. 3.55	shs. 7.80
shs. 2.40	shs. 3.75	shs. 8.25
shs. 2.60	shs. 3.95	shs. 9.50

3.

In each part of these exercises, two prices are given, followed by a third. In most instances, the third is between the first and the second. Try to pick out the instances when it is not. In subsequent use of the exercise, listen to the first two prices and try to quote a middle price.

A. Higher, lower, split the difference:

shs. 10	shs. 8	shs. 9
9	7	8
8	6	7
7	5	6
6	4	9
5	3	4
4	2	3

shs. 3	shs. 1	shs. 0.20
10	7	8.50
8	5	6.50
6	3	4.50
4	1	2.50
5	2	6
7	4	5.50
2	1	1.50
1.50	0.50	1.00

B. Lower, higher, split the difference:

sh. 1.00	shs. 3	shs. 2
shs. 4.00	8	6
6.00	10	8
0.10 cts.	0.30 cts.	0.20 cts.
0.20 cts.	0.30 cts.	0.25 cts.
0.50 cts.	1.00	1.75
1.00	2.00	1.50

4.

Simulate bargaining involving several exchanges of quoted prices, for:

	(usual selling price)
a large basket	shs. 3.00
a pair of trousers	shs. 45.00
3 yards of cloth	shs. 15.00
a pair of shoes	shs. 45.00
a shirt	shs. 24.00
a loaf of bread	0.60 cts.

Unit 85

1. Basic Dialogue. Settling on a price (concluded).

Patel

-vunja

to break

Nasikitika, sina senti za kuvunja. I'm sorry, I can't change (it).

Hadija

Tutafanya nini sasa?

What shall we do now?

Ikiwa huwezi kuvunja utaniuziaje

Inasmuch as you can't change (it),

kile kikapu kikubwa?

how (much) will you sell me that

big basket (for)?

Patel

Kwako wewe, toa hizo shilingi mbili. For you, pay those two shillings.

Hadije

haya

o.k.

Haya, bwana. Nitatoa hizo shilingi

O.K. (sir) I'll give the two

mbili. Lakini kesho nikija tena,

shillings. But if I come again

lázima unipunguzie zaidi.

tomorrow, you've got to reduce

(your prices) for me more.

Patel

mnunuzi (WA)

customer

bila shaka

undoubtedly

Bila shaka! Umekuwa mnunuzi

No doubt! You've become my great

wangu mkubwa. Nitakuuzia kwa

customer. I'll sell to you at a

bei nafuu.

reasonable price.

2.

Try to give the sum of the first two numbers before it is given on the tape.

A.

$2 + 1 = 3$	Mbili na moja ni	tatu
$3 + 1 = 4$	Tatu na moja ni	nne
$4 + 1 = 5$	Nne na moja ni	tano
$5 + 1 = 6$	Tano na moja ni	sita
$6 + 1 = 7$	Sita na moja ni	saba
$7 + 1 = 8$	Saba na moja ni	nane
$8 + 1 = 9$	Nane na moja ni	tisa
$9 + 1 = 10$	Tisa na moja ni	kumi
$10 + 11 = 11$	Kumi na moja ni	kumi na moja

$2 + 2 = 4$	$6 + 2 = 8$	$2 + 3 = 5$
$3 + 2 = 5$	$8 + 2 = 10$	$4 + 3 = 7$
$5 + 2 = 7$	$9 + 2 = 11$	$6 + 3 = 9$
		$9 + 3 = 12$

3.

A.

$20 + 10 = 30$	Ishirini na kumi ni	thelathini
$30 + 10 = 40$	Thelathini na kumi ni	arobaini
$40 + 10 = 50$	Arobaini na kumi ni	hamsini
$50 + 10 = 60$	Hamsini na kumi ni	sitini
$60 + 10 = 70$	Sitini na kumi ni	sabini
$70 + 10 = 80$	Sabini na kumi ni	themanini
$80 + 10 = 90$	Themanini na kumi ni	tisini
$90 + 10 = 100$	Tisini na kumi ni	mia

B.

$15 + 5 = 20$

Kumi na tano,
na tano ni

ishirini

$25 + 5 = 30$

Ishirini na tano,
na tano ni

thelathini

$35 + 5 = 40$

$45 + 5 = 50$

$55 + 5 = 60$

$65 + 5 = 70$

$75 + 5 = 80$

$85 + 5 = 90$

$95 + 5 = 100$

C.

$15 + 15 = 30$

Kumi na tano na kumi na tano ni

thelathini

$25 + 15 = 40$

Ishirini na tano na kumi na tano ni arobaini

$45 + 15 = 60$

$75 + 15 = 90$

$15 + 25 = 40$

$25 + 25 = 50$

$50 + 25 = 75$

$75 + 25 = 100$

D.

$3 + 2 = 5$

Tatu na mbili ni

tano

$50 + 10 = 60$

Hamsini na kumi ni

sitini

$25 + 5 = 30$

Ishirini na tano,
na tano ni

thelathini

$7 + 2 = 9$

Saba na mbili ni

tisa

$75 + 15 = 90$

Sabini na tano na
kumi na tano ni

tisini

$25 + 15 = 40$

Ishirini na tano
na kumi na tano ni

arobaini

$35 + 2 = 37$

Thelathini na tano
na mbili ni

thelathini na saba

$8 + 2 = 10$

$5 + 2 = 7$

$90 + 10 = 100$

$4 + 2 = 6$

$25 + 25 = 50$

$65 + 15 = 80$

$25 + 50 = 75$

$85 + 5 = 90$

Unit 86

1. Basic Dialogue. Buying trousers.

Hamisi

suruali (N)

a pair of trousers

Nataka kununua suruali.

I want to buy a pair of trousers.

Patel

kipande (VI)

a piece

Suruali ndefu au suruali kipande?

Long trousers, or short?

Hamisi

Suruali ndefu.

Long (trousers).

Patel

rangi (N)

color

Wataka suruali ya rangi gani?

What color trousers do you want?

Hamisi

~eupe

white

Nyeupe.

White ones.

Patel

kipimo (VI)

measurement

Na vipimo vyako?

And your measurements?

Hamisi

urefu (U)

length

kiuno (VI)

waist

Kiuno inchi thelathini na mbili,
na urefu thelathini na nne.

Waist 32 inches, and length 34.

Patel

-enea

to fit

Hii inakuenea.

These fit your measurements.

Hamisi

Asante.

Thanks.

- - - - -

2.

Which is greater?

A.

32 - 34	thelathini na mbili	thelathini na nne
44 - 42	arobaini na nne	arobaini na mbili
32 - 44	thelathini na mbili	arobaini na nne
42 - 34	arobaini na mbili	thelathini na nne
54 - 42	hamisini na nne	arobaini na mbili

35 - 33 73 - 65 65 - 73 84 - 92 77 - 66

B.

21 - 31	ishirini na moja	thelathini na moja			
45 - 53	arobaini na tano	hamisini na tatu			
27 - 18	81 - 41	55 - 65	46 - 43	87 - 86	63 - 65
26 - 27	97 - 96				

3.

A.

Try to give the sum before it is given on the tape.

21 + 3 = 24

Ishirini na moja, na tatu ni ishirini na nne.

31 + 3 = 34 Thelathini na moja, na tatu ni thelathini na nne.

61 + 3 = 64 Sitini na moja, na tatu ni sitini na nne.

91 + 3 = 94 Tisini na moja, na tatu ni tisini na nne.

94 + 3 = 97 76 + 3 = 79 52 + 3 = 55 47 + 3 = 50

35 + 3 = 38

B.

38 + 3 = 41 Thelathini na nane, na tatu ni arobaini na moja

18 + 3 = 21 Kumi na nane, na tatu ni ishirini na moja

19 + 3 = 22 17 + 3 = 20 58 + 3 = 61 57 + 3 = 60

72 + 3 = 75 89 + 3 = 92 99 + 3 = 102 97 + 3 = 100

Unit 87

1. Basic Dialogue. Settling the price of the trousers.

Hamisi

Bei yake ni pesa (or: shilingi) What is the price (of it)?
ngapi, Bwana?

Patel

Bei yake ni sh. 7/- na senti 75. It's 7.75.

Hamisi

Oh! Hii ni ghali sana! Oh! That is very high!

Patel

maarufu	famous
Si ghali sana. Hiyo ni suruali maarufu.	It's not very expensive those are [a] well known [brand of] trousers.
Ni ngumu sana.	They're very tough.
kitambaa (VI)	cloth, material
kisasa (Sg. VI)	modern style
Kitambaa chake ni cha kisasa.	The material (of it) is modern.

Hamisi

Hapana! Hii ni suruali rahisi tu. No! These are just cheap trousers!
-raruka to get torn
-upesini quickly
Itararuka upesi. They'll get torn quickly.

Patel

Lete sh. 6/- basi. Just pay six shillings.

Hamisi

Hiyo afadhali. Chukua sh. 6/-.

That's more like it. Here's the six shillings.

2.

A. Concords with the demonstrative stem le.

masomo	Yale masomo ni rahisi sana.	Those lessons are very easy.
somo	Lile somo ni rahisi sana.	That lesson is very easy.
kazi	Ile kazi ni rahisi sana.	That work is very easy.
nauli	Ile nauli ni rahisi sana.	That fare is very cheap.
kitabu	Kile kitabu ni rahisi sana.	That book is very cheap.
nguo	Ile nguo ni rahisi sana.	That dress is very cheap.
machungwa		
	Yale machungwa ni rahisi sana.	Those oranges are very cheap.
bei	Ile bei ni rahisi sana.	That price is very cheap.
lugha	Ile lugha ni rahisi sana.	That language is very easy.

B. Concords with the demonstrative h_o.

bei	Bei hiyo ni ghali sana.	That price is very expensive.
nauli	Nauli hiyo ni ghali sana.	That fare is very expensive.
kitabu	Kitabu hicho ni ghali sana.	That book is very expensive.
nguo	Nguo hiyo ni ghali sana.	That dress is very expensive.

C. Concords with gumu.

kitambaa	Kitambaa chake ni kigumu sana.	Her handkerchief is very heavy material.
kichwa	Kichwa chake ni kigumu sana.	His head is very hard.
kitabu	Kitabu chake ni kigumu sana.	His book is very difficult.

kazi	Kazi yake ni ngumu sana.	His work is very hard.
mtihani	Mtihani wake ni mgumu sana.	His examination is very hard.
moyo	Moyo wake ni mgumu sana.	His heart is very hard.
lugha	Lugha yake ni ngumu sana.	His language is very hard.

D. ConCORDS with ~pya.

suruali	Suruali yake mpya ilikuwa imeraruka.	His new trousers were torn.
nguo	Nguo yake mpya ilikuwa imeraruka.	Her new dress was torn.
kitambaa	Kitambaa chake kipya kilikuwa kimeraruka.	His new handkerchief was torn.
vitambaa	Vitambaa vyake vipya vilikuwa vimeraruka.	His new handkerchiefs were torn.
mbeleko	Mbeleko yake mpya ilikuwa imeraruka.	Her new mbeleko was torn.
shati	Shati lake jipya lilikuwa limeraruka.	His new shirt was torn.

3.

A. -raruka vs. -rarua.

suruali	Suruali yangu imeraruka. Nani ameirarua?	My trousers are torn. Who has torn them?
nguo	Nguo yangu imeraruka. Nani ameirarua?	My dress is torn. Who has torn it?
kitambaa	Kitambaa changu kimeraruka. Nani amekirarua?	My handkerchief is torn. Who has torn it?
shati	Shati langu limeraruka. Nani amelirarua?	My shirt is torn. Who has torn it?

B. -raruka vs. -raruliwa.

suruali	Suruali yangu imeraruka. Imeraruliwa na nani?	My trousers are torn. By whom?
nguo	Nguo yangu imeraruka. Imeraruliwa na nani?	My dress is torn. By whom was it torn?
mbeleko	Mbeleko yangu imeraruka. Imeraruliwa na nani?	My 'mbeleko' is torn. By whom?
shati	Shati langu limeraruka. Limeraruliwa na nani?	My shirt is torn. By whom?
kitambaa	Kitambaa changu kimeraruka. Kimeraruliwa na nani?	My handkerchief is torn. By whom?

4.

A goes to a shop to buy a pair of trousers. He ends by buying two, but at a reduced price.

C buys a table and four chairs, starting with the table and two chairs.

Unit 88

1. Basic Dialogue. Where is the consulate?

Maina

balozi (MA pers)

consul

Unajua ofisi ya Balozi wa Amerika?

Do you know the American Consulate?

Aramian

Ndiyo, iko karibu na Post Office.

Yes, it's near the post office.

Maina

Nitawezaje kufika huko?

How will I be able to get there?

Aramian

njia panda (N)

intersection (N)

Fuata njia hii mpaka penye njia
panda.Follow this road to where there is
an intersection.

mkono wa kulia

right hand

Halafu fuata barabara ya mkono wa
kulia.

Then follow the road on the right.

mtaa (MI)

street

mkono wa kushoto

left hand

Ufikapo penye njia panda nyingine,
fuata mtaa wa Suleman, mkono wa
kushoto, na nenda moja kwa moja.When you get to the next intersection,
follow Suleman Street, on the left,
and go straight ahead.

-ita

to call

Baadaye utacua hoteli inaitwa

Then you will see a hotel called

'Cosy Café.'

'Cosy Cafe.'

(to be continued)

2.

A. Talking about the map.

Using maps, practice pointing out places and giving their names, using the following frames:

Sehemu hii ya	Afrika Tanganyika Kenya Uganda	inaitwa _____
---------------	---	---------------

Njia	hii	(i)naitwa _____
Jimbo	hili	
Mji	huu	

Sehemu hii ya _____ inaitwaje?

Use this as an occasion to become familiar with the geography of East Africa.

Unit 89

1. Basic Dialogue. Where is the consulate? (concluded)

Aramian

Hapo mbele yako pana hoteli ya
'Cosy Café.'

Iipite.

Mbele kuna barabara ya Acacia.

Nenda moja kwa moja tu.

ñje (N)

Na mara utaona jumba kubwa mkono
wa kulia, ñje pameandikwa 'Cable
and Wireless.'

orofa (N)

Orofa ya pili ndio ofisi ya Balozi
wa Amerika.

There in front of you is the 'Cosy
Cafe Hotel.'

Go past it.

Ahead there is Acacia Avenue.

Just go straight ahead.

outside

And immediately after, you will see
a big building on the right, out-
side (of which) is written 'Cable
and Wireless.'

story

The third floor, that is the American
Consulate.

2.

A. Talking about a street map.

Practice giving directions from a number of points in Dar es Salaam to various other points, using a simplified map. Some of the words and phrases that will be most useful are:

utafika kwenye _____

moja kwa moja _____

mbele ya _____

karibu na _____

mkono wa kulia/kushoto _____

utaona _____

Unit 90

1. Basic Dialogue. Clothes for the laundryman.

Magese

Unabeba nguo, wazipeleka wapi?

You are carrying clothes on your back.

Where are you taking them?

Sangai

~chafu

dirty

dobi (MA pers)

laundryman

Hizi nguo chafu, nazipeleka kwa
dobi.

These dirty clothes, I'm taking them
to the laundryman.

Magese

Dobi yupi?

Which laundryman?

Sangai

ng'ambo (N)

on the other side

Yule aliye na duka kule ng'ambo.

That one who has the shop there on
the other side.

Magese

júmla

sum

Unazo ngapi kwa júmla?

How many do you have altogether?

Sangai

koti (MA)

coat

Zote ni suruali tatu na makoti
mawili.

Altogether there are three pairs of
trousers and two coats.

Magese

Atakutoza pesa ngapi?

How much will he make you pay?

Sangai

thumni (N)

50 ct. piece

Kama shilingi mbili na thumni.

About 2.50.

Notes

A. Abstract nouns of the U class.

~chache	few
uchache	paucity
safi	clean
usafi	cleanliness

A large number of abstract nouns are members of the u class. Frequently, except for the u prefix, they are identical in form with adjective stems.

2.

A. ng'ambo; concords with -ko.

duka	Duka lake liko ng'ambo ya mji.	His shop is on the other side of town.
soko	Soko liko ng'ambo ya mji.	The market is on the other side of town.
hoteli	Hoteli iko ng'ambo ya mji.	The hotel is on the other side of town.
kanisa	Kanisa liko ng'ambo ya mji.	The church is on the other side of town.
shule	Shule iko ng'ambo ya mji.	The school is on the other side of town.

shamba	Shamba lake liko ng'ambo ya mji.	His plantation is on the other side of town.
maduka	Maduka yake yako ng'ambo ya mji.	His shops are on the other side of town.
mashamba	Mashamba yake yako ng'ambo ya mji.	His plantations are on the other side of town.

B. Concords with ngapi; U-class singulars with plurals in the N-class.

nguo	Unazo nguo ngapi kwa jumla?	How many clothes do you have altogether?
jembe	Unayo majembe mangapi kwa jumla?	How many hoes do you have altogether?
kidole	Unavyo vidole vingapi kwa jumla?	How many fingers do you have altogether?
mzigo	Unayo mizigo mingapi kwa jumla?	How many loads do you have altogether?
ngoma	Unazo ngoma ngapi kwa jumla?	How many drums do you have altogether?
uma	Unazo nyuma ngapi kwa jumla?	How many forks do you have altogether?
ubao	Unazo mbao ngapi kwa jumla?	How many boards do you have altogether?
ukurasa	Unazo kurasa ngapi kwa jumla?	How many pages do you have altogether?

C. Kiasi gani?

wino	Una wino kiasi gani?	How much ink do you have?	
maji	Una maji kiasi gani?	How much water do you have?	
pombe	chumvi	michele	wali

3. Adjective vs. U-class (abstract) noun.

~zuri	Ule <i>ñji</i> ni <i>ñzuri</i> . Walituambia juu ya uzuri wa <i>ñji</i> .	That city is beautiful. They told us about the beauty of the city.
~chache	Walimu ni wachache <i>ñchini</i> <i>mwetu</i> . Walituambia juu ya uchache wa walimu.	Teachers are few in our country. They told us about the scarcity of teachers.
~refu	Gari la moshi lilikuwa refu. Walituambia juu ya urefu wa gari la moshi.	The train is long. They told us about the length of the train.
~eupe	Shuka zote zilikuwa nyeupe sana. Walituambia juu ya weupe wa shuka.	All the sheets were very white. They told us about the whiteness of the sheets.
~ingi	Wanafunzi wa shule ni wengi sana. Walituambia juu ya wingi wa wanafunzi.	The school pupils were very many. They told us about the [large] number of pupils.
safi	Jikoni <i>mwa</i> hoteli ni safi sana. Walituambia juu ya usafi wa jikoni.	The inside of the hotel kitchen is very clean. They told us about the cleanness of the inside of the kitchen.
~gumu	Masomo yao ni magumu sana. Walituambia juu ya ugumu wa masomo.	Their lessons are very difficult. They told us about the difficulty of the lessons.
hodari	Watoto wake ni hodari sana. Walituambia juu ya uhodari wa watoto.	His children are very clever. They told us about the cleverness of the children.

Conversation Starters

1. A asks B to go pick up his laundry for him, B asks directions for finding the place.

Reading Selection IV

Nama ya Kulima

Katika wilaya yetu Serikali imeanza kuwasaidia wakulima kwa kuwaonyesha jinsi ya kupata mavuno mengi. Wakulima wengi wanayo mashamba yaliyotawanyika mahali mbali mbali. Hawa ndio wanaoonyeshwa vile wawezavyo kuyaunganisha mashamba yao.

Katika Idara ya Ukulima wako watu walio hodari kwa ukulima ambao wanasinamia mipango hii. Watu hawa huenda mashambani pamoja na wakulima na kufanya kazi kwa mikono yao. Hii huwasaidia wenyeji kuona na kujizoeza kulima vizuri.

Shamba hugawanywa katika sehemu tatu; ya kwanza, ni kiwanja cha nyumba; ya pili ni boma la ng'ombe, kuku, mbuzi, nguruwe na kadhalika; na ya tatu ni ya kupanda mimea.

Hii sehemu ya tatu, yaani ya mimea, hugawanywa katika visehemu vidogo vingi ambavyo mimea fulani hupandwa na kubadilishwa kila mwaka.

Mimea ikibadilishwa, haichoshi udongo, na hivi mkulima aweza kulima shamba lake kila mwaka. Hii ndiyo faida ya kupanda mimea tofauti kila mara baada ya kuvuna.

QuestionsAnswers

- | | |
|--|--|
| 1. Ni wapi Serikali imeanza kuwasaidia wakulima? | Serikali imeanza kuwasaidia wakulima katika wilaya yetu. |
| 2. Serikali imeanza kuwasaidiaje? | Kwa kuwaonyesha jinsi ya kulima vizuri. |
| 3. Wenyeji wakulima vizuri hupata faida gani? | Hupata mavuno mengi. |
| 4. Mashamba ya wakulima wengi yako pamoja? | Hapana, yametawanyika mahali mbali mbali. |
| 5. Mashamba yatafanywaje? | Mashamba yataunganishwa. |

6. Kuna wakulima hodari katika Idara ya Afya?
Hapana. Watu hodari kwa kulima wako katika Idara ya Ukulima.
7. Kazi yao ni nini?
Kusimamia mipango hii.
8. Wasimamizi hawa hufanya kazi shambani?
Ndiyo, wanafanya kazi mashambani kwa mikono.
9. Hii ni faida gani?
Wenyiji huona na kuzoea kulima vizuri.
10. Shamba hugawanywa katika sehemu ngapi?
Tatu.
11. Sehemu ya kwanza ni ya nini?
Sehemu ya kwanza ni kiwanja cha nyumba.
12. Na ya pili?
Sehemu ya pili ni boma ya ng'ombe, kuku, mbuzi na kadhalika.
13. Na ya tatu je?
Sehemu ya tatu ni ya kulima.
14. Kuna faida katika kubadili mimea?
Ndiyo. Udongo hauchoki.
15. Ukiwa mkulima utabadili mimea yako?
Ndiyo, nikiwa mkulima nitabadili mimea yangu.

wilaya (N)	district, province
jinsi (N)	way, method
-tawanya	to scatter
-simamia	to stand by, to oversee
-zoea	to become familiar with
-gawanya	to divide up, distribute
kiwanja (VI)	a plot of ground
kuku (N-anim)	chicken
mbuzi (N-anim)	goat
kadhalika	likewise, similarly
kisehemu (VI)	a small section
fulani	such-and-such
-badili	to change
-chosha	to make tired
faida (N)	profit, advantage
tofauti (N)	difference, discrepancy

Unit 91

1. Basic Dialogue. Doing the wash.

Maina

-fua

to launder

Nani afuaye nguo zako?

Who washes your clothes?

Juma

Mama hunisaidia.

Mother helps me.

Maina

Yeye hufua kwa mkono au kwa mashine?

Does she wash [them] by hand or by
machine?Juma

sabuni (N)

soap

(ya) uvuguvugu (U)

lukewarm

Anatumia mikono, sabuni na maji ya

She does them by hand ('uses her

uvuguvugu.

hands') [with] soap, and lukewarm
water.Maina

-ondoa

to get rid of

Unafikiri mikono huondoa uchafu

Do you think that [washing by] hand(s)

kweli?

really gets rid of the dirt?

Juma

Sana!

Definitely!

Maina

wanga (U)

starch

Lakini anatia wanga lini?

But when does she pour in the starch?

Juma

-loweka

to wet something

Kwa kawaida, nguo ikiwa imelowekwa.

Ordinarily, when the clothes are wet.

NotesA. Relative counterparts of the a-tense.

Nani afuaye nguo?

Who washes the clothes?

Nini kiondoshacho uchafu?

What gets the dirt off?

The relative counterparts of the indicative forms of the a-tense are formed as follows:

<u>Subj. pref.</u>	<u>Stem</u>	<u>Rel. affix</u>	
ni	jua	ye	'I who know'
u	jua	ye	'you (sg.) who know'
a	jua	ye	'he who knows'
wa	jua	o	'they who know'
li	ondosha	lo	'(that) which removes'

etc.

atumiaye...

he who uses...

atumialo...

which he uses (referring to something in sg. MA class).

As in other relative forms, the relative affix may refer to and agree with the subject or the object of the verb.

2.

A. Relative counterparts of the a-tense.

kufua	Nani afuaye nguo zako?	Who washes your clothes?
kupiga pasi	Nani apigaye pasi nguo zako?	Who irons your clothes?
kununua	Nani amunuaye nguo zako?	Who buys your clothes?

B.

kulima	(Watu) walimao shamba hili wako wapi?	Where are the people who cultivate this farm?
kuhudhuria	(Watu) wahudhuriao masomo haya wako wapi?	Where are the people who attend these lessons?
kutaka	(Watu) watakao kwenda wako wapi?	Where are the people who want to go?
kujua	(Watu) wajuao Kiswahili wako wapi?	Where are the people who know Swahili?
kufua	(Watu) wafuao nguo wako wapi?	Where are the people who wash clothes?

C. -ondoa.

uchafu	Tutaondoa je uchafu katika nguo hizi?	How shall we remove the dirt from these clothes?
wino	Tutaondoa je wino katika nguo hizi?	How shall we remove the ink from these clothes?
damu	sabuni wanga	

D. -ondoka.

uchafu	Uchafu umeondoka katika nguo sasa.	The dirt is off the clothes now.
wino	Wino umeondoka katika nguo sasa.	The ink is off the clothes now.

damu sabuni wanga

3.

A. Indicative vs. relative (relative subject).

kufua	Nguo hizi zinafuliwa kila wiki.	These clothes are washed every week.
	Nani anazifua?	Who washes them?
kupalilia	Shamba hili linapaliliwa mara kwa mara.	This farm is weeded often.
	Nani analipalilia?	Who weeds it?
kuzuia	Unanizulia nisipumzike.	You prevent me from resting.
	Nani anakuzuia?	Who prevents you?

B. Indicative vs. relative (relative object).

sabuni	Tunatumia sabuni.	We use soap.
	Sabuni gani inayotumia?	What kind of soap do you use?
mafuta	Tuna mafuta.	We use oil.
	Mafuta gani inayotumia?	What kind of oil do you use?
kalamu	Tuna kalamu.	We use pens.
	Kalamu gani inayotumia?	What kind of pens do you use?
jembe	Tuna jembe.	We use a hoe.
	Jembe gani inalotumia?	What kind of hoe do you use?
wanga	Tuna wanga.	We use starch.
	Wanga gani inaotumia?	What kind of starch do you use?
wino	Tuna wino.	We use ink.
	Wino gani inaotumia?	What kind of ink do you use?

Unit 92

1. Basic Dialogue. A good-looking uniform.

Maina

mwenzi (WA)

companion

(mwenzangu)

(mwenzi wangu)

-ng'aa

to shine

Mwenzangu, nguo zako zang'aa.

Your clothes are very bright my
friend.Juma

kabla ya

before

pasi (N)

iron (for pressing)

Ndiyo. Zilitiwa wanga kabla ya

Yes, they were starched before being
ironed.

kupigwa pasi.

moto (MI)

fire

Hata pasi yenyewe ilikuwa ya moto
kweli.Besides, the iron itself was really
hot.Maina

-kauka

to get dry

Ndiyo, nguo zikisha kauka vizuri

Yes, when clothes have dried to the
right point, they iron very well.

sapigika pasi vizuri.

kifungo (VI)

button

Na hivi vifungo vyang'aa. Vimetiwa
wanga pia?And these buttons shine. Have they
also been starched?

Juma

-sugua

to polish

Hapana, lakini vilisuguliwa na
'Brasso'.

No, but they've been polished with
'Brasso'.

2.

A. ~a moto.

kahawa Kahawa hii ni ya moto.

This coffee is hot.

chai nyama

uji Uji huu ni wa moto.

This porridge is hot.

wali

B. -po- in first verb, followed by verb phrase with alikuwa haja-.

kumalisa Hasani alipofika, Ali
alikuwa hajamalisa kazi
yake.

When Hasani arrived, Ali had
not finished his work.

kwanza Hasani alipofika, Ali
alikuwa hajaansa kazi
yake.

When Hasani arrived, Ali had
not started his work.

kusema Hasani alipofika, Ali
alikuwa hajasema.

When Hasani arrived, Ali had
not spoken.

kufunga Hasani alipofika, Ali
alikuwa hajafunga
mlango.

When Hasani arrived, Ali had
not closed the door.

3.

A. Concord: Subject prefix in the first sentence, with object prefix
in the second.

nguo Nguo hisi zimekauka.
(pl.) Usisiloweke.

These clothes are dry.
Don't wet them.

shati	Shati hili limekauka. Usililoweke.	This shirt is dry. Don't wet it.
mashati	Mashati haya yamekauka. Usiyaloweke.	These shirts are dry. Don't wet them.
suruali (sg.)	Suruali hii imekauka. Usililoweke.	This pair of trousers is dry. Don't wet it.
suruali (pl.)	Suruali hizi zimekauka. Usiziloweke.	These pairs of trousers are dry. Don't wet them.
koti	Koti hili limekauka. Usililoweke.	This coat is dry. Don't wet it.
makoti	Makoti haya yamekauka. Usiyaloweke.	These coats are dry. Don't wet them.
B. <u>-ja-</u> negative verb <u>vs.</u> affirmative subjunctive verb		
kukauka	Nguo hizi hazijakauka. Yafaa zikaushwe.	These clothes have not gotten dry. They ought to be dried.
kupigwa	Nguo hizi hazijapigwa pasi. Yafaa zipigwe pasi.	These clothes have not been ironed. They ought to be ironed.
kutiwa wanga	Nguo hizi hazijatiwa wanga. Yafaa zitiwe wanga.	These clothes have not been starched. They ought to be starched.
kufuliwa	Nguo hizi hazijafuliwa. Yafaa zifuliwe.	These clothes have not been washed. They ought to be washed.

Conversation Starters

1. A is a laundryman. B discusses with him the way he wants his shirts done. He doesn't want his drip-dry shirts ironed.
2. B checks through the returned laundry with A and finds some articles missing.

Unit 93

1. Basic Dialogue. Making a bed.

Hadija

-tandika to spread

mgeni (WA) guest

kitanda (VI) bed

Asha, mtandikie mgeni kitanda. Asha make the bed for [our] guest.

Asha

shuka sheet

Uliweka blanketi na shuka wapi? Where did you put the blankets and sheets?

Hadija

ndani ya inside of

Zimo ndani ya sanduku langu. They're inside my cabinet.

Asha

godoro (MA) mattress

Sioni godoro. I can't find the mattress for the bed.

Hadija

-uliza to ask

Mulize Juma akuonyeshe liliko. Ask Juma to show you where it is.

Asha

Juma, tafadhali niletee godoro upesi. Juma, please bring me the mattress quickly.

foronya (N)

pillowcase

Bado foronya tu. Asante, Juma.

And now just the pillowcase. Thank
you, Juma.Notes

A. A verb with two objects.

Mtandikie mgeni kitanda.

Make the bed for the guest.

This verb has two objects. The first of them is translated as what we would call an 'indirect object'.

B. -uliza plus subjunctive.

Mwulize akusaidie.

Ask him to help you.

The verb -uliza may be followed by subjunctive forms, with the meaning 'to ask someone to do something'.

C. -li- as a verb stem.

Atakuonyesha liliko.

He will show you where it (the
mattress) is.

In the word liliko, the first li- is the subject prefix, the second -li- is the stem usually translated 'be', and ko is a suffix with the concord of the ku- class.

2.

A. Number agreement.

mgeni Mtandikie mgeni kitanda.

Make the bed for the guest.

mwalimu baba

wageni Watandikie wageni vitanda.

Make the beds for the guests.

waalimu

B. -onyesha plus a clause; concord: subject noun and -liko.godoro Juma atakuonyesha godoro
liliko.Juma will show you where the
mattress is.

kitanda	Juma atakuonyesha kitanda kiliko.	Juma will show you where the bed is.
shuka	Juma atakuonyesha shuka iliko.	Juma will show you where the bedsheet is.
mito	Juma atakuonyesha mito uliko.	Juma will show you where the pillow is.
mito	Juma atakuonyesha mito iliko.	Juma will show you where the pillows are.
blanketi	Juma atakuonyesha blanketi iliko.	Juma will show you where the blanket is.

C. Concord: noun subject and locative stem -mo.

↓	Vitanda vimo ndani ya nyumba.	The beds are in the house.
shuka	Shuka zimo ndani ya nyumba.	The sheets are in the house.
sanduku	Shuka zimo ndani ya sanduku.	The sheets are in the box.
mito	Mito imo ndani ya sanduku.	The pillows are in the box.
mito	Mito umo ndani ya sanduku.	The pillow is in the box.
shati	Shati limo ndani ya sanduku.	The shirt is in the box.
mashati	Mashati yamo ndani ya sanduku.	The shirts are in the box.

3.

A. Imperative with object prefix vs. subjunctive with object prefix.

kusaidia	Tafadhali, nisaidie. Mwombe Juma akusaidie.	Please, help me. Ask Juma to help you.
kupiga pasi	Tafadhali, zipige pasi suruali hizi. Mwombe Juma azipige pasi.	Please, iron these trousers. Ask Juma to iron them.
kupalilia	Nenda ukapalilie mahindi. Mwombe Juma aende akapalilie mahindi.	Go to weed the maize. Ask Juma to go to weed the maize.

kutunza	Kaa nyumbani uwatunze watoto. Mwombe Juma akae nyumbani awatunze.	Stay at home and look after the children. Ask Juma to stay and look after them.
---------	--	--

B. A-tense: indicative vs. relative.

kutaka	Watoto wataka chakula gani? Nitawauliza chakula watakacho.	What kind of food do the children want? I will ask them the kind of food they want.
kufanya	Watoto wanafanya nini? Nitawauliza kazi wafanyayo.	What are the children doing? I will ask them (what) [work] they are doing.
kusema	Watoto wanasema nini? Nitawauliza wasemalo. (cf. <u>jambo</u> (MA) 'matter')	What are the children saying? I will ask them what they are saying.
kula	Watoto wanakula nini? Nitawauliza vyakula walavyo.	What are the children eating? I will ask them (the kinds of food) they are eating.
kusoma	Watoto wanasoma vitabu gani? Nitawauliza vitabu wasomavyo.	What books are the children reading? I will ask them the type of books they are reading.
kupumzika	Kwa nini watoto wanapumzika? Nitawauliza sababu wapumzikayo.	Why are the children resting? I will ask them the reason for their resting.
kucheza	Kwa nini wanacheza? Nitawauliza sababu gani wanacheza.	Why are they playing? I will ask them why they are playing.

Unit 94

1. Basic Dialogue. The mosquito net.

Maina

Hapa katika jimbo hili pana mibu
wengi sana.

Here in this province there are very
many mosquitoes.

chandalua (VI)

mosquito net

(or: chandarua)

Hivi yatulazimu kuwa na chandalua.

Thus it's necessary for us to have a
mosquito net.

Butler

Mnabadili nguo za kitanda mara
ngapi kwa wiki?

How many times a week do you change
the bed linens?

Maina

Mama huzibadili kila Ijumaa.

Mother changes them every Friday.

Butler

usingizi (U)

sleep

-sumbua

to annoy, tease, trouble

Mkiwa usingizini, hawa mibu
wawasumbueni?

When you are asleep, do the mosquitoes
bother you?

Maina

kelele (N)

noise

Wapiga kelele sana usiku.

They make a lot of noise at night.

Butler

Nasikia kuwa mibu wa hapa waleta
malaria?

I hear that the mosquitoes (of) here
carry malaria.

Maina

Ndiyo, bwana, twasumbuliwa sana nao. Yes, indeed. We are bothered a lot
by them.

Notes

A. Pa as a subject prefix.

Note the subject prefix pa- agreeing with the word hapa.

B.

The use of the na tense (anabadili) followed in the next sentence by the hu tense raises questions about the adequacy with which the published rules concerning these tenses reflect actual usage.

2.

A. Various objects used with -badili.

kitanda	Siwezi kubadili nguo za kitanda sasa.	I can't change the bed linen now.
nguo	Siwezi kubadili nguo zangu sasa.	I can't change my clothes now.
shilingi tano	Siwezi kuvunja shilingi tano sasa.	I can't change five shillings now.
meza	Siwezi kubadili kitambaa cha meza sasa.	I can't change the tablecloth now.

B. Various verbs used with mbu as subject.

kusumbua	Mbu husumbua watu.	Mosquitoes bother people.
kuuma	Mbu huuma watu.	Mosquitoes bite people.
kudhuru	Mbu hudhuru watu.	Mosquitoes harm people.
kuletea	Mbu huwaletaa watu malaria.	Mosquitoes bring malaria to people.

3.

A. Various tenses in reported speech.

kuumia	Nilisikia kuwa uliumia mkono wako.	I heard that your hand was hurt.
	Ndiyo. Niliumia juzi.	Yes. I hurt it the day before yesterday.
kujiumiza	Nilisikia kuwa ulijiumiza mkono wako.	I heard that you hurt your hand.
	Ndiyo. Nilijiumiza juzi.	Yes. I hurt myself the day before yesterday.
kuchelewa	Nilisikia kuwa wewe huchelewa kila siku.	I heard that you are always late.
	Ndiyo. Nilichelewa juzi.	Yes. I was late the day before yesterday.
kupalilia	Nilisikia kuwa utaupalilia ua.	I heard that you were to weed the yard.
	Ndiyo. Niliupalilia juzi.	Yes. I weeded it the day before yesterday.

B. Kama in indirect questions.

kusafisha	Mama amesafisha vyombo? Sijui. Nitamwuliza kama amevisafisha.	Has mother washed the utensils? I don't know. I'll ask her if she has washed them.
kutandika	Mama ametandika kitanda? Sijui. Nitamwuliza kama amekitandika.	Has mother made the bed? I don't know. I'll ask her if she has made it.
kuchemsha	Mama amechemsha maziwa? Sijui. Nitamwuliza kama ameyachemsha.	Has mother boiled the milk? I don't know. I'll ask her if she has boiled it.

kuita	Mama amewaita watoto? Sijui. Nitamwuliza kama amewaita.	Has mother called the children? I don't know. I'll ask her if she has called them.
kulipa	Mama amelipa mafuta? Sijui. Nitamwuliza kama ameyalipa.	Has mother paid for the oil? I don't know. I'll ask her if she has paid.
kutenge- neza	Mama ametengeneza chakula cha jioni? Sijui. Nitamwuliza kama amekitengeneza.	Has mother prepared supper? I don't know. I'll ask her if she has prepared it.
kuenda	Mama amekwenda kununua sukari? Sijui. Nitamwuliza kama amekwenda.	Has my mother gone to buy some sugar? I don't know. I'll ask her if she has gone.

Conversation Starters

1. A (a housewife) discusses with B (a domestic servant) the way in which she wants the bedrooms to be maintained.
2. C and D discuss the furniture that will be needed for C's house in Tabora.

Unit 95

1. Basic Dialogue. A guest is coming for dinner!

Hamisi

-tembelea	to visit
mashuhuri	famous
Leo jioni tutatembelewa na mgeni mashuhuri.	This evening we're going to be visited by a famous guest.
Kwa hivyo Adija, tandika meza vizuri.	Therefore, Adija, set the table well.
Weka kitambaa na nyuma mbili upande wa kushoto.	Put the serviette and two forks on the left.
kijiko (VI)	spoon
Kulia kwa sahani, visu viwili na vijiko vitatu.	[To] the right of the plate, two knives and three spoons.
-sahau	to forget
Usisahau kuleta maji, bilauri, pilipili na chumvi.	Don't forget to bring water, glasses, salt and pepper.
Kwa kupakulia, tutahitaji vijiko vikubwa.	For dishing up the food, we will need some big spoons.

Hadija

Nikimaliza hayo yote nitakuita.	When I finish all those [things] I'll call you.
---------------------------------	---

Notes

1. Concord with a noun having the prefix ku.

In kulia kwa sahani, the prefix kw agrees with the ku of the preceding word.

2.

1. Location of one object relative to another.

kijiko-sahani	Kijiko kiko kulia kwa sahani.	The spoon is to the right of the plate.
sahani-kijiko	Sahani iko kushoto kwa kijiko.	The plate is to the left of the spoon.
kijiko-kisu	Kijiko kiko kulia kwa kisu.	The spoon is to the right of the knife.
kisu-kijiko	Kisu kiko kushoto kwa kijiko.	The knife is to the left of the spoon.
visu-vijiko	Visu viko kushoto kwa vijiko.	The knives are to the left of the spoons.
uma-sahani	Uma iko kushoto kwa sahani.	The fork is to the left of the plate.
sahani-uma	Sahani iko kulia kwa uma.	The plate is to the right of the fork.
nyuma-sahani	Nyuma ziko kushoto kwa sahani.	The forks are to the left of the plate.
kijiko cha supu-sahani	Kijiko cha supu kiko mbele ya sahani.	The soup spoon is in front of the plate.
bilauri-visu	Bilauri ya maji iko mbele ya visu.	The glass of water is in front of the knives.
kikombe-nyuma	Kikombe kiko kulia kwa nyuma.	The cup is on the right of the forks.

kitambaa-sahani Kitambaa kiko kushoto
kwa sahani.

The napkin is on the left of the
plate.

kikombe-kitambaa Kikombe kiko mbele ya
kitambaa.

The cup is in front of the
napkin.

3.

A. -sahau and -kumbuka.

wewe Usisahau pilipili.
Bila shaka nitakumbuka.

Don't forget the pepper.
I will certainly remember.

ninyi Msisahau pilipili.
Bila shaka tutakumbuka.

Don't forget the pepper.
We will certainly remember.

yeye Asisahau pilipili.
Bila shaka atakumbuka.

He must not forget the pepper.
He will certainly remember.

wao Wasisahau pilipili.
Bila shaka watakumbuka.

They must not forget the pepper.
They will certainly remember.

Unit 96

1. Basic Dialogue. At the table.

Hadija

Karibu mezani, Wambua.

Come to the table, Wambua.

Wambua

Starehe.

You're very kind.

~tamu

sweet, delicious

Kweli leo ina vyakula vitamu sana.

Really, you have some very delicious
dishes today.Hadija

Asante, lakini tumeishiwa siagi.

Thank you, but we've run out of
butter.Wambua

Si kitu.

Don't worry. ('It's nothing.')

-sogeza

to bring near

Tafadhali nisogezee maziwa.

Please pass the milk.

- - - - -

Hadija

Juma, tafadhali ondoa vyombo mezani;

Juma, please clear the dishes from

tumekwisha maliza kula.

the table; we have finished eating.

Juma

Ndiyo, mama.

Yes, mother.

Chai na kahawa viko (or: iko) tayari.

The tea and coffee are ready.

Hadija

bakuli (MA)

bowl

birika (MA)

pot (tea)

Leta vikombe na visahani vyake,

Bring the cups and saucers, the sugar

bakuli la sukari na birika la chai.

bowl, and the tea pot.

Juma

Ngoja kidogo.

Wait a bit.

Notes

A. Concord with two or more nouns.

Where two inanimate nouns (e.g. chai and kahawa) are the subject of the same verb, the question arises which subject prefix to use. The question is further complicated when the two nouns happen to belong to different classes (e.g. uma and jembe). Speakers differ in their practice in such situations; a final resolution of the problem must await further study.

On the tenth of next month, I'm going
to go on a trip.

Sangai

-elekea

to be directed towards

Utasafiri kuelekea wapi?

Which way are you going?

Butler

Nitasafiri kwenda mmituni
kuwinda wanyama.

I'm going to make a trip to the forest
to hunt game.

Sangai

Unakusudia kuwinda wanyama gani?

What kind of game do you plan to
hunt?

Butler

kifaru (VI-an.)

rhino

nyati (N-an.)

buffalo

simba (N-an.)

lion

tembo (N-an.)

elephant

Kama kifaru, nyati, simba, tembo na
wengineo.

[Things] like rhino, buffalo, lion,
elephant and such like.

Sangai

~kali

sharp, fierce

Hao ni wanyama wakali sana.

Those are very fierce animals.

Butler

~nene

thick, stout

Ndiyo, tena ni wanene sana.

Yes, and moreover, they are very big.

Sangai

~kuki (MI)

spear

Utawawinda kwa bunduki au kwa ~kuki?

Will you hunt with a gun, or with spears?

Butler

risasi (N)

lead, tin, solder, bullet

Kwa bunduki. Hata risasi

With a gun. I've even bought bullets.

nimenunua.

2.

A. ~ingineo

kifaru Niliona kifaru, nyati,
simba, na wengineo.

I saw rhino, buffalo, lion, and such.

walimu Niliona walimu, wanafunzi,
makarani, na wengineo.

I saw teachers, students, clerks and such.

minazi Niliona minazi, michungwa,
miembe na mingineyo.

I saw coco palms, orange trees, mango trees and such.

nguo Niliona nguo, suruali,
kofia na nyinginezo.

I saw cloths, trousers, hats and such.

sahani Niliona sahani, vikombe,
bilauri na vinginevyo.

I saw plates, cups, glasses and such.

B. Various translations for ~kali

kifaru Kifaru huyo ni ~kali sana.

That rhino is very fierce.

kisu Kisu hicho ni kikali sana.

That knife is very sharp.

pombe	Pombe hiyo ni kali sana.	That beer is very strong.
jua	Jua ni kali sana.	That sun is very hot.
mwalimu	Mwalimu huyo in mkali sana.	That teacher is very severe.
maneno	Maneno hayo ni makali sana.	Those words are very harsh.

C. nene

mtoto	Mtoto huyo ni mnene sana.	That child is very fat.
manyama	Manyama huyo ni mnene sana.	That animal is very fat.
mti	Mti huo ni mnene sana.	That tree is very thick.
mkono	Mkono huo ni mnene sana.	That arm is very thick.
ng'ombe	Ng'ombe huyo ni mnene sana.	That ox is very fat.

3.

A. The root b-d-l: badala and -badili.

kalamu	Nipe kalamu yako badala ya yangu. Nataka kubadili kalamu yangu na yako.	Give me your pen in place of mine. I want to exchange your pen for mine.
kitabu	Nipe kitabu chako badala ya changu. Nataka kubadili kitabu changu na chako.	Give me your book in place of mine. I want to exchange your book for mine.

shati kijiko foronya

B. The root s-f-r: safari and safiri.

mimi	Nilisafiri mpaka Amerika. Safari yangu kwenda Amerika. ilichukua muda wa wiki mbili.	I traveled to America. My trip to America took two weeks.
sisi	Tulisafiri mpaka Amerika. Safari yetu kwenda Amerika ilichukua muda wa wiki mbili.	We traveled to America. Our trip to America took two weeks.

yeye wao

C. The root z-d: zaidi and -zidi.

kuku	Nina kuku wengi zaidi kuliko wako.	I have more chickens than you.
	Kuku wangu wamezidi kushinda wako.	My chickens have increased more than yours.
mpunga	Nina mpunga mwingi zaidi kuliko wako.	I have more rice than you.
	Mpunga wangu umezidi kushinda wako.	My rice has increased more than yours.
pesa	watoto matata	

Unit 123

1. Basic Dialogue. May I go along?

Sangai

Nikiazima bunduki, utakubali niende
nawe?

If I borrow a gun, will you let me go
with you?

Butler

Ndiyo, ningependa mwenzi wa kwenda
naye.

Yes, I'd like a companion to go with.

Sangai

Kuwinda kwangu si kuzuri lakini
tutakwenda tu.

My hunting isn't so good, but at least
we'll go along.

Butler

umaskini (U)

poverty

Kama si umaskini tungekwenda kwa
motokaa.

If it weren't for poverty, we'd go by
car.

Sangai

mpumbavu

a fool, a dupe

Usinifanye mpumbavu bwana, pesa
unazo!

Don't take me for a fool, mister,
you've got the money!

Butler

-sadiki

to believe

Hunisadiki?

Don't ('can't') you believe me?

Sangai

-danganya

to cheat, deceive

mdanganyifu a cheat, deceiver
Hapana, mdanganye mwingine! No, cheat someone else.

Butler

Usisahau, tutaondoka baada ya juma moja. Don't forget, we're going to leave in a week.

Sangai

Kwa heri, bwana. Good-bye.

2.

A. A common way of using applied stems.

chupa	Nataka chupa ya kutilia mafuta.	I want a bottle to put some oil in.
sanduku	Nataka sanduku la kuwekea pesa.	I want a box to put some money in.
birika	Nataka birika la kutengenezea chai.	I want a kettle to make some tea in.
mtungi	Nataka mtungi wa kuchotea maji.	I want a water-jar to put some water in.
mshahara	Nataka mshahara wa kutosheleza mahitaji yangu.	I want pay sufficient for my needs.
nafasi	Nataka nafasi ya kufanyia kazi yangu.	I want a chance to do my work.
karatasi	Nataka karatasi ya kuandikia barua.	I want a sheet of paper to write a letter [on].

B. Infinitives in a noun slot.

kuwinda	Kuwinda kwake si kubaya.	His hunting is not bad.
kusoma	Kusoma kwake si kubaya.	His reading is not bad.
kuandika	Kuandika kwake si kubaya.	His writing is not bad.

kulima Kulima kwake si kubaya. His cultivating is not bad.

C.

kusema Kusema kwake kumenikasirisha. His talking has annoyed me.

kufika Kufika kwake kumenikasirisha. His arrival has annoyed me.

kulewa kuongea kulia kushangilia kuingia

3.

A. kama si

magugu Pana magugu mengi hapa. There are a lot of weeds here.
Kama si magugu, maua yako If it were not for weeds, your
yangeonekana vizuri. flowers would be seen clearly.

hatari Njia utakayofuata ni hatari The road you'll follow is very
sana. dangerous.
Kama si hatari, ningekwenda If it were not for danger, I
pamoja nawe. would go with you.

nauli Nauli ya kwenda Nairobi ni The fare to Nairobi is much.
kubwa.
Kama si hivyo, ningekwenda If it were not for that, I would
huko. go there.

miiba Njia hii ina miiba mingi. This road has many thorns.
Kama si miiba, ingekuwa If it were not for thorns, it
nzuri. would be good.

B. Numbers between 20 and 100. (Add 5 to the number in the first sentence.)

28 Nimesoma kurasa ishirini na I have read twenty-eight pages.
nane.

Mimi nimesoma thelathini na I have read thirty-three.
tatu.

37 Nimesoma kurasa thelathini na I have read thirty-seven pages.
saba.

- Mimi nimesoma arobaini na mbili. I have read forty-two.
- 46 Nimesoma kurasa arobaini na sita. I have read forty-six pages.
Mimi nimesoma hamsini na moja. I have read fifty-one.
- 59 Nimesoma kurasa hamsini na tisa. I have read fifty-nine pages.
Mimi nimesoma sitini na nne. I have read sixty-four.
- 66 Nimesoma kurasa sitini na sita. I have read sixty-six pages.
Mimi nimesoma sabini na moja. I have read seventy-one.
- 77 Nimesoma kurasa sabini na saba. I have read seventy-seven pages.
Mimi nimesoma themanini na mbili. I have read eighty-two.
- 88 Nimesoma kurasa themanini na nane. I have read eighty-eight pages.
Mimi nimesoma tisini na tatu. I have read ninety-three.

Unit 124

1. Basic Dialogue. Hunting.

Sangai

Sasa, mnyama akija nifanyeje?

Now, if any game comes, how do I act?

Butler

-ficha

to hide something

-sikiliza

to listen

Sikiliza, lazima kwanza ujifiche
asikuone.Listen, first you have to hide
[yourself] so that it can't see you.Sangai

-kimbia

to run away

Na akikimbia je? Nimpige risasi?

And how about if it runs away?

Shall I shoot it?

Butler

-lenga

to aim

Ukisha jificha, lenga bunduki.

When you've finished hiding yourself,
aim the gun.

-changa

to collect

-changanyika

to be mixed together

-chagua

to choose

ama ... ama

either ... or ...

Wakiwa wamechanganyika mchagua
umtakaye, kama nyati ama tembo.If they are all mixed up, choose the
one that you want, whether a buffalo
or a elephant.

Sangai

Halafu?

Then?

Butler

shabaha (N)

target

sawasawa

equally, just the same

Kama umelenga shabaha sawasawa, piga
risasi.

If you've aimed at the target just
right, shoot.

Sangai

-fa

to die

Mnyama akianguka maana yake anekufa?

If the animal falls, does that mean
it is dead?

Butler

Kwa kawaida, lakini usiinkimbilie.

Generally, but don't run up to him.

2.

A. Affirmative subjunctive followed by negative subjunctive.

kuficha Ilikuwa lazima wajifiche It was necessary for them to hide
ili wasipigwe risasi. so that they would not be shot.

kulala Ilikuwa lazima walale It was necessary for them to lie
chini ili wasipigwe risasi. down so that they would not be
shot.

kutoroka Ilikuwa lazima watoroke ili It was necessary for them to escape
wasipigwe risasi. so that they would not be shot.

kuangalia Ilikuwa lazima waangalie ili It was necessary for them to look
wasipigwe risasi. out so that they would not be
shot.

kukimbia	Ilikuwa lázima wakimbie ili wasipigwe risasi.	It was necessary for them to run away so that they would not be shot.
kugeuka	Ilikuwa lázima wageuke ili wasipigwe risasi.	It was necessary for them to turn around so that they would not be shot.
kupinda	Ilikuwa lázima wapinde ili wasipigwe risasi.	It was necessary for them to make a turn so that they would not be shot.

B. -changa

Bw. Hassani	Sultani anataka kuchanga fedha kwa Bwana Hassani.	The chief wants to collect money for Mr. Hassani.
askari	Sultani anataka kuchanga fedha kwa askari.	The chief wants to collect money for the soldiers.

wapagazi makarani vyakula

C. -changanya

mchele	Usichanganye mchele na mtama.	Don't mix rice with millet.
maji	Usichanganye maji na petroli.	Don't mix water with petrol.
machungwa	Usichanganye machungwa na maembe.	Don't mix oranges with mangoes.
vitabu	Usichanganye vitabu vyako na vyangu.	Don't mix your books with mine.
maua	Usichanganye maua na magugu.	Don't mix flowers with weeds.
risasi	Usichanganye risasi na misumari.	Don't mix bullets with nails.

Unit 125

1. Basic Dialogue. (continued)

Butler

-chungulia

to examine carefully

Kitu cha kwanza ni kumchungulia
kwanza.

The first thing is to take a good
hard look at him.

Sangai

-jongea

to move, make motion

-kamata

to seize

Nikiona hajongei naweza kumkamata?

If I see that he isn't stirring, can
I take hold of him?

Butler

dakika (N)

a minute

Ndiyo, baada ya dakika chache.

Yes, after a few moments.

Sangai

Kama si wewe, ningekimbilia
akianguka.

If it weren't for you, I'd have run
up to him when he fell.

Butler

-choka

to become tired

Unawaona wale wamechoka, watembea
polepole.

You see those are tired. They are
walking slowly.

Sangai

-fukuza

to pursue

-ua

to kill

twiga (N-pers)

Tuwafukuze, sitaki kuwaua twiga.

giraffe

Let's go after them. I don't want
to kill giraffe.

Butler

mbio (N)

Unafikiri unaweza mbio za twiga?

speed, running

Do you think you can [duplicate] the
speed of a giraffe?

Sangai

Siwezi, lakini napenda kumwona
akikimbia.

I can't, but I like to watch him run.

Butler

sauti (N)

Unasikia sauti za tembo?

voice

Do you hear the trumpeting of the
elephants?

Sangai

-nguruma

Ndiyo, wananguruma kwa sauti sana.

to rumble, roar

Yes, they are roaring with a great
voice.

Review Sentences, Units 1 - 125

- | | |
|---|--|
| 1. Ungependa tubadilishane kalamu? | Would you like to trade pens [with me]? |
| 2. Bilauri iliyohitajiwa iko hapa juu ya meza. | The glass that was needed is here on the table. |
| 3. Magari ya abiria yalifika saa nane leo alasiri. | The passenger lorries arrived at 2 p.m. today. |
| 4. Mtoto hataki maziwa wala maji ya machungwa. | The child doesn't want milk or orange juice. |
| 5. Ilikuwa lazima wajifiche wasishikwe na askari. | It was necessary for them to hide so as not to be seized by the policeman. |
| 6. Pale ng'ambo ya mto pamepatikana simba wengi. | Lots of lions have been found over there on the other side of the river. |
| 7. Kabla ya kuondoka tutachukua pesa za kutosha. | Before we leave, we'll take enough money. |
| 8. Choma karatasi zote zisizohitajiwa. | Burn all the papers that aren't needed. |
| 9. Mwaka ujao tutahamia huko Unguja. | We're going to move to Zanzibar next year. |
| 10. Wanafunzi wote waliojifunza huko Ulaya wamerudi makwao. | All the students who studied in Europe have returned to their homes. |
| 11. Je, wadhani atarudi hapa tena? | Do you think he will return here again? |
| 12. Itamlazimu kurudi hapa mapema sana. | He will have to return here very soon. |

13. Chakula hicho kilikuwa kimeiva sana. That food was quite thoroughly cooked.
14. Inafaa uangalie mbele unapoendesha motokaa. It's a good idea to look ahead when you drive a car.
15. Juma alisema ya kwamba, anataka nguo isiyotumiwa. Juma said that he wants brand new clothes.
16. Watu wa Ufaransa wanaongea upesi kuliko watu wa Kenya. The people of France speak more rapidly than the people of Kenya.
17. Nyumba aliyonunua ilikuwa haina mapambo mengi. The house that he bought didn't have much furniture.
18. Rafiki yangu amejiumiza kwa kisu. My friend has hurt himself with a knife.
19. Watu wengi walikusanyika katika uwanja wa mpira. Many people assembled on the football field.
20. Alifunga nyumba kwa ufunguo ili watoto wasiweze kufungua. He locked the house with a key so that the children wouldn't be able to unlock [it].
21. Amekwisha tembelea nchi zote za Afrika ya Mashariki. He has already visited all the countries of East Africa.
22. Anaweza kuongea lugha zote za Afrika ila Kiswahili. He can speak all African languages except Swahili.
23. Ukijaribu kutoroka askari atakupiga risasi. If you try to run away, the policeman will shoot you.
24. Mletee mchele badala ya nyama ya nguruwe. Bring him rice instead of pork.
25. Wao wana pesa nyingi sana. They have a very large amount of money.
26. Usimkimbize mtoto kwa mbio hivyo. Don't make the child run so fast.

- | | |
|---|---|
| 27. Wafanyi kazi wa Idara ya Elimu wananung'unika juu ya mishahara yao. | The workers in the Ministry of Education are complaining about their wages. |
| 28. Fuata barabara iliyonyoka mpaka kwenye mto. | Follow the straight road to where there is a river. |
| 29. Anakijua Kiswahili barábara. | He knows Swahili perfectly. |
| 30. Twendeni sokoni, au mjini? | Shall we go to market, or to town? |
| 31. Afadhali twende mjini. | It will be better if we go to town. |
| 32. Safari yangu ya kwenda Afrika ilichukua muda wa siku tano tu. | My trip to Africa took only five days. |
| 33. Wazazi wake ni maskini sana. | His parents are very poor. |
| 34. Anataka kalamu ya kukuandikia barua. | He wants a pen to write a letter with. |
| 35. Wasingalifanya hivyo, nisingaliwaambia waondoke. | If they hadn't done like that, I would not have told them to leave. |
| 36. Ukitaka kazi ni lázima kuitafuta. | If you want work, you have to look for it. |
| 37. Kama si wewe, ningempiga yule mtoto. | |
| 38. Chagua nguo utakayo, kama hii ama hiyo. | Choose whichever cloth you want, whether this or that. |
| 39. Ningejifunza Kiswahili ningejua kukiongea. | If I studied Swahili, I would know how to speak it. |
| 40. Hayo ndiyo niliyokuwa nikiongea juu yake. | That is what I was saying about him. |
| 41. Wakati wa joto umekwisha fika. | The hot season has already arrived. |
| 42. Alituingilia tulipokuwa tukila. | He burst in on us while we were eating. |

43. Nyumba yake imejaa mapambo ya
nyumba. His house is full of furniture.
44. Alipokuwa ametembelea jimbo la
Indiana nilifanya kazi peke
yangu. While he was visiting Indiana, I
worked on my own.
45. Penye moto hapakosi moshi. Where there is fire, there is no lack
of smoke.

Directions for use of Units 126 - 150

The last 25 units of this course are based on a series of spontaneous conversations recorded by Swahili speakers in Dar es Salaam. The editing of these texts which was done by speakers of Swahili in Washington, D. C., has been limited to the breaking up of long sentences into short ones, preserving insofar as possible the words which appear in the original. A free translation into English has been provided in lieu of grammatical notes.

It is suggested that the student listen several times to the unedited version before looking at the simplified version and translation which appear in the book. Having done so, the student may practice saying the sentences of the printed text after a tutor, with his book still closed.

Upon opening his book, the student should underline those Swahili words which are new to him, and also write them in the left-hand margin, if they do not already appear there. He should not write the English equivalent under or over the Swahili word in the body of the text.

At the next stage, the student should try to give each Swahili sentence in response to a cue taken either from the list of new words in the margin, or from the English translation. This in turn should lead to temporary memorization of 6 - 8 consecutive lines at a time.

Going beyond memorization, the student should collect, with the help of a tutor, several useful sentences containing each new word. Next, the student should listen again to the original unedited dialogue.

Finally, student and tutor may engage in a conversation which covers the same subject matter, but with no attempt at verbatim reproduction of the original.

Unit 126: Hospitali za mjini.

	Naam, Bwana Yusufu.	Hello, Yusufu.
	Naam bwana.	Hello.
tangu	Habari za tangu jana?	How are you today?
	Nzuri sana.	Very fine.
	Habari za nyumbani?	How are things at home?
	Salama tu.	Just fine.
-jisikia	Je, wasikiaje mwenzangu?	How do you feel, my friend?
-choka	Oh, nimechoka sana.	Oh, I'm very tired.
kule	Nama gani kule nyumbani?	How are things there at home?
	Hawajambo wote?	Is everyone all right?
	Watoto wote hawajambo,	All the children are fine
isipokuwa	isipokuwa mwanangu mdogo	except that my youngest
	ana homa.	has a fever.
-fikiri	Unafikiri ni homa gani hiyo?	What kind of fever do you think
		it is?
mbu	Bila shaka ni homa ya mbu.	It is undoubtedly malaria.
-wahi	Je, umewahi kuonana na	Have you seen the doctor
	daktari?	at all?
-peleka	Sasa hivi nampeleka	I'm just now taking him to the
	hospitalini.	hospital.
	Mnakwenda hospitali gani?	Which hospital are you going to?
	Tunakwenda hospitali ya	We're going to Mnazimoja
	Mnazimoja.	Hospital.
unayo	Je, unayo shilingi moja?	And do you have one shilling?
	La, sina.	No, I haven't.
gharama	Hujui kuwa kuna gharama ya	Don't you know that there is a
saa hizi	shilingi moja saa hizi?	one-shilling charge at this
		time of day?

mfanyakazi	Mimi ni mfanyakazi wa Serikali.	I'm a government employee.
huwa	Huwa sitoi gharama ya hospitali.	I don't generally pay the hospital fee.

Unit 127 (Inaendelea)

-tozwa	Hivi wafanya kazi wa serikali huwa hawatozwi pesa? Hawatozwi!	That is to say that government employees are not made to pay? They are not charged.
-danganywa	Kumbe mimi nimedanganywa siku nyingi.	Then I've been cheated for a long time.
-pata	Hujapata kwenda hospitali hata siku moja?	Haven't you ever been to the hospital even once?
mara	Nimepata kwenda mara nyingi.	I've had the occasion many times.
kila	Lakini, kila wakati nimekwenda saa tatu.	But I've always gone at 9 o'clock.
ndio	Najua saa tatu ndio wakati ambao hawatozi pesa.	I know that 9 is the time when they don't charge.
ye yote	Mtu ye yote anayefanya kazi serikalini ni lazima aende hospitali saa moja na nusu asubuhi.	Whoever works in the government is supposed to go to the hospital at 7:30 a.m.
-andikiwa	Akiandikiwa karatasi yake hupata dawa bila gharama yo yote.	If his sick sheet is signed, he gets medicine entirely free of charge.
-jitahidi	Nitajitahidi siku nyingine.	I'll try some other day.

mtumishi	Lakini, Bwana Yusufu kwa nini hata ukiwa mtumishi wa serikali unatozwa pesa?	But, Yusufu, why is one charged even when one is a government employee?
-wahi	Mimi nimewahi kulipa mara mbili au mara tatu hivi.	I've already paid two or three times.
-tegemea	Inategemea hali ya mtu mwenyewe.	It depends on the [financial] condition of the individual himself.
-lalia thamani	Kuna wengine wanataka kulalia vitanda vya thamani.	There are many [who] want to occupy the most expensive beds.
kawaida	Wengine hulalia vitanda vya kawaida.	Others occupy ordinary beds.

Unit 128 (Inaendelea)

	Vitanda vya kawaida ndivyo vitanda vya namna gani?	What are the ordinary beds like?
vile ambavyo	Vitanda vya kawaida ni vile ambavyo wanalala watu wote wasiokuwa na pesa.	The ordinary beds are those which are occupied by anyone who lacks money.
kama	Kama watu gani?	For instance?
wale	Ni wale wanaotoka mashamba.	They are those who come from rural areas.
wageni	Wako wengine wageni wasiokuwa na pesa.	There are some transients who have no money.
wale wale	Lakini, kumbuka, wale wale washamba wanaweza kulalia vitanda ghali.	But remember that some rural people are able to occupy expensive beds.
ikiwa	Wanaweza ikiwa wana pesa.	They can if they have money.

-dhani	Oh, Mimi nilidhani mtu ye yote anayetoka shamba halipi pesa! La, bwana!	Oh! I had the impression that anyone from the country didn't pay! No!
wenye	Vile vile nakumbuka kule shamba kuna watu wenye pesa nyingi.	I also remember that out there in the countryside there are people with lots of money.
tuliopo	Wana pesa nyingi kuliko hata sisi tuliopo hapa mjini.	They have more money than even those of us who are here in town.
hivyo	Bila shaka ni hivyo! Asante sana Bwana Yusufu.	No doubt about it! Thanks a lot, Yusufu.
-potezea	Sitaki kukupotezea wakati. Mtoto wako ni mgonjwa.	I don't want to waste your time. Your child is ill.
-faa	Sasa yafaa uchukue karatasi hii umkimbilie Bwana	Now it's best that you take this paper and get to the doctor in a hurry.
mganga	Mganga.	
-wezekana	Mkimbilie upesi iwezekanavyo.	Run to see him as fast as you can.
	Vyama. Nitakavyosikia nitakuja kukuambia. Kwaheri! Asante, kwaheri bwana!	All right. I'll come and tell you what I find out. Good bye! Thanks! Good bye!

Unit 129: Uuzaji wa vyakula sokoni

Karibu Bwana Juma!	Welcome, Juma!
Oh, asante sana!	Thanks!
Je, unataka nini leo?	And what do you want today?
Leo nataka machungwa bwana.	Today I'd like some oranges.

	Leo machungwa ni ghali sana.	Oranges are very high today.
	Chungwa moja ni senti kumi, bwana.	Oranges are -/10 apiece.
wakati	Unajua, siku hizi ni wakati wa mvua.	You know, this is the rainy season.
gari	Magari mengi huwa hayafiki hapa upesi.	Not many lorries get here on schedule.
uhaba	Kwa hiyo tuna uhaba wa machungwa.	For that reason, we're having a shortage of oranges.
mlimaji	Lakini walimaji wa machungwa ni wengi sana sehemu za kwenu.	But there are a lot of orange growers in the vicinity!
kwenu	Kwanini yanakuwa ghali hivi?	Why are they so expensive?
uchukuzi	Kwa sababu gharama za uchukuzi ni kubwa mno!	Because the transport charges are excessive.
ingawaje	Lakini, ingawaje gharama za uchukuzi ni kubwa mno,	But even though the cost of transportation is too high,
-chukua	huwezi kuchukua chungwa moja kwa gharama ya senti tano!	you can't sell a single orange for five cents!
	Aaaa, wewe ni rafiki yangu.	Oh well, you're my friend.
zamani	Wewe ni mnunuzi wangu wa zamani.	You've been my customer from way back.
-fanyia	Nitakufanyia chungwa moja senti tano.	I'll make you [a special price of] 5 cents an orange.

Unit 130 (Inaendelea)

Je, unataka nini zaidi -	And what else do you want?
Unataka ndizi au viazi	Would you like bananas, or
ulaya?	(Irish) potatoes?

	Oh, napenda sana viazi ulaya kama vipo.	Well, I like potatoes very much, if there are some.
vipo		
hebu	Hebu nitazame -----	Let me have a look -----
mbona	Lakini mbona vingine vidogo	But some are small and very
~embamba	na vyembamba sana.	irregular in shape.
~nene	Vingine sio vinene kama kawaida.	Some are not nice and round as [they] usual[ly are].
	Ah, bwana, sisi tuendapo madukani kununua, tunanunua	Ah, my friend, when we go to the shops to buy, we buy [them]
gunia	katika magunia.	in sacks.
-chagua	Hatuwezi kuchagua kuwa gunia hili lina viazi vikubwa au vidogo.	We aren't able to select whether this sack [or that] has large potatoes [in it].
	Lakini viazi hivi vinalimwa	But are these potatoes grown
kwenu	sehemu za kwenu, au vinatoka mbali sana?	nearby, or do they come from quite a distance?
-danganyika	Ah, watu wengi wanadanganyika.	Ah! Lots of people are fooled [by that].
	Wakisikia 'viazi ulaya,' wanadhani vinalimwa Ulaya.	When they hear 'Europe potatoes', they think they are grown in Europe.
-dhani	Hivi havilimwi Ulaya, bwana.	These aren't grown in Europe, my friend.
wenyewe	Tunavilima sisi wenyewe hapa hapa Tanganyika.	We grow them ourselves right here in Tanganyika.
	Vingine vyatoka karibu tu hapa pande za Morogoro.	Some come from right nearby, right around Morogoro.
pande	Hivi Morogoro pia kunalimwa viazi ulaya?	You mean that Irish potatoes are grown at Morogoro too?
	Naam!	Certainly!

Unit 131 (Inaendelea)

	Je, wataka nazi?	Do you want some coconuts?
	Nazi, nataka sana, kwa sababu mke wangu anazipenda sana.	Yes, I do want some coconuts, because my wife likes them very much.
	Mimi nilidhani unatumia	But I thought you used Kimbo!
Kimbo	Kimbo!	
	Kimbo sitaki, kwa sababu	I don't like Kimbo, because I
harufu	harufu yake hainipendezi sana.	don't particularly care for its smell.
	Sasa wasemaje?	Well, what do you say, Friend Juma?
-fungu	Nifunge, au unataka kununua nyama pia?	Shall I wrap [it] up, or do you want to buy some meat, too?
kifaa	Nitamunua nyama na vifaa vidogo vidogo.	I'll buy some meat and a few little items.
	Nadhani vinanitoshwa maana kikapu changu si kikubwa sana.	I think that will be enough, because my basket isn't very big.
-kaanga	Je, samaki wa kukaanga, unataka?	And do you want some fried fish?
	Siwapendi, napenda samaki wa makopo tu.	I don't like them; I only like canned fish.
kopo	Mimi naona labda hutaki	I see perhaps you don't like to
-pa	kumpa kazi nyingi bibi yako nyumbani.	give your wife a lot of work around the house.
	Bila shaka, kwa sababu juzi juzi hapa amepata mtoto.	Quite right, because just a few days ago she had a baby.
-paa	Kupaa samaki itakuwa kazi kubwa.	Cleaning fish would be a big chore.

~bichi	Unajua kuwa samaki wabichi wana vitamin?	Do you know that fresh fish have vitamins?
-faa	Pia unajua kuwa ni chakula cha kufaa kwa watoto?	And do you also know that it is good food for children?
-tiwa	Niliambiwa na mzungu mmoja kuwa wale samaki wa makopo hutiwa vitamin.	I was told by a European that that canned fish has vitamins added.
haja	Sina haja ya kumsumbua sana mke wangu.	I have no need to put my wife to a lot of trouble.

Unit 132 (Inaendelea)

~bichi	Je, maharagwe mabichi, hutaki?	And you don't want any [nice] fresh beans?
-chukua	Napenda maharagwe mabichi, nitachukua.	I like fresh beans; I'll take [some].
ulicho	Lakini, siwezi kuchukua mengi.	But I can't take many.
wewe	Nitachukua kila ulicho nacho, kidogo kidogo.	I'll take just a little bit of everything you have.
ratli	Nitachukua kwa sababu wewe ni rafiki yangu.	I'll take it because you are my friend.
taabu	Haya bwana. Sasa nifunge maharagwe ratli ngapi?	O.K. How many pounds of beans shall I wrap up?
	Ratli mbili tu zinatutosha.	Just two pounds will be enough for us.
	Wewe huoni kuja huku kila siku ni taabu?	[But] don't you find that coming here every day is tiresome?
	Ungechukua maharagwe ya kutosha kwa siku kumi!	You could take enough beans for ten days!
	Hapana, bwana, haya yana- tosha kwa leo.	No, my friend, these are enough for today.

zaidi	Nini tena zaidi, Bwana Juma?	And what else?
haja	Basi! Sina haja ya kitu kingine zaidi; asante sana.	That's all. I don't need anything else. Thank you very much.
	Haya, lete kikapu chako sawa sawa tufunge.	All right, bring your basket [hold it level] and we'll tie it up.

Unit 133 (Inaendelea)

hapa	Kikapu changu hiki hapa. Funga vizuri sana.	Here's my basket. Tie it up very carefully.
kamba	Weka kamba chini na juu.	Tie it below and above.
pikipiki	Nitakapofunga kwenye pikipiki yangu, kikapu hakitaweza kuanguka njiani.	When I tie it to my motorcycle, the basket won't be able to fall off in the street.
kumbe	Kumbe una pikipiki, bwana?	Oh, you've got a motorcycle?
-tarajia	Mimi nilitarajia kumpa mtoto akuletee nyumbani. Oh, asante, sina haja ya mtoto, pikipiki ninayo. Haya basi nitamwambia mtoto akuletee kwenye pikipiki yako ufunge.	I was intending to give it to a boy to carry home for you. Oh, thanks a lot, I don't need a boy, I've got a motorcycle. I'll tell the boy to take it to your motorcycle so that you can tie it on.
-onana	Tutaonana kesho, bwana. Asante.	See you tomorrow! Thank you.
wee	Wee mtoto, funga vizuri hapo.	You, boy, tie it well there!
nyuma	Nyuma kusiwe na matata.	There mustn't be any trouble back there!

Unit 134: Mabadiliko mjini Dar es Salaam

	Bwana Yusufu!	Yusufu!
	Naam bwana!	Hello!
	Loo, ni bahati yangu nzuri.	I'm lucky.
-ongoza	Nilidhani sitampata mtu wa kuniongoza.	I thought I wouldn't find anyone to direct me.
	Ninakwenda Msimbazi, bwana.	I'm going to Msimbazi.
tangu	Siku nyingi zimepita tangu nitoke hapa.	Many days have passed since I left here.
-fuata	Sikumbuki vyema ni bara- bara gani nitafuata.	I don't remember very well which road to take.
	Unaweza kuniongoza?	Can you direct me?
	Ulikuwa wapi siku zote?	Where have you been all this time?
mwaka	Bwana, kwa muda wa miaka mitatu iliyopita, nilikuwa Nairobi.	I've been in Nairobi for the past three years.
uhamisho	Unajua nilipewa uhamisho kutoka hapa mpaka Nairobi!	You know, I was given a transfer from here to Nairobi!
kumbe	Ahaa, kumbe! Unataka kwenda Msimbazi, sivyo?	Oh, is that so! You want to go to Msimbazi, don't you?
	Naam bwana.	Yes.
-alikwa kufunguliwa jengo	Nimealikwa kwenda kule kuhuhuria kufunguliwa kwa jengo jipya.	I was invited to go there to attend the opening of a new building.
	Jengo jipya hilo ni la Community Centre.	The new building is (of) the Community Center.

nje	Ulikuwa nje kwa muda mrefu, kiasi cha miaka mitatu.	You've been outside the country for a long time--three years.
vigumu	Nadhani itakuwa vigumu sana kwenda peke yako.	I think it would be very difficult for you to go by yourself.
-elekeza	Nitakuelekeza namna ya kufika huko.	I'll show you the way to get there.
-shukuru	Nitashukuru sana, Bwana Yusufu.	I'll be very grateful, Yusufu.

Unit 135 (Inaendelea)

forodha	Hapa ulipo ni forodhani. Forodhani--hapa najua.	Here where you [now] are is the customs house. The customs house--I know this place.
-itwa	Barabara hii inaitwa Azania Front. Ukitoka hapa Azania Front utakwenda moja kwa moja mpaka Main Avenue. Naam bwana.	This road is called Azania Front. When you leave here, you go straight ahead as far as Main Avenue. Yes.
mwisho	Halafu utafika mwisho wa Main Avenue.	Then you get to the end of Main Avenue.
pale	Pale mwisho utaona pana majumba mawili.	There at the end you will see where there are two buildings.
pahali	Jumba moja lina pahali pameandikwa 'Railway Station.'	One building has a place [where] is written 'Railway Station.'
-andikwa	Jumba jingine lina pahali pengine pameandikwa 'Police Station.'	A sign on the other says 'Police Station.'

	Naam Bwana.	Yes.
-shika	Pale Police Station utashika barabara inayoelekea	There at the Police Station you will take a road which
machweo	machweo ya jua.	runs west.
	Utakwenda moja kwa moja	Go right ahead to where there
penye	mpaka penye 'Keep Left.'	is a traffic circle.
kibao	Hapo pana kibao kilichoandikwa 'Keep Left.'	There, there is a small sign with the words 'Keep Left.'
hapo	Hapo napakumouka bwana. Ehee, pale penye 'Keep Left' pamebadilika.	I rememoer that place. That place at the circle has changed.
sura	Sura yake imekuwa mpya.	The place looks different. ('Its appearance has become new. ')
-chukua	Utachukua barabara hiyo moja kwa moja mpaka Ring Street.	You take that road straight ahead to Ring Street.
kuwa	Ulipoondoka, pale king, hapakuwa na 'Keep Left.'	When you left, they didn't have a traffic circle at King.
	Ah, hivi siku hizi pale	Oh, there is one there
ipo	ipo?	nowadays?
	Kdiyo, ipo!	Yes, there is.
hapo	Baada ya hapo, endelea tu mpaka Msimbazi Street.	From there, just continue on to Msimbazi Street.
mpya	Pale Msimbazi Street pana 'Keep Left' mpya.	There at Msimbazi Street there is another 'Keep Left.'
-tengenezwa	Hapo barabara imetengenezwa vizuri sana.	There the road has been surfaced very nicely.
kupendeza	Barabara hiyo ni safi ya kupendeza.	That road is delightfully smooth.

Unit 136 (Inaendelea)

matokeo	Loo, Bwana Yusufu, matokeo hayo yote yametokea katika miaka hii mitatu?	Say, Yusufu, all this progress has come about in these three years?
nyuma	Matokeo makubwa sana yametokea hapa nyuma.	Great progress has taken place lately.
orofa	Zipo nyumba za orofa nyingi na kubwa.	There are many and large [multi- story] buildings.
uzuri	Nyumba hizo, kidogo kama Amerika, kwa uzuri wake.	Those buildings are a little like America[n buildings] with respect to their beauty.
	Kweli?	You don't say?
kabisa	Kweli kabisa!	Yes, indeed.
pale	Tena nasikia pale Mnazimoja pamejengwa majumba.	And I also hear that buildings have been put up there at Mnazimoja.
-kubwa	Majumba hayo ni makubwa ya orofa.	Those buildings have many stories.
	Kabisa!	That's quite true.
-zidi	Sasa ukisha toka Msimbazi Street utazidi kwenda moja kwa moja.	Now, after you get past Msimbazi Street, you continue straight ahead.
kwenye	Baadaye utafika kwenye barabara inayokwenda Kigogo.	Then you will come to where there is a road that goes to Kigogo.
pana	Hapo pia pana 'Keep Left.' Vizuri sana Bwana Yusufu!	There's another circle there. Very good!
kushoto	Kwa mkono wa kushoto wa barabara ya Kigogo kuna nyumba kubwa.	On the left side of the Kigogo road, there is a large building.

Boma	Nyumba hiyo kubwa iliyo- jengwa ni Boma.	That large [recently built] building is the District Office.
-acha	Mbona Boma hilo nililiacha Acacia Avenue!	('Why, I left that Boma on Acacia Avenue!')
-hamishwa	Imekuwa kuwaje likahamishwa?	How did it happen that it got moved?
-hama	Oh, limehamishwa huko kwa sababu siku hizi mji umekuwa mkubwa sana!	It was moved there because nowadays the city has become very large.

Unit 137 (Inaendelea)

-fanya	Wanafanyia kazi gani katika jumba lile kubwa kule Acacia Avenue?	What kind of work do they use that large building on Acacia for?
	Unajua, kazi za serikali ni nyingi sana.	You know, the work of the government is very extensive.
-gawanya	Kazi hizo za serikali zime- gawanywa kwa ma - D.C.	These duties have been divided among the D.C.'s.
	Sasa ukitoka pale Kigogo, nenda moja kwa moja	Now, when you leave Kigogo, go straight ahead until you
-karibia	mpaka ukaribie daraja la Kigogo.	get near the Kigogo Bridge.
-pita	Halafu pita mkono wa kushoto wa daraja hilo.	Then bear left past the bridge.
-andika	Utaona pahali pameandikwa 'Msimbazi.'	You will see a sign saying 'Msimbazi.'
-kuta mlinzi	Pale bila shaka utamkuta mlinzi atakayekuelekeza njia.	There, you will no doubt run into a watchman who will show you the way.

ugeni	Mwonyeshe kadi yako ya	Show him your visitors card
-karibisha	ugeni na utakaribishwa.	and you will be made welcome.
	Asante sana, Bwana Yusufu.	Thanks a lot!
-wahi	Je wewe umewahi kufika katika	And you, have you ever been
jengo	jengo hilo, likoje?	in that building? What is
		it like?
-penda	Oh, ni zuri la kupendeza	Oh, it's lovely - very
	zuri sana.	beautiful.
-onekana	Je, linaweza kuonekana kwa	And is it visible from any
mbali	mbali kidogo?	distance?
umbali	Naam! Hata umbali wa	Yes! You can even see it
	maili moja unaweza	from a mile off.
	kuliona.	
-lingana	Je, Bwana Yusufu, unalilinga-	How do you compare it with
	nishaje na Arnautoglu	Arnatoglu Community Center?
	Community Centre?	
kwa	Kwa kweli siwezi kulilingani-	I can't really compare it.
	sha sana.	
	Siwezi kulilinganisha kwa	I can't compare it because
	sababu Arnautoglu ni la	Arnatoglu has been there for
siku	siku nyingi.	some time.
mazoea	Watu wamekuwa na mazoea	People have become accustomed
	nalo.	to it.
jipya	Hilo la Msimbazi ni jipya.	The one at Msimbazi is new.
matokeo	Hatujui matokeo yake	('We don't know what will come
	yatakuwa namna gani.	of it.')
	Asante sana Bwana Yusufu.	Thanks!
-ona	Nadhani tutaonana kabla	('I'll see you before I go
-ondoa	sijaondoka kurudi	back to Nairobi.')
	Nairobi.	

Unit 138 (Inaendelea)

-shukuru	Ningeshukuru sana kama ungefika nyumbani kwangu.	I'd be most grateful if you would drop by the house.
-fika	Hivyo tafadhali ufike	So please do come.
jambo	Hilo ni jambo zuri sana Bwana Yusufu.	That's very kind [of you], Yusufu!
-kawia	Lakini, kama unavyojua sisi watu wa mjini hatukawii	But as you know, we city dwellers change our
-hama	kuhama.	residence frequently.
mtaa	Hivi wakati huu uko mtaa gani?	So what street are you living on right now?
	Mini sasa ninakaa Msimbazi Street.	Right now, I'm living on Msimbazi Street.
mwenyewe	Nyumba yangu nimejenga mwenyewe.	I built my own house.
orofa	Nyumba hiyo ni nzuri na ina orofa moja.	The house is very nice, and it has an upstairs.
tajiri	Lo! Bwana Yusufu umekuwa tajiri sana.	Hey! You've been doing all right for yourself!
mara	Mara umekwisha jenga nyumba!	You've already built a house.
	Ehe, kwa sababu ya kulima!	Yes, because of farming.
-hama	Aaa, kumbe sisi tunaohamishwa kutoka hapa kwenda hapa	Ah, [yes], so those of us who are transferred hither and thither just lose out!
hasara	tunapata hasara tu.	
-furahi	Nitafurahi sana kuiona nyumba yako.	I'll be very glad to see your house.

mpango	Vyema! Na nitakueleza mipango mingi.	Fine! ('I'll fill you in on all the details!)
--------	--------------------------------------	---

Unit 139: Duka la nguo

	Habari Bwana Salumu?	How are you, Mr. Salumu?
	Oh, nzuri sana, Bwana Juma.	Oh, very well.
	Karibu bwana!	Come in!
	Asante sana, bwana!	Thanks very much.
-fungua	Karibu bwana! Siku hizi nimefungua duka kubwa sana.	Come in! In the last few days I've opened a large store.
duka	Ni duka la nguo, vitu vya kula, na vitu vingine mbali mbali.	It's a [combination] dry goods store, grocery, and general emporium.
mbali mbali	Kuna nguo gani unauza?	What kind of clothes do you sell?
kuna	Kuna nguo za aina nyingi ambazo ninauza.	There are a lot of kinds that I sell.
aina	Ninauza kanga, shuka za kitanda, mashati fulana za ndani, na fulana ndogo za watoto.	I sell kangas, bed linens, shirts, undershirts and baby clothes.
kanga	Pia ninauza nguo nyingine nyingi.	I also sell many other [kinds of] clothes.
fulana za ndani	Nimepata nguo hizo kutoka Mombasa.	I've gotten these dry goods from Mombasa.
-toka	Nguo hizo niliziagiza.	I ordered those goods.
-agiza	Nataka nguo za watoto - kaptura na shati.	I want some children's clothing- shirts and shorts.
kaptura	Tena ningependa mashati mawili, yangu mimi mwenyewe.	I'd also like two shirts for myself.
mini		

	Vile vile ningependa suruali	I'd also like two pair of
khaki	mbili za kaki ya Amerika,	trousers [made] of American
	na koti moja.	khaki, and a coat.
	Je, una fundi anayeweza	Do you have a tailor who can
-shona	kushona koti?	make a coat?
mwenyewe	Ah, mimi mwenyewe na mke	Oh! My wife sews, and so do I.
	wangu tunashona.	
	Baada ya kufunga duka,	We do this work ourselves
-fanya	huzifanya kazi hizi	after hours.
	sisi wenyewe.	
	Huwa tunazifanya bila ya	We ordinarily do it without
taabu	kupata taabu ya kumpa	the bother of giving [it]
	fundi.	to a tailor.
	Lakini kumbuka kuna	But bear in mind that we also
	nyingine ambazo	have other [clothing] which
kwisha	zilikwisha shonwa kabisa.	is ready-made.
hebu	Hebu jaribu moja katika	Try one of these.
	hizi!	

Unit 140 (Inaendelea)

	Bwana, wasema 'nguo iliyo-	[But] they say that a ready-
-stiri	shonwa haistiri mtu.'	made garment does not cover
		one properly.
	Nisingependelea kuchukua	I wouldn't like to take a
-penda	nguo iliyokwisha shonwa.	ready-made garment.
	Ningetaka kupima mimi	I'd like to be measured in
-pima	mwenyewe.	person.

mawazo	Oh, kumbe bado una mawazo	Oh so! You still have old-
kizamani	yale yale ya kizamani!	fashioned ideas!
-vaa	Tazama shati nililovaa mimi.	Look at the shirt that I'm
		wearing.
Japan	Shati hili limetengenezwa	This shirt was made in Japan.
	Japan.	
	Shati hili ni zuri na la	This shirt is nice
-penda	kupendeza sana.	and very good-looking.
-chukua	Kushona kwake kunachukua	Sewing it takes a long time.
	wakati mrefu.	
	Shati, kama unavyohitaji	A shirt, as <u>you</u> want it, you
wewe	wewe, hulipati mpaka	won't get before tomorrow.
-pata	kesho.	
	Lakini, ukitaka lililoshomwa	But if you want a ready-made
tayari	tayari, unanunua na kuvaa	shirt, you buy it and put
pale pale	pale pale.	it on right on the spot. .
	Kweli, lakini kabla	True, but before we go any
-enda	hatujaendelea mbele,	further, what do you think?
-ona	waonaje Bwana Salumu!	['how do you see?']
ile ile	Bei hii ni ile ile kama ya	Is this price the same as
	mwezi jana?	last month's?
-panda	Au bei hii imepanda kidogo.	Or has it gone up a little?
ushuru	Nasikia kuwa ushuru wa	I hear that the customs duty
forodha	forodha umepanda siku	has gone up recently.
	hizi.	
	Kwa kuwa ushuru umepanda	Because of the fact that the
kuwa	bei ya nguo imekuwa ghali	duty has increased, the price
	sana.	of clothes has become very
		high.
	Je, vipi?	What about that?
-angalia	Usiangalie hayo; ni maneno	Don't pay any attention to
maneno	ya watu tu.	that! It's only a rumor.

hotuba	Watu wengine hawakuweza kuelewa ile hotuba ya Waziri Mkuu.	Some people misunderstood that speech of the Prime Minister's.
--------	--	--

Unit 141 (Inaendelea)

maana	Waziri Mkuu alisema 'Bei ya vitu itapanda.' Lakini watu wengine hawakuelewa maana ya maneno hayo.	He said, 'The price of things is going to rise.' But some people didn't understand the meaning of those words.
maadam -panda -panda	Maadam Bwana Waziri alisema bei itapanda, walianza kupandisha bei.	Because the minister said that prices would rise, they began to raise prices.
kila mara	Lakini mimi kila mara nilikuwa nikienda kwenye Baraza la Taifa.	But I was attending the National Assembly regularly.
-sikia mapato	Nilikuwa nikienda kusikiliza wanasema nini juu ya mapato.	I was going [in order] to listen to what they say about income.
-panda wakati	Kwa sababu hiyo sikuweza kupandisha bei yangu. Wakati huu bei ni ile ile.	For that reason I couldn't raise my price[s]. At the present time the price is the same.
faida kwa	Napata faida ndogo sana. Napata senti ishirini na tano au thelathini kwa kila shati.	I make a very small profit. I make 25 or 30 cents on each shirt.
kwanza humu	Kumbeka! Nadhani hii ni mara yangu ya kwanza kuingia humu dukani.	Really, I think this is my first time to be in this shop.

mwananchi	Hili ni duka la mwananchi ambaye mpaka sasa	This is the shop of a fellow African who up to now hasn't raised prices.
-panda	hajapandisha bei.	
-fahamu	Nafahamu, Bwana Salum, kuna wananchi wachache sana	It seems to me, Salum, that there are very few Africans who have shops.
wenye	wenye maduka.	
	Hivyo basi, wewe ulikuwa kutopandisha mtu wa kwanza kutopandisha bei.	And so you were the first person not to raise prices. [-to- is used to form negative infinitives. It stands immediately after ku-.]
Waarabu	Waarabu wamekwisha pandisha mahali bei kila mahali.	The Arabs have already raised prices everywhere.
hebu	Hebu, Bwana Salumu, kuna nguo za wanawake?	Well, then, Bwana Salumu, do you have women's clothes?

Unit 142 (Inaendelea)

	Nguo za wanawake ni hizi hapa.	The women's clothes are these here.
	Nyingine unaweza kuvaa hivi hivi hivi hivi kama kanga.	Some you can wear just like a kanga.
	Siku hizi bwana tunataka mavazi ya nchi za magharibi.	Nowadays we like Western clothing.
vazi		
kwa	Ningependa gauni mbili kwa bibi yangu.	I'd like two dresses for my wife.
itakiwavyo	Je, fundi wako anaweza kushona vizuri itakiwavyo?	And can your tailor sew as nicely as required?
	Oh, kabisa! Pia kuna mishono mingi.	Oh, by all means! Besides there are many styles.

kibwebwe	Kuna mshono wa kibwebwe na mingine mingi ya kila aina.	There is the kibwebwe style, and many others of every kind.
mkeo	Mshono gani mkeo anapenda?	What style does your wife like?
mchinjo	Naona kama anapenda mchinjo.	I think she likes the mchinjo style.
	Waelewa mchinjo ni nini bwana?	Do you understand what mchinjo is?
hitaji	Naelewa sana, maana mahitaji ya watu wengi nayapata hapa.	I know very well, because I (‘deal with’) the needs of many people here.
	Aha! Basi nataka mchinjo. Mpime, bwana.	Aha! Then I want mchinjo. Measure her, please.
kifua	Nampima kifua thelathini na sita.	I measure [her] bust [at] 36.
kiuno	Pia nampima kiuno ishirini na sita.	And [her] waist at 26.
bega	Pia nampima mabega kumi na nane.	And [her] shoulders at 18.
urefu	Urefu wataka, tuseme, kama arobaini na moja?	The length you want, let's say, about 41?
	Tuseme mpaka hapa. Ina- tosha.	Let's say to here. This is all right.

Unit 143 (Inaendelea)

